Kristo Ni Siri Ya Mungu Iliyofunuliwa

Jeffersonville, Indiana, Amerika
Julai 28, 1963

1 Asante, Ndugu Neville. Bwana akubariki. Bakini mmesimama kwa muda mfupi tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu kwa maombi

2 Baba wa rehema wa Mbinguni, tunakujia Wewe tena asubuhi hii kwa ajili ya rehema na kwa ajili ya uongozi wa Roho Mtakatifu leo, kama tulivyojiliwa na siku hii ili kukutana pamoja asubuhi hii na kufundisha Neno Lako, na kwamba tutaweza kujua jinsi ya kuishi katika siku hii ya leo, na ni wakati gani wa siku ambao tunaishi. Tungeomba uongozi Wako mtakatifu wa mawazo yetu, mioyo yetu leo, kwamba Wewe ungetuelekeza kwa kila Neno ambalo ni muhimu kwetu sisi kulijua; kwamba ungefungua midomo yetu na mioyo yetu kwa unyofu, vilevile, kupokea, na kile ambacho Wewe utasema nasi na kifunga midomo yetu kwa mambo yale ambayo si sawa, tukijua kuwa ni Wewe pekee uwezaye kufunua Neno la Mungu.

Na sasa nitaliacha hili kanisa dogo sasa niende sehemu nyingine za ulimwengu, nawaweka Kwako, Bwana. Wao ni kama kusema wao ni sehemu, mboni ya moyo wangu. Wao ni-ni wale waliozaliwa kwako, kwa Roho na kwa Neno la Kweli. Nami naomba kuwa Wewe utawabariki, Bwana, na kuwaweka wamesukwa pamoja kwa vifungo vya upendo wa Kristo.

3 Mbariki mchungaji wetu mpenzi, mchungaji wa kondoo. Twaomba kuwa utampaka mafuta kwa Roho Mtakatifu, wa Neno Lako, na kuwafunulia na kulisha hili kundi.

Na mara, muda mfupi tu uliopita, ulipoonyesha ono, Hekalu dogo hapa, pa kuweka chakula, kwamba kungekuja wakati hili lingehitajika. Tulipomwona Ndugu Sothmann na Ndugu Woods tayari kuvuka kwenda nchi nyingine, ku.... Lakini Wewe ulisema, "Weka hiki chakula ghalani hapa kwa ajili ya wakati".Bwana, kwa heshima nimejaribu kufanya hilo.

Na sasa, asubuhi hii, katika somo hili ambalo tumeliwazia, naomba kwamba utalifunua lote, Bwana, kuonyesha kuwa wewe ni Mungu, na hili ni Neno Lako na Kweli Yako.Tujalie,Bwana, kwamba watu wataweza kula pale na kunenepa,kama ilivyokuwa, katika neema ya Mungu, kwamba wangeona ya kuwa ni rehema kuu za Mungu kwetu katika siku hii. Wabariki wote waliopo hapa na wale ambao wangependa kuwepo, Baba. Ujipatie utukufu Mwenyewe, kwani tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

4 Nami ninaamini kabla tu hatujaanza tuna mtoto mdogo hapa wa Collins.

Nilikutana na baba yake muda mchache uliopita, na-naye alikuwa na mtoto mdogo aliyetaka awekwe wakfu. Nasi tunataka kufanya hilo sasa, ikiwa Ndugu au Dada Collins, mmoja, atamleta huyo mtoto mbele ili tuweze kuwa na huduma ya wakfu kwa ajili ya huyu mtoto mdogo.

5 Kuacha, unajua, mbona, inasababisha ... kwa kuwa hawa ni washiriki waaminifu au ... wa Mwili wa Kristo. Mnajua, kamwe sikusema "wa Hekalu." "Wa miili ya Kristo, " ule.. huu mwili hapa, sehemu ya Mwili Wake.

Na wanaye mtoto mdogo hapa waliyetaka awekwe wakfu. Na-ni hii siku zote nafikiri ni kazi m-mke wangu ananionea wivu, kushika watoto Loo! Naye Ndugu Neville, uje huku mbele ikiwa utaweza.

6 Jina lako la kwanza ni nani ndugu? [Yule baba anasema "Clyde." - Mh.] Huyu ni Ndugu na Dada Clyde Collins, ni kaka kwa ndugu yetu wa thamani hapa, Mchungaji Collins, Wilbur. Na wamekuwa na ongezeko la idadi ya akina Collins hapa, naona, na mtoto mdogo mwenye akili sana.

Ana umri gani, Dada Collins? [Mama anasema, "Karibu miezi minne." - Mh.] Karibu miezi minne. Naye anaitwa nani? [Mark David Collins."] Mark David. Hilo ni jina zuri. Anaonekana kama mvulana mzuri sana. Sema ni aina ya mvulana mkubwa vile vile.

Basi najua akina mama hapa wanaweza kupendezwa na huyu mtoto mdogo hapa. Je, huyo siyo mwanasesere? [Ndugu Branham anamyanyua Mark David juu mbele ya

kusanyiko - Mh.]

Vema, tuinamishe vichwa vyetu sasa

7 Baba wa Mbinguni, huyu baba kijana na mke anapokuja pamoja na huyu mtoto, bonge la thamani la mwili wa binadamu ambao wamepewa kwa muungano wao na kuweka mikononi mwo kutunza kwa ajili ya Bwana Mungu. Kwa heshima wanamleta mtoto Mark David hapa kwa ajili ya kuwekwa wakfu kwa Mwenyezi, Ambaye ametoa huyu mvulana mdogo wa thamani, mwenye afya njema na mvulana mzuri, wamtunze wamkuze kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Bwana, mbariki baba na mama. Lile pipa kamwe lisiwe tupu nyumbani au chupa isikauke kamwe. Baba awe mzima na mwenye uwezo Bwana, afanye kazi na kutengeneza chakula kwa ajili ya huyu mtoto; mama awe mzima na aweze kukitayarisha; na mioyo yao tayari, Bwana, kumfundisha huyu mtoto, kumkuza katika onyo la upole la Mungu. Tujalie Bwana.

8 Sasa akitoka mikononi mwao kuja kwenye mikono yangu, anakuja huyu mtoto mzuri, Mark David. Na namleta Kwako, pamoja na mzee wa kanisa hapa, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya maisha yake. Aweze kuishi maisha marefu, hadi huku Kuja kwa Bwana Yesu, ikiwa hilo litakupendeza Wewe. Na ikiwa ni hivyo, anaweza kuweka Ujumbe wa Bwana Mungu, katika kipindi kijacho. Tujalie. Mpe afya njema, furaha, na moyo wake siku zote ukae katika kutenda mambo yaliyo sahihi mbele za Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo, tunakupa Wewe huyu mtoto, katika kumweka wakfu. Amina.

Bwana akubariki. Bwana akubariki, Dada Collins, na huyu mvulana mzuri, nawe Ndugu Collins. Bwana awe nanyi.

"Walete," sote pamoja.

Walete, walete,

Toka maporini ya dhambi;

Walete, walete,

Walete watoto wadogo kwa Yesu

9 Nalipenda hilo. Unaona, walete kwa Kristo kabla hata shetani hajawa na nafasi. Tayari wameshapelekwa Kwake basi kwa ajili ya maisha ya huduma.

Kuna yeyote ajuaye kama familia ya Dauch, mmoja wao, amekuja leo, au la, Dada Dauch? Ndugu Brown, uko hapa, Ndugu Brown? Ndiyo, nashukuru. Na ile... Je, Ndugu Dauch bado yu pamoja nasi? Vizuri sana! [Ndugu Tom Brown anaeleza kuhusu hali ya ndugu William Dauch -Mh.] Ndugu Dauch kidogo atutoke. Unaona, hatuwezi kusema mengi au kuomba sana, yeye tayari amekwishapitiliza kwa miaka ishirini na mmoja zaidi ya ule wakati Mungu aliomwambia angeishi. Hayo ni maisha ya kawaida. Hayo ni maisha ya kawaida zaidi ya ule wakati ambao Mungu alimwambia angeweza kuishi.

10 Lakini tulipigiwa simu asubuhi iliyopita, ya kuwa alikuwa-alikuwa anakufa, na tuliharakisha kwenda kule. Naye Bwana Mungu alikuwa mwema kweli kwake, alimnusuru. Nafikiri tu yeye-yeye yuko tayari na anasubiri tu Kuja kwa Bwana. Lakini, unajua, tunashikana mmoja kwa mwingine. Sisi tu .... Yule mtu mzee ni kama-kama baba kwangu hapa.

Namkumbuka akikaa hapa hapa katika Hekalu la zamani, ile sehemu ya zamani, wakati yeye... ile Nuru ilipoangaza, juu ya ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo, yeye alitokea moja kwa moja pale. Na kwenye miaka themanini na saba au themanini na ne, na fimbo, akaja moja kwa moja hapa na kusema, :Nataka kwenda moja kwa moja ndani pale na kubatizwa." Mtu fulani alikwenda na kumletea nguo. Yeye hakuweza kusubiri mpaka wakati mwingine; ilimpasa aje moja kwa moja wakati ule, moja kwa moja wakati ule. Kwa hiyo na-napenda hilo.

Siku moja alisema, nilikuwa nikiongea naye, akasema, "je, unafikiri niko salama sasa Ndugu Branham?"

Nikasema, "Uliwahi kwenda kwa daktari kwa ajili ya uchunguzi wa mwili?" Akasema, "Ndiyo, bwana."

Nikasema, Daktari ataweka stirioskopu ya kupimia mapigo ya moyo katika masikio yake, na kuziweka juu ya moyo wako, aone ikiwa moyo wako unakwenda vizuri; na

kadiogramu ya umeme ya kupima moyo, na msukumo wa damu, kupima mkojo, na kadhalika, vifaa, kujua hali ya mwili wako. Sasa, jinsi anavyofanya hilo, anatazama kwenye-kitabu hapa, pale wachunguzi wa elimu maalum kwenye masomo mbalimbali walikoandika, "ikiwa hili litatokea, hiki ndicho chenye kasoro".

11 Nami nikasema, "Sasa, darubini pekee niliyonayo ni Biblia, unaona, kwa ajili ya nafsi". Na nikasema, "Nakwenda kukuchunguza., Nikasema, "Mtakatifu Yohana 5:24, ilisema, 'Yeye asikiaye Maneno yangu.' Nikasema, "Hiyo siyo kukaa tu na kusikiliza. Hiyo ni kulipokea, unaona kulipokea; unaliamini. Kitu fulani ndani yako kinakuambia Hilo ni sahihi,. Umelipokea, uliamini, ni lako. Yeye asikiaye, 'tayari ni lako, "Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka. "Unaamini hilo?"

Yeye akasema, "Naamini,"

Nikasema, "Basi nitakuambia kile alichosema Daktari Mkuu Yeye amepita kutoka mautini kwenda uzimani, na hataingia tena hatiani au hukumuni." Nikasema, "Kadiri nijuavyo kufuatana na Vitabu umefaulu mtihani.

Yule mzee, wa karibu miaka mia, akiwa siyo mtu wa kanisa hata kidogo; ila tu kwa mara ya kwanza ile Nuru ilimulika katika njia yake, akalipokea. Unaona ile mbegu iliyochaguliwa kimbele imekaa pale? Loo! Ndiyo, bwana. Tazama, mara tu ile Nuru ilipoigonga, inakuja kwenye Uzima mara moja.

12 Sasa, najua kuwa leo kuna joto, na ni kama ni vigumu kwangu kuwaita, ninyi pamoja kwa ajili ya ibada ambapo mnakaa mmejazana kiasi hiki. Lakini bado nili-nilifikiri, kwa neema ya Mungu, kwamba ningekuwa na ibada nyingine kabla sijawaacha ninyi nyote; kwa muda mfupi, naamini.

Na inanibidi niende sasa kesho usiku, Chicago, kuanza Jumatano. Nilifikiri ningekuwa pale mapema kidogo, kama inawezekana na kupumzika kidogo kabla ya kuanza mfululizo wa ibada. Nami naamini wanayo ... Nilikuwa nikiiangalia hapa. Ime-imetangazwa juu kule. Inaitwa Marengo ... [Mtu fulani anasema, "Marigold." -Mh.].... eneo, naam anasema, "Marigold, naam, eneo la uwanja wa michezo. Uwanja wa Marigold ndipo utakapofanyika, kuanzia Jumatano usiku, mpaka Jumapili. Na Full Gospel Business Men walikuwa na kifungua kinywa vilevile, Ju-Jumamosi asubuhi. Nami sijui wapi hasa walipotangaza. Hapana. Baadaye Jumamosi jioni itakuwa kule Lane Tech. Naona ime-imetangazwa hapa.

13 Sasa, ikiwa upo eneo lile, au juu kule, itakuwa ibada ya kiinjili ya kawaida, ya kawaida kama tunazokuwa nazo wakati wowote. Nyingi ya Jumbe kimsingi zitakuwa juu ya jambo ambalo limefundishwa hapa, kwa sababu hapa ndipo tumerekodi kanda zetu, unaona. Nje kule wanaweza kufanya fujo. Lakini ikiwa watapenda kanda zilizorekodiwa hapa, hiyo ni juu yao ikiwa wanataka kusikiliza kanda yoyote. Inatoka hapa hapa. Hii ni mimbara yetu wenyewe.

Kwa hiyo nje kule, kwa kawaida huwa najaribu kuchukua jambo ambalo sio la ndani sana, kwa kuwa wengi wao wana uzoefu mdogo na kile kilichoingia. Lakini hapa najisikia nina haki kusema chochote kile Mungu anachoweka moyoni mwangu, nikiseme kutoka hapa hapa. Kwa hiyo kanda zetu zote zinatengenezwa hapa hapa. Unaona? Nao wako pale chumbani sasa, unaweza kuona vichwa vyao juu ya vioo vya mawingu ndani pale, ambapo wamekaa na vinasa sauti vyao.

14 Basi, na ikiwa unataka kuja kwenye mkutano, tutafurahi sana kuwa nawe. ikiwa utafika tu pale, na hujui tu mahali pa kwenda, basi wasiliana tu na watu wa Full Gospel, au-au Ndugu Carlson, na ata-atakwambia, au lile Kanisa la Philadelphia, au yeyote kati yao, wanaweza kukwambia jinsi ya kupafika pale mahali.

15 Basi nitarudi Jumatatu ijayo jioni, kwenye mchana au jioni. Na Jumanne tunarudi Arizona kwa ajili ya kuwapeleka watoto shule, na kadhalika. Nami sijui ni lini tu hasa nitarudi tena, kwa sababu, namtaka Bwana Yeye aniongoze juu ya kila kitu cha kufanya.

Jambo la ajabu sana lilitokea. Ningeweza vilevile... Najua hili linanaswa, kwenye kanda na naweza vile vile kuliingiza hapa. Na pale maono na maongozi ya Roho Mtakatifu yanaendelea, napenda nilenge pale hasa Yeye anapopita. Hiyo ni ... Basi, mwaka uliopita kumekuwa na moja, mojawapo, kati ya nyakati kuu sana za maono nilizowahi kuwa nazo, katika huduma yangu yote ni huu mwaka uliopita, juu ya mambo ambayo yametokea tayari, yale ambayo ninyi watu mnajua kuwa linaelezwa kimbele kabla halijatokea, na lilitokea jinsi tu li-livyosema.

16 Sasa, tunarudi hapa, na-ni kuzuru. Tabia ya nchi katika sehemu hii, hakika siipendi, kwani mimi ni.... hunishinda mara tu ninapofika hapa. Na nina .... Naweza kuvuka juu ya vinubi juu kule na kuja chini kwenye hili bonde, na niwe hapa kwa karibu dakika kumi napata ugonjwa wa mabaka ngozini, naugua. Hali ya hewa, kizunguzungu, kila kitu kinakuwa kizuka, weusi, na nina-ninataka nitoke tu katika hilo. Unaona?

17 Na siku ile nyingine nilikuwa nikiongea na mke wangu .....

Lakini nini kinanileta hapa, kwanza, kitu gani kinanileta hapa, ni ninyi watu, unaona, hili kanisa. Nawaambia, kati ya mahali pote nilikowahi kwenda katika maisha yangu, hapa ni mahali pangu ninapopenda zaidi kuja na kuhubiri Injili. Na inaonekana kuwa tunaweza kutengeneza kanda kutoka hapa ambazo ni nzuri mara kumi kuliko mahali pengine pote. Unaona? Tazama, hiyo ndiyo sababu nasema, "Pale ambapo Mungu anatenda jambo fulani, basi udumu hapo hapo pamoja nalo". Lakini nafikiri, pale mambo makuu yaliko, ndiyo sababu niliposhindwa kwenda nje kwa mara ya kwanza. Yeye aliponiita, ndiyo sababu ananisababishia hali ngumu ninapokuja hapa. Utii ni bora kuliko dhabihu.

18 Na ndipo nitakuwa nikija na kurudi wakati wote, nikihubiri Hekaluni. Na ninyi watu mnaotoka nje ya mji mtafahamishwa. Billy Paul atakuwa hapa, hapa ofisini, na-ninaweza kupatikana wakati wowote , kupitia yeye. Na tutakuja hapa, kuwa..... Na ndipo zile Baragumu Saba zitakuja moja kwa moja, Bwana akipenda, Mapigo Saba ya Mwisho, na vile Vitasa, na kadhalika, tutakavyoweza tu, tukipata hali ya hewa ya baridi, labda, au jambo fulani, vyovyote Bwana atakavyoongoza.

19 Na sasa, siku moja, nikiingia, kulikuwa na swali lililoletwa kuhusu jambo fulani, kuhusu mtu fulani aliyenipa hu-hundi, na ilisema "binafsi," kwangu tu mimi hasa, na mimi pekee, "ililipiwa ushuru, bure," kila kitu kinginecho. Vema, tulikwenda na Billy alijua nilihitaji ile hundi sasa.

Yeye alikwenda na kuuliza wanasheria iwapo tungeweza kulipwa fedha taslimu kwa kutoa hundi. Akasema, mbona yeye ni raia wa Marekani. Kwa nini asilipwe fedha taslimu?" Mnaona, kasema, "imeshalipiwa ushuru, na kila kitu kingine; bure.' Raia yeyote anaweza kufanya hivyo."

20 Hivyo basi Billy asingetosheka na hilo, kwa hiyo alikwenda kwa mtunza hesabu wa serikali. Akasema, "Kwa nini, hakika, yeye anaweza kulipwa fedha hizo." Kasema, "Yeye ni raia wa Marekani."

Kwa hiyo, vema yeye hakuweza kufikiria hilo, kwa hiyo akampigia simu Marle na Miller, ambaye ni mkuu wa-wa shirika la kodi kule-kule Indianapolis, walikuwa mawakili wetu, hivyo Ice na Miller. Kwa hiyo "Hakika ni vyema. Unaona? Hakika yeye anaweza kuchukua hiyo hundi. Ime-ime-imeandikwa kwa ajili yake, mweka sahihi tu.'" Naweza, ni mmoja tu awezaye kutia sahihi, kadhalika, na isingeweza kupigwa muhuri wa kwetu.

21 Tazama, sichukui pesa kwa hundi. Hilo ndilo walilonipatia wakati ule. Mtu fulani analeta furushi la hundi, na kusema, "Hapa, Ndugu Branham," mkutanoni. Ningesema, William Branham, William Branham ,,,, " Vema, serikali ilikuwa inashughulikia yote hayo, wakati wote. Nami nilikuwa nikizitia sahihi, mwenyewe na kulipa madeni nje kule, lakini walisema nilidaiwa kodi za hatia juu ya hizo zote, kwa vyovyote, dola laki tatu. Kwa hiyo-kwa hiyo hapo ndipo ulipokuja usumbufu.

Kwa hiyo ndipo mara nilipoingiza benki hii hundi, lo, anakuja hapa karani anasema "Tutamfungulia tena mashtaka sasa." Kwa hiyo itafanya hali fulani ya ugumu.

22 Naye Ndugu Lee Vayle akiwa ameketi hapa, nadhani ni sahihi kulisema, sisi tu ... Yeye alikuwa ameteremka chini, na huyu Mbaptisti mzuri msomi hapa alikuwa ... Nilimbatiza katika Jina la Yesu Kristo, hapa katika kisima siku ile nyingine. Ndugu Lee Vayle. Naye ni mtu mzuri hasa, ndugu katika Kristo. Aliwahi kutuhubiria hapa hapo awali na kitaaluma anayo elimu ya juu na, mbali na hiyo mtu anayeongozwa na Roho. Wakati ile Nuru ilipomwangazia, alisema alijaribu kutoroka lakini asingeweza kufanya hivyo, kwa hiyo nilimbatiza hapa hapa asubuhi nyingine. Asingeweza kuvumilia zaidi tena, kwa hiyo tulikuja tu chini hapa na kuvaa nguo zetu, na kuingia, na alibatizwa kwa Jina la Yesu Kristo.

23 Vema, nilifikiri kuwa alikwishapata kile chakula kizuri cha kiroho, labda kwa kuongea kidogo tungekula chakula cha asili. Kwa hiyo tukaenda kule Blue Boar, na kukaa chini tukawa tunaongea, na somo likajitokeza "Unaachaje watu wanasema juu

yako hivyo?”.

Basi, Ndugu Vayle ni mmojawapo wa watu wazuri mno niliowahi kuwajua lakini yeye ni “mwepesi tu kidogo kwenye kufyatua,” siku zote nimemwambia, unajua. Kwa hiyo yeye, hivyo nikasema .... Natumaini hiyo ni sahihi, Ndugu Vayle. Kwa hiyo yeye .... nikasema, “Usirukie kwa haraka. Kaa kwa utulivu. Mungu ndiye anayelifanya.”

Yeye akasema, “Loo! Inaweza kuwa vema kwako,” akasema, akasema. Lakini, vema, yeye-yeye ... Naamini yeye-yeye ni mwerevu mpaka anakutana na hao watu werevu wenye akili nyingi, kwa hiyo yeye anajua jinsi ya kulimwaga ndani pale, na hawana mahali pa kusimama. Hivyo ndivyo.

24 Hivyo nikasema, “Tazama, Ndugu Vayle” Tumekuwa tumekaa kule Blue Board. Nikasema, “Daudi, siku moja baada ya kuondolewa kutoka kwenye ufalme na mwanaye mwenyewe akakimbia kutoka kwenye kiti cha enzi, maasi, Israel iligawanyika, na Daudi akanyang'anywa ufalme na mwanawe mwenyewe, na alikuwa akitoka mjini, akilia. Na mtu ambaye hakutaka ujumbe wa siku yake ya mwisho, unajua hakumjali; mtu mzee, aliye mlemavu akitembea mwenyewe pale, akimfanyia dhihaka na akamtemea Daudi mate. Na yule mlinzi akatoa upanga, akasema, ”Nimwachie yule mbwa kichwa kikae juu yake, yule anayemtemea mate mfalme“' Daudi akasema, 'Mwacheni. Bwana amemwambia afanye hivyo! Unaona? Kumtemea mate, kumtania, na kumtemea mate. Kasema, 'Bwana amemwambia afanye hivyo.' Vema, tunaijua hiyo historia, jinsi ilivyorudi nyuma. Ndugu Vayle alifikiri ya kuwa hiyo ilihitaji neema nyingi kufanya hivyo.

25 Hivyo siyo zaidi ya kurudi na kuingia ofisini, mtunza hesabu wa serikali alimwita Billy Paul na kumweleza kuhusu hili. Hivyo Ndugu Vayle akaenda nyumbani pamoja na mimi. Nilipoingia, nikamwambia mke wangu ... Muda mrefu kwenye majira ya mchana. Tukaingia chumbani. Nikasema, “Nina jambo la kukuambia Mpenzi.”

49

Tulikuwa tukiongea kabla sijaondoka. Akasema, “Bill, najua kuwa Mungu alikutuma nje kule; sote tunajua hilo, lakini Yeye hakukwambia urudi. Unaona, sasa, hilo ndilo linalonikera”.

26 Nikasema, “Vema, nafikiri ni kwa ajili yako na watoto. Haidhuru kwangu. Nitamtumikia Yeye, Bwana akipenda, popote niendapo.” Na kwa hivyo nikirudi, na nikamwambia kuhusu hilo namna hiyo. Hivyo niligeuka tu nyuma na kuinua kofia yangu.

Na mtu fulani akasema jambo fulani, kuhusu, “Ee, huyu, mtoza ushuru! Inapasa tutoke nje ...” Namna tu ya kushambulia jambo fulani namna hiyo.

Bila ya kuwazia juu ya kile nilichosema juu ya Ndugu Vayle, nikasema, “Mwache. Labda Bwana alimwambia afanye hilo.”

Pindi tu nilivyosema hilo, Nuru iliangaza ukutani na kuandika pale, Ndugu Vayle na mke wangu wakiwa wamekaa pale, “Rudi Arizona.” Tarakimu zikiwa zimeandikwa ukutani, “Rudi Arizona.” Hilo ni sahihi. Hivyo ninakwenda, amina, kurudi Arizona.

27 Sasa, juma hili limekuwa juma la baraka kuu. Tulikuwa na mahojiano ya faragha juma hili, ya watu waliokuwa wakingojea tangu ile Mihuri Saba. Na sina shaka ila baadhi yao, bila shaka, walikuja kutoka nje ya mji, kote katika taifa. Lakini ile asubuhi kabla ya kuanza mahojiano nilikuwa chumbani, Roho Mtakatifu aliniwezesha kuandika sawasawa kila kitu walichokijua, kila kitu walichotaka kuuliza, kufuata kwa zamu jinsi tu walivyotaka kuuliza maswali na kuwaambia ndoto zao na kuwaambia ndoto zao tafsiri kabla hata hawajaniambia.

Sasa, watu wako chumbani hapa, pale. Na nikaendelea na kuwaacha waongee. Wangalisema, “Vema ndugu Branham, natoka huku na huku”.

28 Nikasema, “ Sasa, kumbuka, tumekusanyika hapa sio kwa ajili ya ushirika.

Hatukuja hapa kuwa na ushirika mmoja kwa mwingine. Kuna swali akilini mwako, moyoni mwako ambalo-ambalo ndani yake umejikwaa na hujui ni kitu gani. Na labda nitaweza, kwa msaada wa Mungu kulifanya.

Nikasema, “Kumbuka, yule malkia wa Kusini alikuwa na maswali vile vile yeye alipokuja kwa Sulemani. Na Biblia inasema hakuna chochote ambacho kiliwekwa wazi au kufichwa ambacho ”Sulemani hakuweza kutoa jibu lake.“ Na nikasema, ”mkuu kuliko Sulemani yuko hapa. unaona? Hilo ni sahihi Bwana Yesu Kristo aliahidi, 'Popote

wakusanyikapo wawili au watatu katika Jina Langu, nami nipo miongoni mwao. Na lolote watakalofikiria, au kutamani, na-na kuliomba! Na sasa swali lako ni jambo fulani usilojua kulihusu, jambo fulani usilolojua jinsi ya kuliendea, jambo fulani ambalo hujui cha kufanya kulihusu."

29 Na nikasema, "Tena Maandiko yalisema hili," kuwa, "Malaika wa Mungu huweka vituo pamoja na wale wanaomcha Yeye," hivyo katika ulimwengu mwingine ambapo zile hisi tano hazina mawasiliano nako".

Zile hisi tano huwasiliana na ulimwengu huu tu. Ikiwa huwezi kujisikia, usingeweza kuhisi chochote. Kuhisi kusingekuwa chochote kwako; hiyo ingekuwa ulimwengu mwingine. Kama usingeweza kuona, kile ambacho ungetazama kingekuwa ulimwengu mwingine, hujui chochote kuuhusu. Kwa hiyo hizi hisi tano ni kitu pekee ambacho Mungu ametuwekea sisi kuzitumia.

Sasa kuna nyingine inaitwa imani. Lakini kwa imani unapanda ngazi na mwishoni unaweza kuwa juu sana mpaka unaingia katika ulimwengu mwingine, ambao ni ono. Pale unaweza kuona.

Kama tu ikiwa hukuwahi kujua hiki kilikuwa nini ulichokuwa ukihisi kwa hisi yako ya kugusa, kamwe hukuiona; basi macho yako yangefunguka, ungeiona. Ingekuwa yote ni siri kwa yule mtu ambaye hajawahi kuona. Ingekuwa siri kwake, lakini bado hilo ndilo jambo lenyewe.

30 Na ndani pale, Bwana ... Kabla hatujafika hapa, kwa watu kutoka nchini kote, kila mahali, kutoka kaskazini, kusini, magharibi, wanakuja kwa ajili ya hayo mahojiano. Na mara tu wanapomaliza kuongea, yale maswali tu ambayo wangeuliza hasa, lile jambo ambalo wangeliuliza ningesema. "Tazama hapa, inuka juu ya hilo, na kulikuwa na kipande cha karatasi na kila swali, lizungukezunguke sawasawa tu jinsi walivyouliza, wangekwenda kuliuliza, jibu la swali lao chini hapa jinsi tu lilivyojibiwa. Bwana ni mkuu. Yeye anajua mambo yote. Lakini bado, ilinichukua karibu siku tatu kutoka kwenye mambo yaliyotokea mchana ule, mambo yalivyokuwa ni kuraruararua tu. Na sasa nilifikiria kulipata, hata hivyo kabla hatujaondoka.

31 Na kuna njia inayofaa, njia hasa kwa mtu mmoja mmoja. Sasa, kuna mambo yanayoweza kusemwa.

Na ikiwa wako watu hapa, wanaojua kuwa siri za mioyo zilizofunuliwa ambazo hakika zinge... Ingetisha; ingesababisha uvunjaji wa sheria, ingesababisha mtu fulani kumpiga risasi mwingine, au jambo fulani, ikiwa hilo lingefunuliwa hapa hapa kwenye jukwaa namna hii hadharani, mbele ya umati wa watu,. Ingesababisha hatia zinazostahili adhabu ya kifungo gerezani na kila kitu kingine, ambacho kingeweza kuwa.

32 Lakini wakati mnapokaa pamoja namna hiyo, Roho Mtakatifu, mkiwa wawili tu pamoja. Lakini tunalielewa hili, kuwa lile waliloniuliza ni la siri. Sisemi lolote kuhusu hilo. Na kile ninachowaambia, ni juu yao kama wanataka kukisema au la. Unaona? Lakini kinafahamika kati yetu, mahojiano. Hiyo ni kuchukua mtu mmoja kwa wakati mmoja na kukaa pale mpaka kila kitu kimewekwa sawa kabisa, unaona, Roho Mtakatifu.

33 Na sasa kufikiria juu ya neema, Roho Mtakatifu akiniambia yote kuhusu hilo, kwa kila mmoja, mstari wao wote, kabla hata hawajaja hapa; nchini kote, wakija, watu ambao sijawahi kuwaona maishani. Na kuyaandika ili kwamba wangejua kwa utaratibu tu kufuatana na maswali jinsi ambavyo wangeyajibu.

34 Ndugu mmoja alikuwa na maswali juu ya uzao wa nyoka, ambayo sikuyajibu vile hasa ilivyotakiwa kwa sababu wakati wao wa nusu saa ulikwisha. Natumaini kuwa yeye aliyapata vema majibu ya maswali yake, kwenye karatasi. Ni ... Yeye alikuwa amekwishayaandika, na hakuweza kupata majibu yake yote, hivyo nilimrudishia tu ile karatasi yake ya maswali, majibu kwenye karatasi kama hajaipata bado ni Billy Paul aliye nayo. Najua huyo mtu ameketi hapa, nimemtazama tu muda mfupi uliopita. Kwa hiyo ikiwa yeye- anataka kuipata hiyo imeandikwa kwenye kipande cha karatasi, majibu ya maswali yako.

35 Sasa, ee jinsi Bwana alivyo mwema, mnajua. Natumaini kila mtu anajisikia vizuri. Loo!

Na sasa tukumbuke, na sasa ninaoomba kwa ajili ya hizi leso, kumbuka Ndugu Dauch. Yeye ni ndugu wa thamani, na tunataka kumkumbuka katika maombi.

36 Na na- namwona Ndugu Ungren, ila si-simoni Dada Ungren popote, ikiwa yeye ni mzima sasa. Ndiyo, amekaa pale karibu na yeye. Hakika naam. Ninafurahi. Kwani tuliitwa kwa ghafla kumhusu yeye.... usiku ule mwingine yeye na binti yake, Dada... Siwezi .... Downing, Downing wakiwa wanaendesha gari waliacha njia na ni neema ya Mungu tu, au wote wawili wangekuwa wamepondwa vipande vipande pale pale. Na hapa, wanakuja moja kwa moja kanisani, wanapakia treni na kuja.

37 Kamwe sitawasahau ninyi nyote. Nawapenda. Mungu anajua hilo. Na nawapenda. Jinsi nilivyowajia kwa kukatisha nchi nzima, kupitia katika hali ya utelezi!

Ninapowaangalia baadhi ya ndugu hapa kutoka Georgia na Alabama, na sehemu mbalimbali, na Tennessee, na kote, wanakoendesha magari yao barabarani, penye barafu wakiteleza mbele na nyuma kama hivyo kuja hapa kwa ajili ya ibada moja.

38 Nilipokuwa na ule wito wa dharura kwa Ndugu Dauch siku ile sikutambua kuwa Lima, Ohio ilikuwa mbali kiasi hicho. Tu... Nilifikiri ilikuwa ni kurukaruka kwa mguu mmoja kisha kuweka kamba na kuiruka unakuwa hapo. Lakini, jamani, niliondoka hapa mapema sana asubuhi ile, sikufika pale mpaka saa saba mchana nikiendesha kila-kila kitu jinsi vile viwango vya mwendo vilivyoamriwa barabarani vingeruhusu, na kwenye njia kuu ya barabara mbili. Na nawazia jinsi kulivyo karibu, na kule Kusini ambapo hawa watu wengine wanatoka, kule Kaskazini na Magharibi, wanakotoka.

Nawapenda, na hiyo ndiyo sababu najaribu kuwa mnyofu wa moyo mno hapa.

39 Na wale waamini wa tangu miaka mingi Namwona Ndugu Creech na wao wamekaa nyuma kule sasa, na ambao wamekuwa pamoja nami miaka yote hii na mengineyo, na jinsi ambavyo tumekuwa tukikua pamoja. Nilikuwa nikitazama picha ya Mary Jo, naamini ilikuwa usiku mmoja siku kadhaa zilizopita. Alikuwa tu kamtu kadogo tulipokutana naye mara ya kwanza, na sasa ameolewa, nadhani na ana watoto. Ndugu Creech na Dada Creech, wadogo, wenye nywele nyeusi, na Meda na mimi, na hapa tuna mvi na kibiongo. Unaona, kuna jambo fulani kuhusu watu kama wale, linalokuvutia. Unaona, una-una-unataka kukaa nao. Unaona? Kuna jambo fulani lingine ambalo-ambalo siku zote linafanya mawazo yako kuvutwa nyuma. Nawatoa tu kama mfano kwa wengine walioko hapa, vijana na wazee. Tunatazamia kwa furaha Kuja kwa Bwana.

40 Hivyo, asubuhi hii nimeliweka.... Naamini Mungu aliliweka moyoni mwangu kufundisha somo la shule ya Jumapili hapa asubuhi hii, Mungu akipenda, kwa kitambo kirefu. Na mimi ... Na sasa, hii ikiwa ni huduma yangu ya mwisho kwa muda kidogo, kadiri nijuavyo, ile....

41 Na nawataka mkumbuke ya kuwa Ndugu Neville hapa, amebakia hapa kanisani, katika uangalizi wa hili Hekalu, chini ya Roho Mtakatifu, kwamba anahudumia hapa, naye anaamini Ujumbe huu na -na anaufundisha kama tu nifanyavyo. Vema. Na wakati wowote utakaotaka, unaweza kuona sawa kuja kumsikiliza Ndugu Nevile, hakika yeye angekufanyia jema, nina hakika. Yeye ni mtumishi mkuu wa Yesu Kristo.

Nimemfahamu Orman Neville tangu nilipokuwa mvulana mdogo, na hajabadilika hata chembe moja, ila tu anaendelea zaidi kuwa karibu na Mungu. Nakumbuka mara ya kwanza nilipomwona juu ya ... nilikaribishwa kwenye jukwaa lake la Kimethodisti. Na niliporudi hapa Hekaluni, nikasema, "Siku moja, nitambatiza katika Jina la Yesu Kristo". Na yuko hapa akiwa na Ujumbe sasa, akiendelea, mtumishi shupavu hasa.

42 Na Ndugu Neville anapitia katika majaribu na huzuni kubwa ambayo haonyeshi hapa Hekaluni. Lakini kwa vile Bwana ananiwezesha kuona kidogo katika maisha ya watu, najua kile anachopitia mambo yake mengi, unaona., na hakika anapitia chini ya masumbufu mengi, majaribu na mambo ya aina hiyo. Na ninyi, ninyi watu hapa, mwinueni-kama Yoshua na Kalebi walivyoinua mikono ya Musa wakati yeye analeta lile Neno.

43 Pendaneni ninyi kwa ninyi zaidi ya yote. Pendaneni ninyi kwa ninyi Msi.... Haidhuru kile shetani anachojaribu kusema! Sasa ninyi ni kundi moja kubwa tamu sasa, lakini kumbukeni onyo langu, unaona, Shetani hawezi kuachia hilo lidumu namna hiyo. Hapana, bwana. Atatupia kila kitu mshale, ikiwa yeye angemleta mtu fulani ndani amfanye lengo lake. Atamleta ndani mtu mkosoaji au asiyeamini, na kumketisha chini, na kumfanya yeye kushiriki pamoja nanyi chini ya utulivu na mambo ya aina hiyo na ndipo atamtupia yule mtu aina fulani ya sumu, naye ataanza kuzunguka nayo kanisani. Msikae upande wake. Msiwe na chochote cha kufanya na kitu kingine chochote. Mdumu

kupendana na wema na wenye kuhurumiana ninyi kwa ninyi. Mwombeeni yule mtu, kwamba aokolewe vile vile, au yule mwanamke, au yeyote yule awaye, waombeeni tu. Na shikamaneni ninyi kwa ninyi

Na dumuni na mchungaji wenu. Unaona, Yeye ni mchunga kondoo, nanyi mpeni heshima. Yeye atawaongoza hadi mwisho na kwa sababu yeye ameamriwa na Mungu kufanya hivyo.

44 Sasa mnalikumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." -Mh] Adui atakuja. Naye anapokuja. mshikamane tu pamoja kwa karibu zaidi. Na yule ambaye shetani anamtumia kama adui ama atatoka nje ama aingie ndani na kuwa mmoja wenu. Ni hilo tu.

Kamwe msifanye ukoo miongoni mwenu, au-au kuongea na kujifanyia mshikamano wa kiukoo. Sisi ni wamoja. Singesema "Mkono wa kushoto nimekukasirikia, nitakuondoa kwa sababu wewe si wa mkono wa kulia." Yeye ni mkono wangu wa kushoto. Nataka akae pale. hata ncha ndogo ya kidole changu, nataka ikae pale pale tukae kila mmoja na mwingine, kila mmoja akae kabisa na mwingine.

45 Na sasa mnazo kanda juu ya hilo. Mnazo kanda juu ya kile tunachoamini. Mnazo kanda juu ya nidhamu kanisani, jinsi tunavyoenenda kwa kujiheshimu katika kanisa la Mungu, jinsi itupasavyo kuja hapa pamoja na kukaa pamoja katika makao ya Kimbinguni. Msikae nyumbani. Ikiwa Mungu yuko moyoni mwako huwezi kusubiri milango ifunguliwe pale, ili uingie hapa kushiriki pamoja na ndugu zako. Kama huwezi, hujisikii namna hiyo, ni wakati wa kwenda kwenye kuomba.

Bila shaka tuko katika siku za mwisho, pale Biblia ilipoinuka... au ilitufundisha ku-ku, "Zaidi tuonapo ile siku ikiwadia" kumpenda mwingine kwa upendo wa Kikristo na upendo wa Kiungu, 'kukusanyika wenyewe pamoja katika sehemu za Kimbinguni na-na Kristo Yesu," na pendaneni ninyi kwa ninyi. Kwa hili watu wote wajue ninyi ni wanafunzi Wangu, mtakapopendana ninyi kwa ninyi." Hilo ni sahihi. Kaeni pamoja kila mmoja na mwingine.

46 Kama unafikiri ndugu amekosea kidogo, au dada, sema "Bwana usiniache kamwe shina la uchungu likachipuka kwa sababu ita-itamuathiri Yeye na itamtoa Kristo nje kutoka katika maisha yangu". Ile sumu ya tindikali ya nia ya kudhuru wengine na wivu, na chuki, hayo yatamtoa tu Roho Mtakatifu atoke kwako. Itamwondoa Yeye hapa Hekaluni. itamuua Roho wa Mungu, au itamwondoa Yeye atoke hapa, kumsononesha mchungaji wenu. Itafanya kila kitu. Unaona? Msifanye hilo.

Mzidi zaidi kushikana tu karibu pamoja. Vuteni .... Chukueni kishikizo kama ndugu alivyoshuhudia mhudumu hapa usiku ule, kuhusu kuwa na bakoli akiona kwenye ono. Tu... Hiyo inafunga pamoja silaha zote za Mungu. Hiyo inafunga pamoja tu, kaza, jongeeni karibu zaidi kila mmoja kwa mwingine, pendaneni ninyi kwa ninyi, kwa vyovyote... Zungumzeni mema kila mmoja juu ya mwingine. Semeni mambo mema kila mmoja kuhusu mwingine na ndipo Mungu atawabariki.

47 Sasa asubuhi hii, Bwana akipenda, kwa msaada Wake na neema nina furushi la maswali hapa, namaanisha ya Maandiko. Na sasa kabla hatujaliendea ... Nafikiri nilisikia vinasa sauti vikigonga ndani pale. Tunakwenda kuleta Ujumbe sasa, kwa neema ya Mungu.

Neno la maombi kwanza.

48 Bwana Yesu, nikiunenea huu mwili wa Kanisa, kuwa wangeshikana pamoja kwa mkono wa Mungu usiobadilika. Lile Neno lina madaraka ya kileleni, likiwaonya, kama Paulo alivyoonya kundi lake, kuwa "mbwa mwitu wangeingia." Wewe ni Mungu yule yule leo kama ulivyokuwa wakati ule, na yule adui ni yule yule. Hebu huu ushirika na vifungo vya upendo ukae miongoni mwa watu hawa siku zote, katika Kristo Yesu.

Tusaidie Bwana asubuhi hii, tunaposoma Neno. Hebu Roho Mtakatifu afunue hilo kwetu, kuwa Kanisa liweze kuthibitishwa kikamilifu katika "Imani ile waliyopewa watakatifu mara moja tu" kuwashikilia. Na iwe kama Wewe ulivyotoa ono miaka miwili iliyopita, kuhifadhi chakula, mboga nzuri zilizoonekana kuwa na afya nilizoona kwenye ono zikihifadhiwa hapa katika hili Hekalu, na tupokee leo pipa zima lililojaa Hilo. Tujalie Bwana. Au mzigo wa kanda, ili liweze kumfunua Yesu Kristo kwetu katika wakati huu tunaoishi, litupe nguvu ya kuhimili nguvu ya kiroho kwa ajili ya kazi iliyopo mbele. Tujalie Baba.

49 Wabariki hawa watoto wako. Wapo hapa ndani asubuhi hii kutoka sehemu mbalimbali za taifa, asubuhi yenye joto na kunata, lakini bado tunasikia Uwepo wa Roho Mtakatifu, katika lote hili.

Tunawawazia John wesley, na Calvin, na Sankey na Knox, Finey, na wengi wa wale, bila hata kuwa na panga boi ya umeme pale watu walipoketi kwenye kumbi, na jasho likitiririka kwenye nyuso zao. Wanawake waliovaa na kufunikwa vyema, waliketi katika kusanyiko na kutokwa jasho mpaka nguo zao zikalowa, wakisikiliza Neno la Mungu, wakilisha nafsi zao. Sasa tunaona moyoni Bwana, ya kuwa wamepumzika mahali fulani kule wakisubiri Kuja kwa Bwana.

50 Tuweke pamoja Baba. Roho Mtakatifu na atuongoze na kutuelekeza. Tupe maisha marefu ya huduma kwa ajili Yako. Tupe Ujumbe huu mkuu asubuhi hii ambao tunautegemea toka kwenye Neno Lako, kwamba unaweza kwenda katika kila moyo. Fanya ile midomo itakayonena, Bwana , inene Kweli. Ifanye ile mioyo itakayosikia kurutubishwa kupokea Kweli, na ikue na kuwa miti mikubwa ya Uzima wa Milele, iwe nuru zing'aazo na nyaraka zisomwazo na watu wote, ili wajue kuwa Yesu Kristo amefufuka toka kwa wafu na anaishi miongoni mwetu. Tufanye tuwe waliojaa upendo mno na tunda la Roho mpaka wanaume wengine, na wanawake, wavulana na wasichana waone matokeo ya Uhai wa Kristo ukiishi ndani yetu, baada ya miaka elfu mbili tangu lile tukio kuu. Tujalie Baba, kukuheshimu Wewe. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

51 Sasa nataka kusoma baadhi ya Maandiko. Na naamini sasa kuwa mnazo kalamu zenu za risasi na karatasi, na kila kitu tayari.

Na Ndugu Neville, umekaa kwa utulivu. Nitavua koti langu tu, ikiwa hilo ni ... [Ndugu Neville anasema, Hiyo ni sawa."-Mh.] Ni ... Samahani kwa kuvua koti langu, ila hapa-hapa pana joto sana.

52 Sasa nataka mfungue Kitabu cha Wakolosai, sura ya 1 ya Wakolosai. Na ndipo tunaposoma hili, tukianza na ... Nawatakeni, mtakapokwenda nyumbani, msome sura yote ya hawa Wakolosai. Lakini nataka msome asubuhi hii pamoja nami, kutoka aya ya 15, pamoja na aya ya 29.

Na sasa iweni wavumilivu mwezavyo, kwani najisikia kwamba katika hili hapa, ikiwa Mungu atanisaidia, litafunua na kuleta akilini mwenu haya mambo mengine yote ambayo nimeyasema wakati wote wa siku za Hekaluni; kwa nini nimesema kile nilichosema, na kwa nini nimefanya kile nilichofanya. Hii ndiyo sababu. 98 Sasa kutoka aya ya 15

Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote:

Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni, na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana, … visivyoonekana, ikiwa ni viti vya enzi, … usultani, … mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake:

Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikamana katika yeye.

Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani cha kanisa: naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu; ili kwamba awe mtangulizi katika yote.

Kwa kuwa katika yeye ilimpendeza Baba kuwa katika yeye utimilifu wote ukae-utimilifu wote ukae;

Hebu niweke msisitizo kidogo kwenye hiyo tena, hii aya ya 19

Kwa kuwa katika yeye ilimpendeza Baba kuwa katika yeye utimilifu wote ukae;

Na, kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake, akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni.

Tazama pale ule upatanisho ulikokwenda

Na ninyi, mliokuwa wakatimwingine mmefarikishwa tena adui katika nia zenu kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa;

Katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete nimyi mbele zake, watakatifu ... wasio na mawaa wala lawama.... mliopata kibali mbele zake:

Mkidumu tu katika ile imani hali mmewekwa juu ya msingi, mkawa imara; msipogeuzwa na kuliacha tumaini la Injili, mliyosikia habari zake, iliyohubiriwa katika

viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu ambavyo mimi Paulo nalikuwa mhudumu wake.

Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu, tena nayatimiza yale yaliyopunguka ... mateso ya Kristo... mwili kwa ajili ya mwili wake, yaani kanisa:

Ambalo nimefanywa mhudumu wake, sawasawa na uwakili wa Mungu niliopewa kwa faida yenu, nilitimize Neno la Mungu;

Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake:

100

Na ninataka kusoma ile aya tena.

Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake:

Ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa: nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu:

Ambaye sisi tunamhubiri habari zake, kila mtu katika hekima yote; tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo.

Nami najitaabisha kwa neno hilo hilo, nikijitahidi kwa kadri ya kutenda kazi kwake Yeye atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu.

53 Sasa kwa ajili ya somo ninalotaka kuchukua pale, hili kwa ajili ya somo, nikijenga msingi kwenye Biblia yote, ila nataka tuliite: Kristo ni Siri Ya Mungu Iliyofunuliwa. Kristo akiwa ni siri ya Mungu iliyofunuliwa! Basi nimelichukua kama somo la shule ya Jumapili, kwa hiyo tungeweza kusoma pamoja na-na kuwa na ushirika pamoja.

54 Sasa siri ya fumbo la Mungu, Yeye alikuwa nayo kabla ya kuwako ulimwengu. Sasa, nyuma katika sehemu ya nyuma ya nia ya Mungu kulikuwa na jambo fulani ambalo, Yeye alikuwa akijaribu na alikuwa anakwenda kutimiza, naye alikuwa na sababu katika kulifanya; ili kwamba aweze kujidhihirisha Mwenyewe wazi. Kwa sababu, kwanza hakukuwa hata na mwezi, nyota, atomi, molekuli, au chochote. Yeye alikuwa Mungu. Lakini Yeye hakuwa Mungu sawasawa kwa wakati ule, kwa sababu Mungu ni kitu cha kuabudiwa, na hakukuwa na chochote cha kumwabudu Yeye.

Kwa hiyo, katika nia Yake kuu, Yeye alitaka hizi Sifa zidhihirike. Na katika Yeye kulikuwako upendo; Katika Yeye kungekujakuwa Baba; katika Yeye kungekujakuwa Mwana, katika Yeye kungekujakuwa Mwokozi; katika Yeye kungekujakuwa mponyaji. Na Sifa zote hizi tunazoziona tayari zimedhihirishwa, zilikuwa ndani ya Mungu.

55 Kwa hiyo, oni langu, kitu cha kwanza Yeye alichofanya kilikuwa Malaika. Na ndipo wakamwabudu, na hilo likamfanya Yeye kuwa Mungu. Naye alianza pale. Kama katika Jumbe zilizopita nimejaribu kuelezea kulirahisisha . Na sasa, basi, Malaika walipoanza kumwabudu Yeye, hiyo ni kabla hata hakujawa na molekuli duniani. Hakukuwa na chochote. Kulikuwa giza kote. Hakukuwa na jua, wala mwezi, hakuna nyota, hakuna chochote. Ndipo Yeye alikuwa Mungu. Kama alivyomwuliza Ayubu, "Ulikuwa wapi nilipoweka misingi ya ulimwengu, unaona, wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, wana wa Mungu walivyopiga kelele kwa shangwe? Unaona, sasa ulikuwa wapi?" Unaona? Hiyo ni kule nyuma kabla ya dunia.

56 Sasa, Mungu alikuwa na kusudi na siri iliyofichwa. Na hilo ndilo nataka kunena juu yake kwa Kanisa asubuhi hii, ile siri ya Mungu iliyofichwa, ile Yeye aliyokuwa nayo katika nia Yake kabla dunia haijaanza, na jinsi ilivyojifunua yenyewe moja kwa moja mpaka saa hii ambayo tunaishi. Unaona? Ndipo mtaelewa kwa ufasaha basi, unaona, juu ya naamini kile kinachofanyika.

57 Fumbo kuu la Mungu la jinsi ilivyo siri. Aliiweka kuwa siri. Hakuna mtu aliyejua chochote juu yake. Hata Malaika hawakuelewa. Unaona, Yeye hakuifunua. Hiyo ndiyo sababu, chini ya siri yetu ya saba, wakati ule muhuri wa saba ulipofunguliwa, kulikuwa na ukimya. Yesu alipokuwa duniani, walitaka kujua Yeye angekuja lini. Yeye alisema, "Siyo .... Hata Mwana Mwenyewe hajui ni wakati gani itatokea." Unaona, Mungu alilihifadhi hili lote ndani yake Yeye Mwenyewe. Ni siri. Na hiyo ndiyo sababu kulikuwa na ukimya mbinguni kwa muda wa nusu saa, na ngurumo saba zikatoa sauti zao, naye Yohana hata alikatazwa kuliandika, unaona, kule Kuja kwa Bwana. Hilo ni jambo moja ambalo hajalifunua bado, juu ya jinsi Yeye atakavyokuja, na lini Yeye atakuja. Ni jambo

jema kwamba Yeye hafanyi hivyo. Hapana.

58 Yeye amelionyesha au kulifunua katika kila mfano uliopo kwenye Biblia. Kwa hiyo, Biblia nzima ni ufunuo wa siri ya Mungu katika Kristo. Lo. Biblia nzima ni udhihirisho wa shabaha moja aliyokuwa nayo Mungu, kusudi moja alilotaka kulitimiza katika Biblia nzima. Na matendo yote ya-ya waamini katika Biblia yamekuwa katika mfano, na kudhihirisha ile shabaha kuu ya Mungu ni nini, na sasa katika hii siku ya mwisho Yeye amelifunua na kulionyesha. Na msaada wa Mungu, vema mtauona hapa hapa asubuhi hii, kile ambacho Bwana amekuwa nacho katika nia Yake wakati wote, na amelidhihirisha.

Kwa hiyo, unaweza kuona maana kuu ya kile kilichokuwa kwa kulijua hili, na na kisha kujaribu kulileta kwa watu. Unaona? Na ndipo hufanyi .. Sijaingia ndani kujaribu kulieleza kama Mungu alivyolifunua kwangu.

59 Sasa iwapo unataka kuliwekea alama. Nina sehemu nyingi ninazotaka kuzisoma. Na sasa katika-katika Kitabu cha Mtakatifu Luka, sura ya 24 ya Mtakatifu Luka, tunakuta ni ,,, Ni wawili wa wale mitume njiani kwenda Emau. Na Yesu akatokea, baada ya ufufuo Wake, nao walikuwa kwenyenjiani mwao kwenda Emau, wakitembea barabarani, wakifikiri na kuongea, na- kulia, juu ya kifo Chake, na jinsi walivyomwona akiteseka kwa ajili ya kile walichokuwa wamedhani hakikuwa na thamani hata kidogo; Walimchukua Bwana wao na kumsulubisha. Nao-nao walikuwa wakitembea pale, wakilia.

Na alijitokeza kutoka pembeni mwa barabara na kuanza kuongea nao kuhusu Kristo. Alisema, "Enyi msiofahamu na wenye mioyo mizito. Je, hamjui ya kuwa manabii wote na Zaburi..." Unaona, alikuwa akifanya nini? Akijitambulisha Mwenyewe kwa hawa wanafunzi, yakuwa manabii wote, na Zaburi yote, na kila kitu kilikuwa ni Yeye aliyedhihirishwa. Unaona?

60 Na sasa madhumuni ya mimi kutokuhubiri asubuhi hii, ni kwa sababu, nilifikiri katika kufundisha, tungeelewa vema zaidi kuliko kuchukua tu somo na kuruka juu yake. Tungelifundisha hilo tu .

61 Sasa, Yeye alikuwa akisema kuwa Zaburi yote na manabii wote walinena juu Yake. Vema, kwa hiyo pale, hiyo inaonyesha ya kuwa Agano la Kale lote, Agano Jipya lote, na Zaburi yote, kuimba, zile nyimbo zilizoimbwa, ziliimbwa kumhusu Yeye.

Chukua Zaburi ya 22 na uiimbe, na uilinganishe na ile asubuhi ya usulubisho. Unaona, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha? Mifupa Yangu yote inanikodolea macho. Walichoma miguu Yangu na mikono Yangu." Bado mambo yote hayo pale, wao wakiimba ile Zaburi chini kule hekaluni, na wakimsulubisha Yeye Mwenyewe hasa. Unaona? Unaona, wale viongozi wakuu wa kidini, wale watu wakuu, wale walimu wakuu, na bado walikuwa vipofu mno, wale waliokuwa wakisoma manabii na walikuwa wakiimba nyimbo, na kufanya uahalifu ule waliosema wangefanya.

Jambo lile lile linatokea asubuhi hii!

62 Sasa sikiliza kwa makini kwa sababu.... Sasa sitaangalia ile saa itakachosema. Nataka mlipate hili. Unaona? Sijali. Unaona? [Kusanyiko linashangilia, linasema, "Amina."-Mh.].

Kwa hiyo unaweza kuona hapa, kimsingi, hapa mwanzo, lile wazo hasa alilokuwa nalo Mungu katika nia Yake, Yeye alilificha kwa wale wasomi wote. Na ... Ni idadi fulani tu, idadi fulani ya waliochaguliwa kimbele tu, watu waliochaguliwa kimbele, ndio hao tu waliolisikia. Na sasa chunguza Maandiko rudi nyuma kote katika kizazi cha manabii na uone kama ikiwa halikuwa jambo lile lile. Unaona?

Sasa, na Yesu hapa akiwarejesha kwa manabii na Zaburi, Alisema wote walinena yaliyomhusu Yeye. Unaona? Na hawa walimu wa Kiyahudi hapa marabi madaktari wa sheria, maprofesa, walifanya sawasawa tu kama walivyofanya hapo kabla.

63 Sasa angelia tena, Yeye alisema, "Chunguzeni Maandiko, kwani Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Chunguzeni Maandiko, Maandiko, Maandiko yote. Kitu gani najaribu kufanya? Kuwaonyesha kuwa hii Biblia ndicho kitu kilicho sahihi.

64 Siku ile nyingine nikiwa nimesimama ndani ya chumba cha hospitali nikiongea, dada mmoja aliniomba kuelezea kuhusu madhehebu, kwa nini tulikuwa-tulikuwa kinyume na madhehebu, dhidi ya baadhi ya watu wa madhehebu.

Unaona, lazima irejee kwenye Neno, kwa sababu Neno ni Mungu. Unaona? Na Yesu

alitangaza jambo lile lile hapa, kuwa lile Neno ni Yeye.

Huwezi kufanya Andiko Lijipinge Lenyewe. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu Naye Neno alikuwa Mungu. Na lile Neno likafanyika mwili! Unaona?

65 Sasa Yesu anasema hapa, "Chunguzeni Maandiko, Yananishuhudia. Ndani Yake mnadhani kuna Uzima wa Milele," na hiyo ni kweli," Nayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Nami nayashuhudia Hayo. Na kama sitendi kazi zilizoahidiwa kuwa ningefanya, basi msinisikiye Mimi. Lakini kama natenda kazi, nanyi hamwezi kuniamini, aminini zile kazi, kwa sababu zinamshuhudia kuwa Yeye ni Lile Neno." Ee, inaonekana kama kwamba lisingeweza kuwa wazi zaidi ya hivyo. Unaona? Vema. Sasa, "Chunguzeni Maandiko." Yeye alisema Musa na torati yote, na kadhalika, na manabii na Zaburi, zilizungumza juu Yake. Na tena, Yeye alisema Maandiko yanamshuhudia.

66 Yeye ni hoja kuu ya Biblia yote. Kama ulisoma Biblia, na usimwone Kristo katika kila mstari Wake, rudi nyuma na uisome tena. Unaona? Kama huwezi kumwona Kristo katika kila mstari wa Biblia, basi uisome tena, kwa sababu kuna jambo umelikosa. Biblia ni Kristo. Yeye ni Neno. Unaposoma, "Hapo mwanzo Mungu aliumba," kuna Kristo. Unaona? Kila... Toka hilo, mpaka "Amina" katika Ufunuo, kila Neno linamshuhudia Yesu Kristo.

Hiyo ndiyo sababu hivi vitabu vilivyoongezwa wanavyoviita "Kitabu cha Pili cha Danieli, na kile-kile Kitabu cha Makabayo, na Agesi na Toharani," na vitu kama hivyo, unaona havikunenwa katika Maandiko. Unaona? Haiendani na Neno lote. Hakuna mahali pa kuweka toharani ndani pale. Hakuna mahali pa kuweka maombezi ya watakatifu, na vitu. Hakuna mahali ndani pale kwa ajili ya hayo. Hakuna sehemu kwa ajili ya dhehebu. Hakuna sehemu kwa ajili ya-kwa ajili ya Kanuni za imani nje ya hayo; ya Biblia. Unaona? Kwa hiyo unapoona hayo mambo, haya-hayaji tu kwenye picha. Na hiyo ndiyo sababu watu wameongeza hivyo, na kupata fumbo lililochanganywa lote. Unaona? Hawawezi kuliweka sawa "yule yule jana, leo, na hata milele!"

67 Lakini, ikiwa mambo yatawekwa sawa pamoja, kuna picha nzima ya kuanguka na wongofu . Picha yote ya uumbaji, na mpango wote wa Mungu ilifunuliwa katika Yesu Kristo. Amina! Hiyo ni picha yote imewekwa pamoja, kila mahali palipojikunja na kila kona. Ni kama tu ... Sasa, simaanishi kupuuza mambo ya kiroho yaliyo ya kweli isipokuwa tu ni kufumbua fumbo kwa kuunganisha mitego yake pamoja.

Hiyo ndiyo sababu tuna picha siku hizi zinazoonekana za kutisha. Mnasema, "Sisi ni waamini," na ng'ombe akila majani juu ya mti. Haiwezekani. Hiyo ni wakati wanasema, "Naam, Yeye ni kila njia, lakini kwa ajili tu ya akina ... Yeye ni yule jana, leo, na hata milele, yote ila kitu fulani." Unaona? Ndipo unaharibu picha yako.

68 Biblia ilisema Yeye ni yule yule! Mtakatifu Yohana 5, au Mtakatifu Yohana 14:12, Yeye alisema, "yeye", yeye, mtu yeyote. "Yeye aniaminiye, kazi nizifanyazo, naye atazifanya."

"Vema, hiyo ilikuwa kwa ajili ya kizazi kingine".

Hapo unakuwa na picha yako ya makosa tena. Unakuta mtu akivua samaki jangwani, kwenye rundo la mchanga wenye joto ambako hakuna samaki. Unaona? Unaona, inakupasa kumrudisha pale ambapo anavua, pale Galilaya, ambako kuna samaki wengi, unaona. Unaona?

Ya-yakupasa uweke picha ionekane sahihi. Ni picha kuu ya Mungu. Na kuna njia moja tu ya kuona, pale ambapo unamwona Yesu Kristo. Pale ndipo kuna Biblia nzima. Yeye ni hoja kuu ya Biblia..

69 Sasa unatambua kuwa kokote kwenye sehemu hizi hapa ungeweza kupata somo, na ni vigumu kwa muhubiri kujizuia. Anaonekana kama anataka kuendelea nalo, lakini yakupasa kurejea kile tunachofundisha.

Yeye ni hoja kuu ya Biblia. Yeye alikuwa katika manabii. Yeye alikuwa katika Zaburi. Yeye alikuwa katika historia ya Biblia. Biblia ni Kitabu cha kinabii. Ni kitabu cha kihistoria. Ni Kitabu cha upendo. Ni kitabu cha-cha nyimbo. Ni Kitabu cha Uzima. Na ndani kule unamkuta Kristo. Yeye alikuwa katika manabii. Yeye alikuwa katika Zaburi. Yeye alikuwa katika historia. Na Yeye pia, katika manabii. Yeye alikuwa katika Zaburi. Yeye alikuwa katika historia. Na Yeye pia, katika Biblia, ndiye mambo yale yatakayokuja.

Kwa hiyo Yeye alikuwako tangu kabla mpaka baada. Hilo linamfanya Yeye kuwa nani basi? "Yeye yule jana, leo, na hata milele."

70 Nawe uingize jambo ndani Pale, ambalo halimfanyi "Yeye yule jana, leo, na hata milele," Ndugu Lee unakwenda wapi? Una picha ya kutisha hapa. Kwani, Yeye alikuwa historia, unaona, na Yeye ni Nabii. Yeye ni Zaburi.

Yeye ni kila kitu. Na kama huwezi kumfanya Yeye kila kitu, na yule yule, wapi, picha yako inaonekanaje? Unaliona? [Kusanyiko linasema, "Amina." Mh.] Vema.

71 Yeye ndiye hilo! Yeye alikuwa manabii. Alikuwa ndani yao. Yeye alikuwa katika Zaburi. Yeye alikuwa katika historia, naye ni mambo yatakayokuja, "yule jana leo, na hata milele." Waebrania 13:8, ikiwa unaliandika. Angekuwa basi, Yeye angekuwa mkuu, kama Yeye yu Hilo. Na tunaliamini hilo, au sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina.:-Mh.] Ndipo ikiwa Yeye Ndiye Hilo basi Yeye angekuwa hoja kuu ya mazungumzo yetu, ya kufikiri kwetu, ya uimbaji wetu, ya mienendo yetu. ['Amina."] Yeye angekuwa hoja kuu ya maisha yetu . Ikiwa Yeye ni hoja kuu ya Biblia, na Biblia iko ndani yetu, basi ingempasa kuwa hoja kuu ya kila kitu tufanyacho, tusemacho au kufikiri, angekuwa Kristo. Hiyo ni sahihi? [Amina."] Vema.

72 Kwa kuwa, twawaza hivi, kwa kuwa Yeye amefanywa-amefanywa kichwa cha "vitu vyote" kwetu. Wakolosai ilisema hivyo hapa. Yeye ni kichwa cha "vitu vyote kwetu." Kwani Yeye alifanyika ..... kwa ajili yetu, ambao tumehesabiwa kuwa "vitu vyote". Unasema, "Vipi kuhusu mwenye dhambi?" Yeye alifanywa kuwa Jaji wa mwenye dhambi ikiwa hatalipokea. Yeye alifanywa utukufu kwa mwamini anayelipokea. Kwa hiyo pale, kitu, "vitu vyote viliumbwa na Yeye, na kwa ajili Yake."

Na inahitaji kuweko usiku ili kudhihirisha utukufu wa mchana. Inahitaji chombo kisichokuwa na heshima ili kudhihirisha ule-upendo na matunzo ya chombo kilicho na heshima. Itahitaji mwanamke mwovu ambaye angevaa nguo zisizo na uadilifu na… na kuuza maadili yake, ili kudhihirisha wema wa mwanamke mwadilifu. Unaona? Inahitaji kuweko mwanamume mkora na mwizi, kudhihirisha uhalisi wa mwamini wa kweli, Mkristo wa kweli. Inahitaji kuweko mnafiki, kuonyesha mwamini kile alicho.

73 Hivyo "Vitu vyote vilifanywa na Yeye." Na kwa kuwa Yeye alifanywa vitu vyote... alifanywa, kwa ajili yetu wote, vitu vyote vilifanywa kwa ajili yake, na Yeye. Ndipo, kwa vile hilo ni kweli, tungejitambulisha (ingepasa) na Yeye. Tungetambulishwa, sisi wenyewe na Yeye kwa sababu Yeye amejitambusha Mwenyewe na sisi. Inabidi tutambulishwe na Yeye. Jinsi gani? Kwa kuishi kwa ajili Yake, sio kukiri tu.

Hivyo watu wengi hukiri, sema ....Nasema imefika mahali hapa sasa. Je, wewe ni Mkristo? "Mimi ni Mmethodisti," Vema, hiyo ni mbali na kuwa, kufanya mwenyewe ujulikane kama Mkristo. Vema, tazama kile wanachofanya Wamethodisti "Mimi ni Mbaptisti," Vema, tazama kile Wabaptisti wanachofanya. Mimi ni Mkatoliki," Tazama kile wanachofanya.

Unaona?

74 Lakini njia pekee ambayo wewe unaweza kwa hakika kuwa Mkristo ni kwa Kristo kujitambulisha Mwenyewe ndani yako. Jinsi gani tumepata kitu kichungu pale! Natumaini kila mtu mwenye kanda analipata hilo vile vile. Unaona? Unaona? Unaona?

Unasema, "Mimi ni Mpentekoste" Hilo halimaanishi lolote

75 Ni Kristo ajitambulishe ndani yako. Hiyo ni wakati Yeye amekutambua wewe.

Unasema, "Nilinena kwa lugha". Mashetani wanafanya hivyo vile vile.

"Nilipiga kelele." Waislamu, Wabudha, na kila kitu hupiga kelele.

Wahindi hulia kwenye ngoma ya nyoka. unaona? Hakika. Wote wanafanya Madhehebu, koo, na kila kitu kingine, hupiga mayowe na hupiga makelele. Hupiga makelele na kupaza sauti. kwenye mchezo wa mpira wa gongo.

Lakini Kristo anapojitambulisha ndani yako, anapojitambulisha Mwenyewe, basi wewe wafanana na Kristo. Ambalo, neno Mkristo humaanisha kuwa wafanana na Kristo. Huo hapo utambulisho wako. Vema. Sasa, na kwa kuwa Yeye ni utambulisho wetu, basi yatupasa tujitambushe na Yeye kwa kuishi kwa ajili Yake.

76 Angalia, Mungu alikuwa na kusudi lenye awamu tatu katika hili fumbo la siri kuu. Mungu, katika fumbo la siri Yake kuu ile aliyokuwa nayo kabla ulimwengu haujaanza,

Yeye alikuwa na kusudi lenye awamu tatu ndani yake. Na sasa kile tunachotaka kukiendea asubuhi hii ni hilo kusudi lenye awamu tatu ni nini? Sasa naamini, kwa msaada wa ...wa Mungu, Ambaye yupo hapa na Yeye -atatuonyesha hilo. Sasa, ikiwa Yeye alikuwa na kusudi lenye awamu tatu tunataka kujua hilo kusudi lenye awamu tatu ni nini.

77 Jambo la kwanza lilikuwa, kwamba Mungu alitaka kujifunua Mwenyewe kwa watu.

Yeye asingeweza kulifanya kama Yehova Mungu mkuu Ambaye amefunika anga lote, wakati, na Umilele wote. Asingeweza kufanya Yeye ni mkuu mno kuweza kufunuliwa kwa watu, kwa sababu ingekuwa ya kimiujiza kupindukia. Jinsi gani kile Kiumbe kikuu ambacho hakikuwa na mwanzo... ambapo ukishatoka nje ya mzunguko wa mamia ya mabilioni na matrilioni na matrilioni ya karne za anga na kuingia kusikokuwa na mwisho, ndani ya Umilele, na Kiumbe mkuu namna hii. Aliyekuwa vyote hivyo na hivyo ndivyo alivyo hadi leo.

78 Lakini kile Yeye alichotaka kufanya, Yeye alipenda Ubaba, kwani Yeye alikuwa Baba. Na njia pekee ambayo Yeye angejidhihirisha ilikuwa ni kuwa Mwana wa Adamu. Hiyo ndiyo sababu Yesu alidumu kusema "Mwana wa Adamu. Unaona, hawakujua kile Yeye alichokuwa akiongelea, wengi wao. Lakini sasa mnalielewa? [Kusanyiko linasema, " Amina."-Mh] Unaona? Yeye alitaka kujidhihirisha Mwenyewe. Hilo lilikuwa Lake, mojawapo ya awamu tatu za kusudi Lake ilikuwa ni kujidhihirisha Mwenyewe katika Kristo.

79 La pili, kuchukua nafasi ya utangulizi katika Mwili Wake wa waamini, yaani Bibi arusi Wake, ili kwamba Yeye aweze kuishi ndani ya watu.

80 Sasa, Yeye angeweza kufanya hilo ndani ya Adamu na Hawa, lakini dhambi iliwatenganisha, kwa hiyo sasa ingepasa njia fulani kulirudisha tena. Ee, jamani! Ee, sasa, hili, hili ni jambo la kina kwangu, hata kule kulifikiria tu. Unaona? Unaona kusudi la Mungu lilikuwa nini? Sasa kwa nini Yeye hakuwaacha Adamu na Hawa vile? Basi Yeye kamwe asingeweza kuonyesha utimilifu Wake., tabia Yake kikamilifu. Kwa sababu, Yeye angeweza kuwa Baba pale, hiyo ni kweli, lakini Yeye ni Mwokozi vile vile. Unasema "Unajuaje Yeye alikuwa hivyo?' Yeye ni hivyo, kwa sababu nimekuwa na ushirika Naye. Unaona? "Yeye ni Mkombozi, na ilipasa adhihirishe hilo. Na angelifanya hilo vipi? Kwa kupitia Kristo pekee. Angewezaje kuwa Mwana? Kupitia Kristo tu Angewezaje kuwa Mponyaji? Kwa kupitia Kristo tu. Unaona, vitu vyote vimekamilishwa katika yule Mtu mmoja, Yesu Kristo. Lo, jamani! Nilipo-nilipo .....

81 Ninapoliwazia na-naona tu madhehebu yalipita na kutokomea na kila kitu kingine vikienda tu, unaona mnapoona kusudi kuu la Mungu akijifunua Mwenyewe. Na kwanza ikiwa ni kule kujifunua Mwenyewe katika Kristo, "utimilifu wa Uungu katika mwili." Na kisha kuuleta "utimilifu wa Uungu katika mwili" ndani ya watu ili aweze kuchukuea nafasi ya utangulizi, usimamizi wa uongozi.

82 Usiku ule mwingine mmoja, kama hukupata ile kanda, nilihubiri hapa jioni moja, juu ya Mfungwa wa Yesu Kristo. Paulo, mtumwa. Unaona? Mungu anapokufanya kuwa mtumwa Wake, basi huwezi kufanya chochote ila kile Roho anachosema ufanye. Paulo, pamoja na akili zake nyingi, alifundisha... alifundishwa na Gamalieli kuwa kuhani mkubwa au rabi, siku moja. Naye alikuwa na matazamio makubwa. Kiakili alikuwa mtu mkuu katika taifa. Lakini ilipasa atoe kila kimoja cha hayo mhanga, unaona, awe sehemu ya Neno, kumdhihirisha Yesu Kristo. Yeye alijua ilikuwa ni nini kusema...

Alikuwa na wazo la kwenda mahali fulani, ndugu fulani walikuwa wamemwita, lakini alikatazwa na Roho kufanya mapenzi yake mwenyewe. Ee, laiti-laiti watu wa kiroho nusu wanaweza kuchukua hilo! Unaona?

Alikatazwa kufanya mapenzi yake mwenyewe. Angeweza tu kufanya ... "Roho alinikataza." Unaona? Yeye alikuwa mfungwa wa Kristo.

83 Ndipo, huyo mpiga ramli siku moja, ambaye yeye Paulo alijua alikuwa na uwezo wa kutoa yule pepo, lakini angeweza tu kufanya hivyo jinsi Mungu alivyotaka. Siku kwa siku alimfuata, akimlilia, lakini siku moja Roho alimpa ruhusa. Ndipo akamkemea yule msichana ile roho iliyokuwa ndani yake. Unaona? Yeye alijua kuwa mfungwa ilikuwa ni nini.

84 Musa, akili zake, ingepasa azipoteze ili kumpata Kristo, kuwa mfungwa. Basi Mungu alipouondoa ulimwengu wote ndani yake, na uwezo wote aliokuwa nao, na kusimama

kwenye Uwepo wa ile Nguzo ya Moto siku ile alishindwa kusema. Hakuweza hata, alisema hakuweza hata kuongea. Basi hapo Mungu alikuwa na mtumwa. Unaona? Huwezi kujaribu kwa uchunguzi wako mwenyewe. Basi Mungu ilimpasa amjalie huyu mtu, kumjalia nguvu ya kutosha ili kwamba weze kwenda chini kule.

Naye akasema, "Bwana, nilimwambia Farao kile Wewe ulichosema naye hakufanya."

Akasema, "Basi chukua hii fimbo yako." Mungu akinena, hilo ni Neno la Mungu, "nenda kule na uielekeze Mashariki, na uite inzi." Na mainzi yakaumbika, kwa sababu Yeye alikuwa na mfungwa ambaye Farao asingeweza kumlipa mshahara kwa chochote. Hakuna mtu mwingine yeyote angeweza kumgeuza aelekee kwingine. Yeye alikuwa mtumwa kamili katika minyororo ya Neno la Mungu aliyekuwa amefungwa kutii tu HIVI ASEMA BWANA.

85 Ee, ikiwa Mungu anaweza kujipatia watumwa wa aina hiyo! Sasa, hiyo ni wakati Yeye anaweza kudhihirisha nafasi Yake ya utangulizi, unaona? Yeye, Yeye ana mtu, au mtu, ambaye kwamba hajui chochote ila Kristo. Mnalipata ninalomaanisha? [Kusanyiko, "Amina." -Mh.] Vema. Hilo ni la pili.

Kwanza, kujidhihirisha kabisa Mwenyewe, Mungu katika Kristo.

Pili, kuchukua nafasi ya utangulizi, kwa hili, katika Kanisa Lake, ambalo ni Mwili Wake, Bibi arusi, mpaka Yeye awe mtangulizi ajidhihirishe Mwenyewe kupitia kwao. Vema.

Na, tatu, kurejesha Ufalme mahali pake panapostahili, ule ulioanguka kwa kwa dhambi kwa a jia ya Adamu wa kwanza, hadi kurejea kule nyuma wakati Yeye alipotembea jioni wakati wa kupunga kwa jua, pamoja na watu Wake, akaongea nao akawa na ushirika nao.

Na sasa dhambi na kifo vimewatenganisha na Uwepo na udhihirisho Wake wote. Je, mnalisoma? Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu kudhihirisha tabia zake-zake- zake zote, kile Yeye alichokuwa.

86 Kwa hiyo, ikiwa Mwamini wa Utatu yeyote hapa angejiachia kwa dakika, unaweza kuona kuwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu si Miungu watatu. Ni sifa tatu za Mungu yule yule. Unaona, ni udhihirisho. Yeye alikuwa Baba alitaka kuwa Baba. Yeye alikuwa Baba, Yeye alikuwa Mwana, na Yeye ni Roho Mtakatifu. Na Baba na Roho Mtakatifu ni Roho yule yule. Je, hamwoni? Mnalielewa? [Kusanyiko linasema, "Amina." -Mh.] Siyo miungu watatu. Mashetani walikuambia vitu hivyo, kuwafanya muabudu sanamu. Unaona? Ni Mungu mmoja akielezwa katika sifa tatu. Kuwa Baba, kuwa Mwokozi, kuwa Mwana, kuwa Mponyaji, unaona ni madhihirisho Yake.

87 Nataka kuendelea kwa ulaini kwa muda kidogo tu ili kwamba hata watu wanaosikiliza kanda wataweza kupata hilo wazo, wale wawezao kuona. Ingenichukua mzunguko mzima wa saa, siku nzima, kuelezea moja tu ya masomo hayo. Lakini nadhani nalifanya dhahiri vya kutosha kiasi kwamba unaweza kuona kile ninachokiendea. Unaona?

Mungu, aliyejidhihirisha katika Yesu Kristo, Ambaye alikuwa yote, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, "utimilifu wa Uungu katika mwili".

Sasa, "utimilifu wote wa Uungu katika mwili" unakaa katika Kanisa Lake, nafasi ya utangulizi wote. Yote yale Mungu aliyokuwa, Yeye aliyamwaga kwa Kristo; na yote aliyokuwa Kristo, yalimwagwa katika Kanisa, waamini.

Si dhehebu! Tutafikia hilo katika dakika chache, na italiondoa kutoka akilini mwako daima, unaona, kukuonyesha kinachosababisha hilo, kwa msaada wa Mungu, kama Yeye ataliruhusu lije kwetu .

88 Kusudi lake ni nini Sasa? Kujidhihirisha Mwenyewe kama Mwana, unaona, na, sasa ndani Yake ungekaa, "Utimilifu wa Uungu katika mwili." Nina Wakolosai imekaa hapa, mbele yangu hapa hapa. Unaona? Kwamba, katika Andiko lote, hilo ndilo lilikuwa kusudi la Mungu. Ndipo, na kupitia huu uzima wa huyu Mwana, msalaba wake, "ile Damu," linasema hapa, "ya msalaba Wake," kwamba aweze kujipatanishia na nafsi Yake Mwenyewe Mwili, Bibi arusi: ambaye ni Hawa, Hawa wa pili. Na Mungu hulitoa katika mfano, kama alivyofanya kwa Musa na wote. Jambo lile lile alilofanya katika Adamu na Hawa, akatoa mfano, kuwa walikuwa Kristo na Bibi arusi. Yeye ni Adamu wa pili; Kanisa

ni Hawa wa pili.

Na kadiri Hawa wa pili anavyofanya suluhu dhidi ya Neno, je, hafanyi jambo lile lile alilofanya Hawa wa Kwanza? [Kusanyiko linasema "Amina"Mh]. Akijaribu kusema, "Vema, ilikuwa kwa ajili ya kipindi kingine." Na tutalifikia hilo katika dakika chache zijazo, ikiwa Yeye alisema ilikuwa kwa ajili ya kipindi kingine. Itakuwaje kipindi kingine wakati Yeye ni Yeye "yule jana, leo, na hata milele?"

Lakini Mungu alilikusudia hilo na "kulificha machoni pa wenye busara na hekima na kuwafunulia watoto waliochaguliwa kimbele" ambao walichaguliwa kimbele kulipokea.

89 Hiyo ndio sababu tazama kwa kurudi nyuma vizazi vyote kila mara ile Nuru ilipogonga baadhi, waliikataa na kuitupilia mbali. Na Makuhani wakubwa walisimama pale, kulikuwa na Marabi toka kwa waalimu wakuu na mamlaka, kama wengine kadhaa, kama Nikodemu na wengine, mtu aliyeng'arishwa katika elimu, naye asingeweza hata kulielewa.

Na kulikuwa na wale makuhani wakubwa waliosimama pale, na marabi waliofundishwa katika lile Neno. Jamani, walilijua kiakili! Na Yesu akasema, "Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi, na kazi zake mnazifanya." Lifikirie hilo, watu watakatifu, usingeweza kuwaonyeshea kidole popote katika maisha yao, au maisha ya baba zao, au maisha ya babu zao, au maisha ya babu-wa babu-wababu-wa babu wa babu yao. ikiwa walifanya, walikufa katika aibu walipigwa mawe hadi kufa. Lakini hapa amesimama Yesu akiita lile kundi, "kundi la mashetani," watu wa kidini.

90 Sasa, ee, ule ufunuo mkuu sasa! Sasa ili kurejesha Ukoo Wake kuwarejesha sasa, ingempasa Yeye kuwaachia wapotee. Mnalielewa hilo? Yeye ingempasa kuwaacha watende dhambi, awaweke wawe na uhuru wa kuchagua watakalo.... Yeye, Yeye asingeweza kuwafanya watende dhambi, na kubakia angali Mungu na ndipo awaadhibu kutokana na jambo alilowafanya walitende.

Lakini alipomweka mwanadamu kwenye ushirika Naye, basi akamwacha mwanadamu atende kama mwenye kuchagua atakalo, unaona, jambo lile lile Yeye analokuletea leo. Unaona? Unaona? Unatenda jinsi upendavyo; wewe ni mwenye uhuru wa kuchagua upendavyo kufanya. Hivyo, basi ikiwa alimweka wa kwanza hivyo, hana budi amweke wa pili hivyo yampasa Yeye amweke kila mmoja hivyo hivyo. au Yeye alitenda kosa hapo mwanzo. Unaona? Ila kila mtu yuko kwenye msingi ule ule.

91 Sasa mtazameni Yeye, katika kulirudisha hilo; na kumwacha yule mtu afanye hilo, na hali akijua kuwa yeye angelifanya hii alijua yeye angelifanya hilo. Lakini hiyo ilisababisha nini? Ilimwonyesha sifa Yake kama Mwokozi. Na kusudi zima basi limeachwa katika Yesu Kristo kufanyika ... Mungu Mwenyewe kupata adhabu ya sheria Yake Mwenyewe, kifo, kufa, amkomboe yule mke aliyepotea kwa kumkataa Yeye.

Hawa alipoondoka kwenye Neno, aliondoka kwa mwenzi wake wa maisha. na kanisa linapoondoka kwenye Neno kwenda kwenye dhehebu linakataa na kufanya uasherati na dunia ya hekima ya mwanadamu, likikataa mamlaka ya Neno la Mungu. Hilo linaeleweka? [Kusanyiko linasema "Amina."-Mh.] Biblia ilisema, "Kufanya uasherati wa kiroho." Neno lolote katika Biblia lililokataliwa, au kama liliwekewa fasiri kama mtu apendavyo, huko ni kukataa kabisa na kufanya uasherati juu ya Mungu ambaye ni Mume wako. Mwanamke mzinzi kamwe haingii U falme wa Mbinguni, tunajua hilo. Unaona? Sasa, unaona, hicho ndicho Hawa alichofanya hapo kwanza.

92 Sasa angalia tena kusudi lake lenye awamu tatu ni nini? Alijidhihirisha Mwenyewe katika Yesu Kristo; kuja katika Mwili, kwa Yesu Kristokuchukua nafasi za utangulizi kwa (nini?) kurejesha Edeni, kurudisha kile kilichopotea. Hilo ndilo jambo pekee lililokuwa nje ya utaratibu. Mambo Yake mengine yote yalikuwa yakienda katika utaratibu.

Lakini ilimpasa amwache, amweke mwanadamu kwenye uhuru wa kuchagua atakalo, aanguke, ili kwamba Yeye awe Mkombozi, ili kuonyesha kile kilicho ndani Yake, unaona, sifa Yake ya Mkombozi. Kitu fulani ilipasa kipotee. Na jambo hasa, ambalo mwanadamu alianguka na kupotea, Yeye anakuwa Mkombozi wa hilo. Akitii sheria Yake Mwenyewe. Na asingefanya hilo kama Yehova mkuu aliyefunika anga lote, wakati, unaona, Yeye asingeweza kufanya hilo. Na ilimpasa awe Mwanadamu. Na alichukua ujamaa wa mwanadamu yule aliyepotea, amina, na kuwa Mwanadamu: Mungu aliyefanyika mwili!

Haleluya! Utafikiri nimesisimka; ila sijawa hivyo. Jambo fulani ndani!

93 Mungu alifanyika, kutoka Mungu, kuwa mimi, kuchukua dhambi zangu juu Yake, ili Yeye anifanye mimi kuwa Yeye, amina, kurejea kwenye kusudi Lake kuu la wana na binti za Mungu, kwani Yeye ni Baba wa Milele. Hiyo sifa ilikuwa ndani Yake, unaona ilibidi hiyo idhihirike.

Sasa unaona kusudi lake lenye awamu tatu? Unaona, kujiweka wazi Mwenyewe, Yeye anataka kufanyika ... . Sasa, du-dunia imepotea, sasa Yeye yampasa ajidhihirishe Mwenyewe katika Mwanadamu, ili awe Mwokozi kupitia upatanisho kwa Damu kutoka msalabani Mwake. Sasa ilibidi afanyike hicho, awe hivyo afe, ili kwamba aokoe na kujirejesha Mwenyewe katika Kanisa, awe na utangulizi katika Kanisa Lake.

94 Sasa kumbuka, haiwezekani, na haitawezekana, na kamwe halitakuwa na halijawahi kuwa dhehebu! Yampasa Yeye kuwa na utangulizi na Yeye ni Neno. Amina. Jinsi gani kanuni yoyote ya imani itaingizwa pale? Ni... inageuza kanisa kuwa kahaba, kuchukua neno la mtu ye yote la kanuni ya imani yoyote au dhehebu lolote. Imewekwa alama haraka katika Ufunuo 17 kama kahaba mkuu na makahaba; kanisa Katoliki likiwa ndiyo kahaba mkuu, na Waprotestanti wakiwa makahaba. Liko wazi tu kama vile ambavyo mtu yeyote angeweza kulisoma. Tumepitia vipindi vya Kanisa, na unaweza kuona hilo katika zile-zile kanda kama ukitaka. Ndiyo kabisa. Basi, chochote kile kinachojiunga na kanuni za imani nje ya Biblia ni kahaba mkuu mbele za Mungu. Na kufanya kile kile Hawa alichofanya; kutoka kwenye Neno, ambalo ni Kristo. Lo, jamani! Vema.

95 Sasa tunaona siri Yake aliyoificha katika nia Yake kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu. Sasa Je, mngependa kusoma kidogo juu ya hili? Hebu tulisome tu. Mnao muda mwingi? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Tutalisoma. Sasa hebu sote tufungue, kwa kusoma mara moja tu, vyovyote vile kwenye Kitabu cha Waefeso, na hebu tuanze kwenye -ule mlango wa Waefeso, kusoma na sasa somo la Jumapili likiendelea sasa, katika huku kudhihirishwa kwa awamu tatu kwa Kristo, hebu tusome.

Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu, ...

Sasa tazama, haukuandikwa kwa dunia, ila; ..... kwa watakatifu walioko Efeso wanaomwamini Kristo Yesu:

96 Unaingiaje ndani ya Kristo Yesu? Kwa kujiunga na kanisa? [Kusanyiko linasema, "hapana,"-Mh.] Kwa Kuzaliwa! "Kwa roho mmoja", 1Wakorintho 12, "sisi sote tulibatizwa kuwa Mwili mmoja," Unaona?

Vema hao ndio anaowazungumzia. Hilo halikuandikwa ulimwengu wa nje. Hatuwezi kunena na mwenye dhambi juu ya hili, kwa sababu hajui chochote kulihusu. Paulo hakuwaandikia wenye dhambi. Alisema, "Hili ni kwa lile-lile Kundi pale lililoko Katika Kristo Yesu."

Neema na iwe, na amani zotokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo.

Atukuzwe Mungu, baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetu bariki kwa baraka zote za rohoni (wapi?) katika ulimwengu wa roho ndani ya Kristo.

97 "Ulimwengu wa roho". Lo, jinsi gani natamani ningekuwa na muda! Nimeliweka alama hapa katika Biblia yangu, kuhusu Ulimwengu wa roho kile kilicho Ulimwengu wa roho. Ulimwengu wa roho, kwa muda mfupi tu, ni "nafasi ya mwamini katika Kristo," unaona, "pale mwamini anaposimama katika Kristo," Katika Ulimwengu wa roho.

Kama vile alivyotuachagua sisi.... (sikiliza kwa makini) na alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

Lini Yeye alituchagua sisi? "Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu," wakati fumbo lake kuu lililofichwa siri Yake kuu.

.... Yeye alituchagua katika Kristo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika (nini?) pendo:

Kwa kuwa alitangulia kutuchagua (nini?) kutuchagua ili tufanywe wana kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake,

98 Kuchaguliwa kimbele. Fumbo lipo hapo. Yeye, kabla Kristo au chochote kuwa duniani, unaona siri Yake kuu, kuwa Yeye alimchagua Bibi arusi. Alijua Hawa angeanguka, kwa kutokuliamini lile Neno, akijua kuwa angeanguka; lakini Yeye

angemchagua Bibi arusi ambaye hangeanguka, ambaye angeshikilia lile Neno bila kuangalia kile ulimwengu mzima u ungeweza kusema kuhusu Hilo. Wangeshikilia hilo Neno! Tangu asili walichaguliwa kusimama pale, "kufanywa wana kwa njia ya Yesu Kristo," kulichagua kanisa kimbele kuwa katika huo msimamo mkuu wa utukufu.

99 Sasa unaona siri Yake? Ya kufanya nini? Kumrejesha Hawa aliyeanguka kwani yeye alikuwa picha ya kimbele ya Kanisa. Na sasa angalia, kama Mungu alivyofungua ubavu wa Adamu na kumtoa Hawa, kwa nyama na damu yake mwenyewe; na kugawanya roho yake kutoka katika hali ya kiume na ya kike, (kuwa ya kike) na kuiweka ndani ya Hawa. Akachukua ubavu upande wake wa pembeni, na kumfanya Hawa kutokana na huo; kwa hiyo Mungu alifanya jambo lile lile, alichukua Damu na maji upande wa pembeni mwa Kristo. Na Kristo ni Neno, na kuchukua Neno na kulifanya Kanisa Lake, Hawa, unaona, analirejesha Kwake mwenyewe tena likakombolewa kwa

Damu ile iliyotoka katika Mwili Wake. Unaliona sasa? [Kusanyiko "Amina."Mh.]

Fumbo kuu la Mungu linafumbuliwa sasa, lile lililokuwa limefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, ila limeonyeshwa kimbele kwa jinsi ya mifano katika nyakati zote zilizotangulia. Sasa tazama, tunaona kuwa, kuwa Yeye- kwa Yeye alifanya hilo. Na hapa katika Waefeso, na sehemu nyingine nyingi, ila hilo litakupa vya kutosha ku... Sasa, katika nyakati zote, Yeye amekuwa akifumbua fumbo hili taratibu . Unaweza kuona sasa? Sasa kote katika .....

100 Je Yeye alifanyaje? Kulitokea nini katika mfano sasa? Alifungua sehemu ya pembeni mwa Adamu na kuchukua sehemu ya nyama yake, ambayo ilikuwa Adamu, kumfanya Hawa. Inampasa Bibi arusi awe Neno, kwani Yeye ni Neno. Hawezi kusimama kwenye mafundisho ya kanuni za imani. Yeye hawezi kusimama kwenye dhehebu. Yeye hawezi kusimama akitegemea msingi wa tabia nzuri. Inampasa asimame mwenyewe kwenye Neno, kwa sababu Yeye (Bibi arusi) ni sehemu Yake (Neno). Yeye alitolewa toka kwake Kristo. Unaona?

101 Na kuwa na hakika kuwa, Unyakuo wote sasa; Luther alikuwa sehemu yake, Wesley alikuwa sehemu yake, manabii walikuwa sehemu yake. Ikiwa wao ni-si sehemu .... Katika ufunuo tu kuwa walikuwa wakikamilisha mwili, miguu, vidole, mikono, na kadhalika mpaka Kichwa (tutafikia hilo baada ya dakika chache), unaona, hilo linafanya Unyakuo mzima. Ni Mwili wa Neno, ambao ni Kristo. Amina!

Nje ya Hilo, umepotea. Sijali jinsi wewe ulivyo mwema au uhusiano wako ni nini, au ushirika wako nini, au shirika lako la dini ni nini, umepotea, nje ya hilo Neno kuwa ndani yako.

102 "Kama mkikaa ndani Yangu, Neno, Neno Langu ndani yenu, basi ombeni lolote mtakalo," kwa sababu wewe na Neno ni kitu kile kile. Yeye anao utangulizi. Yeye anao utawala. Wewe .... wewe ni mfungwa Kwake. Ulimwengu umekufa. Huna chochote zaidi... Unaona watu wengine wote wakiishi jinsi wanavyofanya, lakini bado wewe hufanyi hivyo. Wewe ni mfungwa. Umefungwa nira pamoja Naye. "Nira Yangu ni laini." Umefungwa nira na Kristo, na Neno Lake. Nafanya tu kile ... kinachompendeza Baba, Na kama hamwezi kuamini kwamba Mimi Ndiye, basi aminini lile Neno Kamilifu mno, Tazama.

103 Angalia sasa, katika nyakazi zote, Yeye amekuwa akiliachia hili litoke, taratibu akiifunua ile siri, kupitia manabii na mifano. Sasa tunaweza tu kuliendelea hilo na akijidhihirisha Mwenyewe.

Yeye alijidhihirisha Mwenyewe kwa Musa. Mtazame Musa. Alizaliwa wakati wa mateso ya watoto. Alizaliwa awe mkombozi. Alifichwa katika nyasi, kama tu Yesu alivyopelekwa Misri. Alitokea. Akaenda juu mlimani, akarudi na zile amri.

Yesu alikwea juu mlimani, mahubiri yake ya kwanza hotuba ya mlimani akarudi chini akiwa na amri. "Mlisikia wakisema, wale wa zamani, "Usizini., Nawaambia, yeyote amtazamaye mwanamke na kumtamani, ameshazini naye." Mtoa sheria, Kuhani, Mfalme, Kiongozi, sahihi tu!

104 Yeye alijidhihirisha Mwenyewe katika Yusufu, aliyezaliwa katikati ya dhehebu, ndugu zake. Walimchukia bila sababu, kwa sababu yeye alikwa wa kiroho. Aliona maono. Mungu alikuwa pamoja naye, aliweza kufasiri ndoto. Na ndugu zake walimchukia. Aliuzwa kwa ... na ndugu zake, kwa karibu vipande thelathini vya fedha. Kama tu Yeye alivyouzwa na Yuda Iskariote, mmoja wa ndugu Zake, kwa vipande

thelathini vya fedha. Alitupwa shimoni kama kwamba amekufa. Hilo ni kweli. Baba na wengine waliambiwa kuwa alikuwa amekufa. Kwamba ametupwa katika shimo; akachukuliwa kwenda kwenye mkono wa kuume wa Farao.

Aliumia jinsi gani kule kwenye gereza la chini ya ardhi! Na-na kulikuwa na wawili waliookolewa.... Mnyweshaji mkuu na mwokaji mkuu, mmoja wa hao alipotea na mwingine akaokolewa bila shaka. Na yule-yule mnyweshaji mkuu. Mmoja wa hao alipotea na yule mwingine akaokoka. Kama tu pale Msalabani, wakati Yeye alipokuwa kwenye nyumba Yake ya gereza, akashambuliwa pale msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, Yeye alipokuwa mfungwa, mwizi mmoja alipotea na mmoja akaokolewa. Unaona, hivyo hivyo tu.

105 Ndipo akaja mkono wa kuume wa Farao, yule mfalme aliyemuota, yule aliyekuwa na ono kuwa angeketi miguuni pa mfalme, na mamlaka yote ya Misri alipewa yeye. Ono lake lilipasa litimie . Aliweza kujifunza hilo mara nyingi alipokuwa katika-katika lile gereza chini kule. Sharafa zake zikikua na kadhalika, lakini alijifunza hilo. Siku moja ono lake lilikuwa litimie.

Ingawa litakawia, lazima litukie! Kama nilivyonena usiku uliopita, au usiku wa juzi, Jumatano Usiku hapa kwenye ibada. Unaona, ilibidi litukie. Ni nabii aliyethibitishwa, na ilibidi litukie kwa sababu ni Neno la Mungu

106 Na Neno huja tu kwa nabii. Neno nabii humaanisha mfunuaji wa Neno la Kiungu lililoandikwa, kama tu anavyofanya mtabiri wa yatakayotokea mbele, unaona, au mwonaji. Tazama. Na mwonaji, jinsi, unajua anasema yatakayokuja, yeye amethibitishwa Kiungu kwa kuona kimbele na linakuja kutokea " Kukiwa na mmoja ambaye ni nabii, atasema, nanyi na kuwaambia mambo fulani yatakayotokea. Na kama hayakutokea, msimsikilize. Lakini kama yatatokea, basi Mimi nipo pamoja naye. Ni vyema mkamwogopa, kwa sababu Mimi Nipo pamoja naye, unaona. Ndivyo hivyo hasa. Hapo kuna udhihirisho, pale ambapo unajua kama ni Kweli ama la.

Mungu ananena kupitia Neno Lake, kwa watu Wake, kwa kutumia watu. Unaona, Mungu hunena tu kupitia mtu. "Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi." Mzabibu hauzai matunda. Matawi huzungumza, huzaa matunda ya Mzabibu.

Angalia, siku zote imekuwa namna hiyo.

107 Sasa tunakuta Yusufu, basi, kuwa hakuna mtu angeweza kuguza au kuja kwa Farao bila kwanza kumwona Yusufu. "Hakuna mtu awezaye kuja kwa Baba, ila kwa njia ya Mwana," Na Yusufu alipoondoka kwenye kiti cha enzi, walipiga tarumbeta, "Kila goti lilipigwa! Yusufu anakuja!"

Utukufu! Na siku moja kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri, Yeye atakapoondoka kwenye kiti cha Enzi cha Baba Yake, unaona, kuja mbele.

Kila mtu atashuhudia kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu. Ama wewe... Umeshachelewa basi. Lifanye sasa.

108 Sasa tunaona hilo kupitia mifano. Tungeweza hata kumchukua Daudi, kama nilivyosema muda mfupi uliopita, akiondoka kwenye kiti chake cha enzi, aliyekataliwa na watu wake mwenyewe; akipanda mlima ule ule. Mlima wa Mizeituni, kama anayekwenda kwenye gereza lake. Alikuwa anakwenda kwenye nyumba yake ya kifungo kwa sababu alikataliwa na ndugu na watu wake mwenyewe. Alikwea akilia. Huyo alikuwa Roho wa Kristo ndani yake, akikataliwa akiwa ameangalia Yerusalemu na kulia, na kusema ... "Yerusalemu mara ngapi ninge..." Mfalme aliyekataliwa. Miaka mia nane baadaye, Mwana wa Daudi alisimamia Yerusalemu, juu pale Yerusalemu na kusema, "Sasa saa yako imefika." Hiyo ni sahihi. Unaona?

109 Hayo mambo yote yalikuwa mfano Wake, katika mfano tu lakini bado ile siri ilikuwa imefichwa. Wale watu hawakujua kile walichokuwa wakifanya. Walijua tu waliongozwa na roho kufanya mambo fulani. "Sasa , Aliyazuilia hayo kufahamika hadi siku za mwisho, kwa ajili ya ule ufunuo mkuu. Lakini kuyadhihirisha, Alijidhihirisha Mwenyewe ndani ya Musa, na Daudi, na Yusufu, na Eliya, na katika nyakati zote zilizopita. U... tungechukua kila mmoja wa wale manabii, na kuleta maisha yao wazi na kuyaonyesha yakiwa yanamdhihirisha Yesu Kristo kikamilifu kabisa lakini bado hakutoa siri Yake yote; akisubiri kuifanya ijulikane katika siku za mwisho kama Yeye alivyoahidi, akisubiri ifahamike yote, unaona, kabla hajaidhihirisha, kama Yeye alisema jambo lote.

Kwa sababu,Biblia imeandikwa kwa mafumbo.Yesu alimshukuru Baba kwa hilo, unaona, kwamba limeandikwa kwa mafumbo.

110 Sasa, Kuja kwa Bwana kuko katika fumbo. Hatujui Yeye anakuja lini, anakuja namna gani, lakini tunajua anakuja. Unaona? Na kwa hiyo ndivyo siri zote za Mungu zilivyosubiri hii siku ya mwisho. Baada ya Yeye kukamilisha tayari ndipo anafunua na kuonyesha kile alichofanya. Lo, jamani! Hakuwahi kutoa siri Yake yote.

Ni kama hili tu, kulinganisha na Mihuri Saba. Sasa, Mungu alipomtumia Martin Luther kwa kutoka kwa lile kanisa la kwanza au kile kipindi cha kanisa, na alipomtumia John Wesley, na kwa pole pole aliwaleta nje, na alikuwa akifunua kwao kile kipindi cha kanisa, wakati sisi... yeyote anaporejea katika Biblia sasa na kugundua... Lakini katika siku za mwisho sababu likawa jambo kuu hivi, kwamba alisema juu yake hapa na kuonyesha zile Ngurumo Saba. Na magazeti ya Look na Life....

111 Gazeti la Life lilionyesha ile Duara ya Wingu na Nuru pale ambayo wasingeelewa, na bado hawalijui. Lakini hapa akisema, "Nenda kule na usubiri kufunuliwa kwa hizi siri," na kwa miezi kadha hapa kabla haijatokea, na ndipo ikatokea kwa vile vile tu jinsi Yeye alivyosema ingekuwa. Je mliona -Mliona katika ile picha? Hata yule Malaika upande wa kulia, alipokuwa akitokea, akishuka mbawa zake nyuma na kichwa Chake kimeangalia pembeni, iko moja kwa moja pale katika ile picha vile vile tu. Kwa miezi kadha kabla haijatokea, niliwaambia hapa kuwa, "Yeye anakwenda kuleta Mwili wa waamini pamoja; kufunua, kuunganisha miisho iliyopotea".

112 Luther anatokea na kupita hapa, alihubiri kuhesabiwa haki tu, akatwanga kwa nguvu katika kile kipindi. Hakujua kile kilikuwa kipindi gani. Akaja hapa Wesley, akapigapiga katika kipindi chake. Unaona? Na mikondo mingi ikachipuka humo, makanisa mengine yakainuka. Ndipo ikaja Pentekoste, wakatwanga kwa nguvu, na walijiunda kuwa shirika la dini na wakarejea tena moja kwa moja katika kifo; kama tutakavyoliona dakika chache zijazo, moja kwa moja nyuma katika "kifo".

Na ndipo ukaja ufunuo wa siri, kufunua haya yote yamekuwa juu ya nini. Pale, ambapo haya mafundisho madogo, kama Luther alivyoleta katekismo na kila kitu kingine; na Wesley akaleta hiki, kile na kingine: na mambo haya mengine; na Pentekoste ikaleta shirika la dini kama tu hao wengine na ubatizo wa "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," na mambo, bila kujua hata kidogo tofauti na hivyo kwa sababu... Ndipo anarudi katika siku za mwisho na kuchukua siri zote hizi na kuzieleza kwa uwazi, kulifunua. Kwa nini? Yote ni siku za mwisho ambapo hii siri kuu aliyokuwa nayo Mungu katika moyo Wake inafunuliwa.

113 Je mnalipata hilo? [Kusanyiko linasema Amina."-Mh.] Ikiwa utashindwa, rejea kwenye hii kanda tena. Sijui nitakuwa nanyi kwa kirefu zaidi kiasi gani. Kumbukeni hii ndiyo kweli ya HIVI ASEMA BWANA. Ndiyo ile kweli. Ni andiko.

Kama zile siri saba za ile Mihuri Saba ya mwisho, siri zake. Ile mihuri ilikuwa imeshavunjwa, na kila kipindi kimekuja, na wameacha pale kutawanyika kwingi. Na Mungu, Yeye hakupenda kuwa Hilo litawanyike. Yeye anarudi na kuchukua yale mambo, yale mafundisho waliyoanza, na kuyatoa nje na kufunua jambo lote. Jambo lile lile analifanya sana katika kufunua siri ya Kristo, jinsi Yeye alivyokuwa kusudi la Mungu lenye awamu tatu kwa ajili ya Kanisa! Lo, jamani! Amemwachilia Yeye atoke, Anafunua!

114 Kufunua, Webster anasema, Fanya lijulikane fanya ijulikane, na hasa," Webster anasema, "Katika Kweli ya Kiungu," kile Ufunuo unachomaanisha, Ufunuo ni njia ya Kristo ya kufanya Mwenyewe ajulikane kwa Kanisa Lake.

Sasa tunakwenda kusema, "Sasa, Ndugu Branham, unasema tu hili." Sasa, Hatutasema, sema tu hili.

Sasa angalia, Yeye alijijulisha Mwenyewe kwa Petro, Sasa kama unataka kuliwekea hili alama, na sisi..... Kama unataka kulisoma tuta... Tutalisoma, ikiwa unataka, katika Mtakatifu Mathayo 16-15 na 17. Nitalinukuu. Walipotoka Mlima wa Ugeuzo alisema "Watu hunena Mimi Mwana wa Adamu ni nani?"

115 Wengine hunena, ee, wanafikiri Wewe ni 'Eliya' na wengine hunena kuwa wewe ni 'mmojawapo wa manabii", "Yeremia," au baadhi yao." Lakini sio hilo alilouliza Yeye.

Akasema, "Ninyi mnadhani kuwa Mimi ni nani sasa? Sasa pale anazungumza na Kanisa. Unaona?

"Watu hufikiri Mimi ni nani?"

Leo, "Yeye ni mwanafalsafa; hii dini ya kijamii. Yeye alikuwa mtu mwema. Tunaamini fundisho Lake ni sahihi. Ni somo la kuliishi. Nadhani litatufanya vyema sote, ikiwa tutaliishi. Tunapaswa kuwa na Makanisa yetu, yetu - yetu na kadhalika". Hiyo ni Santa Claus, kama hadithi ya Santa Claus.

Siyo udhihirisho wa kanisa fulani ambalo tungedhihirisha jambo fulani.

Ni uhai ambao huishi wewe mwenyewe, ila Yeye huja ndani yako na kuishi Yeye Mwenyewe, nawe unakuwa mtumwa; kwa akili yoyote ya kibinadamu. Unaongozwa na Roho. Na unajuaje?

116 Sasa, unasema, :Naweza kujua nilikuwa ninarukwa na akili. Huenda mtu anayerukwa na akili hufanya vile."

Lakini kama ukiwa na nia ya Kristo, Kristo hujidhihirisha Mwenyewe kupitia wewe, inaonyesha kuwa ni Yeye na siyo .... akili zako hazijaruka.

Baadhi ya watu wakiwa wanaangalia mambo juu juu tu hutoka nje na kuwa vichaa. Vema, hilo, tunajua hilo ni kosa. Huyo ni shetani akijaribu kuiga jambo halisi kabla halijafika hapa. Unaona? Wao daima ni wa bandia.

Unaona?

Lakini mtu halisi, achanganyikiwe mawazo yake na kufikiri kwake! Hawezi kuja akiwa kipofu namna hiyo. hapana, bwana. Unakuja na akili zako timamu na Kristo anakuchukua na kujidhihirisha Mwenyewe. Na sasa, kwa ulimwengu, wewe ni mtu kichaa.

Sasa, ikiwa wewe ni mwendawazimu, wewe ni mwendawazimu kweli, basi hakuna lolote, shetani hawezi kukudhibiti kikamilifu. Atakufanya ufanye kila kitu kinyume na hili Neno.

Lakini Kristo anapokuchukua, Yeye atalidhihirisha lile Neno moja kwa moja kupitia wewe kwa sababu ni Yeye. Yeye ni Neno!. Unaona? Na ndipo unaweza kuona udhihirisho wa Kristo. Sio kugusagusa juu juu kwa namna fulani, ila Kristo halisi akijidhihirisha Mwenyewe moja kwa moja kupitia kwako. Ni zuri jinsi gani!

117 Sasa tazama, Yeye alisema, "Mnasema Mimi ni nani?" Anauliza Kanisa, wale waliokuwa kumi na wawili. Kati ya mamilioni wa siku ile, Yeye aliwauliza wale Thenashara, Kanisa Lake.

Katika mamilioni katika siku za Nuhu, aliuliza wanane. Lo Unaona?

Naye akasema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo i takavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu, unaona, ambapo nafsi nane ziliokolewa."

Sisemi kutakuwa na wanane watakaookolewa sasa. Sasa usilielewe hilo kwa makosa. Sijawahi kusema hilo. Sijui ni wangapi wataokolewa, wanakwenda kuokolewa katika hiyo ambapo ni .. ile dakika ya mwisho kukunyakua lile kundi dogo. Litakuwa kundi dogo, nitawaambia hilo. "Kwani mlango ni mwembamba, na njia imesonga, na ni wachache waionayo."

118 Lakini ule Mwili mkuu uliokombolewa katika nyakati zote utakapotokea basi patakuwepo na kiti kikubwa cha enzi pale! Ufunuo 7 unadhihirisha hilo, "idadi kubwa, ambayo hakuna mtu awezaye kuhesabu," kutoka katika nyakati zote, wale waliotembea katika ile Nuru ya Biblia kadri ilivyofunuliwa kwao. Na sasa tunajua kuwa Wesley alikuwa na Nuru zaidi ya Luther. Tunajua Pentekoste walimulika zaidi ya Wesley. Unaona? Hakika, ilimzidi.

Kwa sababu ilifunguliwa kidogo kidogo, kama ilivyofanyika chini kote kupitia manabii, na kadhalika, mpaka lilipojulikana kikamilifu, "Uungu katika mwili ndani ya Kristo.

Na sasa Kristo ndani y a Kanisa anaanza tu kujulikana. Jambo lote ni ufunuo wa Mungu kumrejesha Hawa kwenye nafasi yake sahihi tena pamoja na Mume wake. Tazama, na Mungu ni Mume wa Kanisa, na Kanisa ni Bibi arusi Wake.

119 Sasa, Petro, alipoita, akasema, "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

Sasa tazama, kasema "Heri wewe Simoni Bar-yona", ambalo lamaanisha, "Mwana wa Yona." Unaona? "Heri wewe, kwa kuwa nyama na damu havikukufunulia hili.

Hukujifunza hili kamwe kutoka shule fulani. Bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili", Angalia alichomwambia, "Juu ya mwamba huu..." Huyo ni Petro, Mbegu ya Mungu iliyochaguliwa kimbele iliyopokea hii Nuru na kupewa funguo za Ufalme. "Juu ya mwamba huu wa ufunuo wa Yesu Kristo ni nani,: Yeye ni Mungu mtimilifu aliyedhihirishwa." "Juu ya mwamba huu..." Siyo Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu; na Yeye kuwa Nafsi ya pili. "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu kamwe haitautingisha, kamwe haitalishinda." Unaona? "Nitalijenga Kanisa Langu juu ya huu mwamba," Ufunuo wa Yesu Kristo.

120 Tazama, Kristo ndani yako humfanya Yeye kuna kiini cha Uhai wa Ufunuo. Unaona? Uzima wa Kristo ndani yako humfanya Yeye kiini cha ufunuo. Kristo katika Biblia, hufanya Biblia u funuo kamili wa Kristo. Kristo ndani yako hukufanya wewe uwe ufunuo kamili wa jambo lote, unaona, kile Mungu anachojaribu kutenda.

Kuzaliwa upya ni nini basi? Ungesema, "Vema, Ndugu Branham, Kuzaliwa upya ni nini?" Ni ufunuo wa Yesu Kristo kibinafsi kwako. Amina! Unaona? Sio ulijiunga na kanisa ulishikana mikono, ulifanya jambo fulani tofauti ulisema kanuni za imani, uliahidi kuishi kwa mfu-mfumo wa sheria fulani. Lakini Kristo, Biblia, Yeye ni lile Neno lililofunuliwa kwako. Haidhuru kile mtu yeyote anachosema, kile kinachotokea, ni Kristo; mchungaji, kasisi chochote kiwacho. Ni Kristo ndani yako, ambao ndio ufunuo ambao kanisa lilijengwa juu Yake.

121 Unasema, "Vema, mimi ni Mlutheri, Mimi ni Mbaptisti, Mimi ni Mpresbiteri." Hilo halimaanishi chochote,halimaanishi [Ndugu Branham anafyatua kidole chake-Mh.] hilo kwa Mungu si kitu, sio kufyatua kidole chako.

Ni kitu gani? Ni Kristo akifunuliwa, Naye ni Neno. Na Neno linapofunuliwa, linajidhihirisha Lenyewe. Unaona? Hilo ni kusudi la Mungu kwa ajili ya Kristo, ilikuwa kujidhihirisha Mwenyewe, kuchukua sheria Zake Mwenyewe na kuishi kwa sheria Zake... na kutimiza sheria Yake, kwa kifo. Na Kristo, Mungu, alikufa katika mwili, ili kwamba dhambi ilaaniwe katika mwili, kwamba Yeye aweze kujiletea Kwake Mwenyewe Bibi arusi wa utukufu, aliyekombolewa, atakayeamini katika Neno la Mungu pekee; na si kupokezana kama Hawa alivyofanya kupokea dhana za kiakili za mwanadamu.

Mnaliona? Hilo ni wazo la Kristo. Hilo ni wazo la Mungu. Kuzaliwa upya kunafunua hili.

122 Na kama mtu anasema amezaliwa mara ya pili na kujaribu kuweka hizi ahadi za Kristo, katika hizi siku za mwisho, kuziweka kwenye kipindi kingine, kumfanya Kristo wa jana lakini si wa leo, basi huyo mtu au huyo mwanadamu amekuwa katika madanganyo ya Shetani. Na kama yule mtu anasema kwamba analiamini Hilo, na halijidhihirishi Lenyewe kwake?

Yesu alisema, katika marko 16, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; ulimwenguni mwote, na kwa kila kizazi." Watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya, na-na udhihirisho huu wote mkuu wa karama ambazo zingefuata, kwamba, "watafanya!" Siyo, wataweza kufanya yawapasa kufanya." Watafanya! Na mbingu na nchi zitapita lakini Neno Lake halitapita.

123 Hivyo ni Kristo akijidhihirisha Mwenyewe katika mtu binafsi ikiwa yeye ni msomi au kama yeye ni - hajui ABC zake. Nusu ya mitume hawakujua, unaona, lakini walimjua Kristo. Hawakumtilia maanani kamwe Petro na Yohana, kwa kujua kuwa walitokea seminari fulani. Wao walisema, "Walitilia maanani na kuzingatia kuwa wale walikwishakuwa na Kristo, wakati walipomponya yule kilema, tazama, pale langoni. Walijua ya kuwa wao - wao walikwishakuwa na Kristo.

124 Kuzaliwa upya ni Kristo, ni ufunuo. Mungu amekufunulia hii siri kuu, na hiyo ni kuzaliwa upya. Sasa unakwenda kufanya nini unapolikusanya hilo kundi lote pamoja, ambapo ule ufunuo unapatana kikamilifu, na Mungu akiudhihirisha kupitia katika Neno Lake kwa matendo yale yale, mambo yale yale aliyotenda, akidhihirisha wazi Neno! Ee, kama Kanisa lingejua tu nafasi yake! Litajua siku moja. Litakapojua lenyewe ni kitu gani, ndipo Unyakuo utatokea. Sasa tazama.

Unasema, "Ndugu Branham, lakini hilo-hilo siyo... "Ee, ndiyo,ni hivyo vile vile. Ni ile kweli.

125 Je, uliona? Paulo hakuwahi kumfahamu Yesu kwa kumwona. Paulo hakuwahi kumfahamu Yeye. Njia pekee ambayo Paulo alimfahamia ilikuwa kwa ufunuo, kwa ono.

Hiyo ni sahihi [Kusanyiko, "Amina,"] Paulo alimfahamu Yesu kwa ufunuo, kama tu Petro alivyomfahamu.

Petro alikuwa anamwona katika mwili, lakini hakumfahamu katika mwili, kwa sababu Yesu alisema hivyo. "Mwili na damu havikukufunulia hili. Lakini Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili jambo, kuwa Yeye ni Neno la Mungu, na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu." Petro hakumfahamu Yeye kwa kumwona mwili. Watu walitembea naye na kumshika, na kila kitu.

126 Paulo alikuwa na jambo fulani kuu kuliko alilokuwa nalo mtume mwingine yeyote. Mnaona?

Walisema, "Vema, - ni-nina ufunuo mwingi zaidi yako Paulo, kwa sababu, unajua, nilitembea Naye. Nilikwenda kuvua samaki pamoja Naye siku moja. Nilimsikia akiongea. Aliketi kwenye mtumbwi pamoja nami, na hakika aliniambia, "Hebu twende hapa na tuvue samaki mahali hapa, na tutapata samaki wengi zaidi. Na tulifanya hivyo." Unaona? Unaona? "Tulimwona akifanya mambo.

Lakini Paulo alimwona baada ya Yeye kufa, kuzikwa na kufufuka tena, na kujidhihirisha Mwenyewe katika Nguzo ya Moto ile iliyowaongoza wana wa Israeli. Akijua.... Paulo akiwa Myahudi, asingeita ile kamwe "Bwana" ila awe ameona udhihirisho, Yeye alirejea yule jana, leo na hata milele. Akasema, "Paulo:, kwa maneno mengine, "Mimi ni Mungu yule yule leo ambaye nilikuwa jana. Niko hapa, katika Nuru ile ile, ile Nguzo ya Moto Musa aliyozungumza nayo, katika kichaka kinachowaka. Si ajabu aliweza kutenganisha sheria na neema, katika Kitabu cha Waebrania; alikutana na ile ile Nguzo y a Moto. Akasema, "Mimi ni Yesu, unayeniudhi.

127 Na yupo hapa leo, katika tabia ile ile, kwa ile ile Nguzo ya Moto akijidhihirisha Mwenyewe na akijithibitisha Mwenyewe yule y ule, akifunua ile siri ya Mungu aliyofichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Unaona?

Paulo alimjua Yeye kwa - alimjua Yeye kwa ufunuo tu, Petro alimjua Yeye kwa ufunuo.

Alitembea Naye, akazungumza Naye. Kwa hiyo, unaweza kuliweka hili Neno. Sasa, nilisema hivi punde kuwa Yeye alikuwa Neno. Sasa, msomi anaweza kukaa na kusoma hilo Neno mpaka aweze kuifunga akili yako kwa namna yoyote, unaona, ikiwa atataka kufanya hivyo, kwa sababu yeye ni mwerevu, mwenye akili. Mchukue kasisi wa Kikatoliki au si zaidi sana hivyo, kama mwanathiolojia mzuri hasa aliyefunzwa katika Biblia. Ndugu, Mbaptisti au Mpresbiteri, au kitu fulani, atakufanya ufikiri kuwa hujui chochote, unaona, inapokuja katika kuongea. Kitu gani. Unaona, kwa sababu amemfahamu

Yeye katika Mwili, lile Neno. [Ndugu Branham anaipigapiga Biblia yakeMh.]

128 Lakini njia pekee unayookolewa kwayo ni kwa kumjua Yeye kwa Ufunuo!

Kama naweza kuchukua, naweza kuchukua fundisho la Kipresbiterian na kukufunga wewe Mpentekoste usiweze kujua. Naweza kuchukua fundisho la Kibaptisti na kuwaonyesha ninyi Wapentekoste mambo milioni ambayo hamjui chochote kuyahusu. Hilo ni sahihi lakini silo lenyewe. Hilo silo Kanisa lake. Hilo silo Kanisa Lake.

Kanisa Lake ni Yeye Mwenyewe aliyefunuliwa. (Amina! Mnaliona?), na kudhihirishwa na Neno Lenyewe, kuwa Yeye ni Mungu. Unaona?

129 Unaweza kusema, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," baadaye na kubatizwa katika hilo? Wapagani! Sawa! Unawezaje kusema unamjua Yesu Kristo, Yeye ni Neno, wakati, hakuna Andiko katika Biblia, hakuna sehemu ambapo yeyote aliwahi kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu"?

Na ninyi- na ninyi watu wa Yesu-tu, mkitumia tu jina la "Yesu" kwa ajili ya ubatizo! Mimi binafsi nawajua akina Yesu wanne au watano, mwenyewe. Kwa hiyo mnaona kule dhehebu lenu linakowapeleka? Hilo ndilo giza, udhihirisho wa Kaini, aliyeleta matunda badala ya damu. Unaona?

130 Lakini ufunuo unakuja kupitia ile Damu, unaona, kupitia Yesu Kristo. Ambaye ni Damu ya Mungu, Damu ya kuumba katika tumbo la uzazi la Maria. Na Paulo alimfahamu Yeye kwa ufunuo. Hivyo ndivyo tunavyomjua Yeye leo, ni njia pekee ungeweza kumjua Yeye. Siyo kusema, "Mimi ni "Mmethodisti" Hilo halimaanishi chochote" Mimi ni "Mbabtisti." Hilo halimaanishi chochote. "Mimi ni Mkatoliki" Hilo halimaanishi chochote. Lakini kwa ufunuo, ambao Mungu amelifunua Neno kwako. Yeye ni Neno. Na Neno

unajuaje limefunuliwa, linaishi Lenyewe na linajidhihirisha Lenyewe kwa kupitia kwako. Lo!

Makanisa yameusahau ule ufunuo mkuu siku nyingi. Hiyo ni sahihi. Ufunuo wa ile Kweli, wameusahau. Walikwenda kwenye ....

Sasa, Luther alipoinuka, alikuwa mtu mkuu. Alikuwa na ufunuo wa siku ile. Lakini kulitokea nini? Kundi la watu watukutu liliingia ndani, wanaokata nywele kwa kusawazisha juu ya kichwa, kama tunavyoita leo, na wenye mitindo ya kiulimwengu na wote wa aina hiyo walikuwa pale. Na-na-na, jambo la kwanza unajua hilo lipo.

131 Ule Msemo Kama uli-ulijua tu tarakimu za Biblia, na kujua kile Elvis au au Ricky humaanisha nini kwa Maandiko! Aha-aha. Kama tu, kwa nini Yesu... Unasema, "Hakuna lolote kwa hilo, jina lako." Hakuna? Hilo jina lingeweza kuja tu katika hizi siku za mwisho, kwa ajili ya hawa watu wa siku za mwisho.

Kwa nini Yesu alibadili jina la Abram kuwa Abraham, baadaye Sarai kuwa Sara? Kwa nini ni alibadilisha Sauli kuwa Paulo? Kwa nini alibadili Simoni kuwa Petro, na kadhalika? Unaona, hakika inamaanisha jambo fulani. 260 Lile jina lisingeweza kunenwa mpaka leo hii. Hiyo ndiyo sababu tuna hili jambo la kuzimu tulilo nalo duniani leo, kwa sababu ya mambo kama haya. Jamii ya mwanadamu yote imeharibika. Imekwisha, unaona, na hiyo ndiyo sababu iko hivyo.

132 Angalia sasa, Luther alikuwa sahihi, katika siku zake. Naye alikuwa na ufunuo; lakini mara tu alipoondoka, angalia kile walichofanya. Wesley alikuwa na ujumbe; angalia kile ulichofanya. Wale Wapentekoste wa zamani wa kwanza walikuwa na ujumbe; tazama kile walichofanya. Walikusanya kundi la watu pamoja kama tu sawasawa na jambo lile lile ambalo...

Mungu, kwa neema, aliwatumia Israeli Nguzo ya Moto, nabii, dhabihu na akajionyesha Mwenyewe miongoni mwao, na kuwatoa Misri, kupitia Bahari ya Shamu. Nao walitaka sheria, ili wawe na waheshimiwa wakuu waweze kuwa na jambo la kufanya katika hilo. Na walifanya nini? Waliachwa jangwani kwa miaka arobaini, watangetange, na hakuna hata mmoja wa lile shirika la dini aliyevuka kamwe.

133 Kalebi na Yoshua, ndio wawili tu waliosimama na kusema, "Tunaweza kuichukua, kulitazama Neno la Mungu."

Kila mmoja wao alikufa jangwani. Na Yesu alisema walipotea Milele, moja kwa moja, baada ya Yeye kuonyesha baraka Zake na uwezo katika nyakati zao; kama Luther, Wesley, na kadhalika. Alisema hivyo? Wakasema, "Babu zetu walikula mana jangwani."

Yeye akasema, "Na kila mmoja wao alikufa." Hiyoni kutenganishwa Milele na Mungu. Mizoga yao iliangamia jangwani, Unaona? Walikufa.

Lakini Mimi ni Mkate wa Uzima ushukao kutoka Mbinguni kwa Mungu. " Wasingweza kuliona hilo. Wasingeweza tu kuliona hilo.

134 Vema, kanisa limesahau hilo, tangu kitambo kirefu. Walipokea ujumbe wa kiakili, wasomi, wanachama, maarifa, badala ya ufunuo wa ile Kweli ya Neno.

Sasa tazama hapa wanasema leo. Unaamini kuwa Mungu alituagiza kwenda ulimwenguni kote, na kuponya wagonjwa, na kuhubiri Injili, na kutoa pepo? "Ee, ee, ndiyo, nadhani hilo ni sawa, lakini ..." Unaona?

135 Mwanamke fulani akiongea nami siku ile nyingine, alisema, "Vema, makanisa yote yamo katika amani kila moja na lingine".

Nikasema, "Hakuna hata moja linalopatana na lingine." Kuna Wakatoliki wamesimama pale. Nikasema, "Vipi kuhusu ninyi? Wewe ni Methodisti na yule ni Mkatoliki, mnapatana ninyi kwa ninyi?" Nikasema, "Huyu papa alikuja kuwaunganisha pamoja, hilo ni jambo jema kwa watu wote wa aina hiyo".

Lakini Kanisa la Mungu halihusiani na hilo, kwa chochote. Liko nje kutoka kwenye hilo kundi lote. Aha-aha. Vema ndiyo bwana.

Unataka kuunganisha hayo pamoja, na mmoja anaamini katika jambo fulani na mwingine; Mmethodisti ananyunyizia, Mbaptisti anazamisha na wote wawili wakikana Roho Mtakatifu katika utimilifu Wake wa uwezo. Walisema, "Tulipokea Roho Mtakatifu pale tulipoamini.

136 Biblia ilisema, "Mlipokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?". Tofauti iko hapo. Unaona? Hiyo ni sahihi. Unaona?

Nao wanasema, "Sisi ni kanisa Katoliki. Tulianza zamani. Tulifanya hili". Wamethodisti husema, "Tumeweka msingi juu ya Biblia."

Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Sasa hilo liko wapi? Aha-aha. Unaona? Naam. "Kazi nizifanyazo nanyi mtazifanya," kila kiumbe, mtu yeyote amwaminiye, Yeye sasa hilo liko wapi?. Hayo ni Maneno Yake. "Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno Yangu hayatashindwa kamwe". Sasa hilo liko wapi? Unaona? Ee, linaonyesha tu!

137 Ni kitu gani? Ni hali ya mbegu chotara. Tazama hapa, unachukua nafaka nzuri kubwa ya hindi chotara, na unachukua lile hindi chotara. Chotara ni hindi zuri. Hebu ulipande, unapata nini? Shina dogo linatokeza namna hii, na linageuka kuwa njano na kudhoofu. Hiyo ndio jinsi kila dhehebu lilivyo, wakati likiwa chotara likiwa na maneno ya mwanadamu yaliyochanganywa na Maneno ya Mungu. Litakuja kwenye ishara na maajabu, na kile Yesu alichosema kuhusu kule kuliamini Neno, na inabadilika kuwa rangi ya njano, na kusema, "Hatuwezi kulipokea," na kurudi nyuma.

138 Kama tu vile walivyofanya wale wapelelezi wengine waliokwenda wakavuka na kuangalia Kanaani. Walikuja pale na kusema, "Ee, tunaonekana kama panzi mbele yao! Hatuwezi kuwashinda! Waamaleki wataweza, yote haya, kile wanachokwenda kufanya! Nao wakarudi.

Nao Kalebi na Yoshua, wakiwa mbegu njema, amina, kwa Neno la Mungu, walijua Mungu alisema, "Nawapa ile nchi." Walisema, "Twaweza kushinda bila shaka!"

Inategemea umezaliwa wapi. Kama umezaliwa kutokana na Neno la Mungu, Neno la Mungu limechukua utangulizi katika Kanisa Lake. Hilo ndilo ambalo Yeye alikufa kwa ajili Yake. Hilo ndilo kusudi Lake, kuwa angeweza kutimiza lengo, awe na utangulizi Wake ukitenda kazi katika Kanisa Lake. Hebu Neno la Mungu ling'are kwanza haidhuru chochote kingine kinaonekana vipi. Sijali kama wasomi wanasema hili, lile na lingine, haihusiani kwa lolote na hilo. Neno la Mungu lilisema hivyo, na sisi twaweza kushinda bila shaka. 279 Mhubiri mmoja aliniambia "Kama nikihubiri hilo kanisani mwangu," akasema, "Nitahubiria nguzo nne kanisani."

Nikasema, "Ningehubiria hizo." Ndiyo, bwana. Neno la Mungu lilisema hivyo. Tunaweza kufanya hilo. Mungu alisema ulifanye. Amina!

139 Ee, naam, wanajiwekea kisingizio kwa hilo. Unaona? Hiyo ndiyo sababu wao ni vipofu kwa Ujumbe wa wakati wa mwisho, hizi siku za mwisho wakati Mungu anapojithibitisha Mwenyewe. Wanajaribu kuweka Hili katika kundi la wanaoshirikiana na mapepo na mizimu au lingine, ee, (Niliite nini?) vichaa, mazingaombwe au kitu cha jinsi hiyo. Unaona. Wao-wao wanajaribu kulifanya hili liwe kitu fulani ambacho lenyewe haliko hivyo.

Kama tu walivyofanya yeye alipokuwa hapa, Yesu alipokuwa hapa walimwita "Beelzebuli; mpiga ramli," sasa wanasema ni namna ya uwezo wa kusoma mawazo ya wengine. Unaona? Wakati wanajua kuwa Yeye angeweza kusimama pale na kutazama watu na kutambua mawazo yaliyoko mioyoni mwao. Biblia alisema hivyo.

Vema, Waebrania mlango wa 4 hausemi, "Neno la Mungu lina nguvu, tena lina makali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, na laweza kuyatambua mawazo ya moyo"? Naye alikuwa lile Neno. Na lile Neno linapokuwa utangulizi ndani ya mtu, jambo lile lile linatokea tena, kwani ni Neno! Amina! ... tazama jinsi unaweza kujikwaa juu ya hili kuanzia sasa na kuendelea. Liko pale wazi kikamilifu. Unaona? Vema

140 Hiyo ndiyo sababu wao ni vipofu, kama vile ilivyokuwa katika siku za Kristo, alipokuwa duniani. Lo, jamani! Wanayumbayumba jinsi ile ile. Walisema, "Yeye ni Bellzebuli. Beel- ..." Walimwona Yeye angeweza kulifanya, kwa hiyo wakasema, "Yeye tu ni ... Yeye alizaliwa mtoto haramu, na mtu aliye tofauti na wengine wote. Amepagawa tu na pepo fulani Yeye ni - Yeye ni Msamaria kule, na anaye pepo ndani yake. Hivyo ndivyo anavyofanya hilo".

141 Yesu alisema, "Nitawasamehe juu ya hilo," unaona, wakiita Neno la Mungu, matendo ya Mungu roho mchafu. Yeye alisema, Nitawasamehe juu ya hilo. Lakini siku fulani Roho Mtakatifu atakuja, na neno moja kinyume Naye kamwe halitasamehewa, katika ulimwengu huu au ule ujao, au ile siku kuu. Halitasamehewa." Kwa hiyo, unaona,

hilo limeandikwa wazi katika Maandiko.

Kwa hiyo watu watakapokuja kwenye ile siku, haidhuru ni msomi, au ni wa dhehebu kubwa jinsi gani, limehukumiwa. Lazima wahukumiwe! Wamemkufuru Roho Mtakatifu walimwita "mtakatifu anayejiviringisha" na kitu kingine ambacho kina jina lisilo na utamu au kitu kama hicho. Na Kanisa la Mungu yapasa listahimili hilo wakati wote.

142 Hata Paulo mbele y a Agripa, alise,a "Kwa njia ile iitwayo 'uzushi' "yenye maana ya wendawazimu, hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu." Yule msomi mkuu mashuhuri ilimpasa aje sehemu ile, "kwa njia ile iitwayo ya "uzushi".

Kwa nini? Lilifunuliwa kwake. Ile Nguzo yaMoto ikining'inia mbele yake, akasema, "Mimi ni Yesu, Mungu mkuu niliyekuwa kule jangwani na Musa, Mimi ndiye, na ni vigumu kwako kuupiga mateke mchokoo."

Paulo akiwa amesimama pale, alijua maisha yalikuwa hatarini, akasema" Kwa njia ile iitwayo ya 'uzushi' hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu." Iliitwa hivyo kwa sababu ilifunuliwa kwake ile iliyokuwa Kweli kuu ya Kristo ni nini.

Na leo, watu husema, "Ni dhehebu."

Ni Yesu Kristo, kuzaliwa upya, aliyefunuliwa ndani yako kuwa Yeye anao utangulizi kwamba aweza kudhihirisha Maneno Yake. Na lolote aliloahidi katika siku hizi za mwisho, anaweza kulitimiza, kupitia Mwili Wake wakati Yeye anapotenda kazi. Amina! Ni Neno la Mungu halisi tu likidhihirishwa. Tazama. Vema.

143 Kama ilivyokuwa katika siku za Kristo, Mungu Mwenyewe hushikilia ufunguo wa huu ufunuo wa Kristo. Unaamini hilo? [Kusanyiko, "Amina".] Shule za thiolojia haziwezi kuliona hili. Yesu alisema hivyo. Kama unataka kulisoma. Sasa, katika Mtakatifu Mathayo 11:25 na 27. "Nakushukuru, Baba, Mungu wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, na ukawafunulia watoto wachanga." Unaona? Unaona? Sijali...

Tazama wasomi wa siku ile, wale Wayahudi, watu waliotukuka sana. Mashirika yao Mafarisayo, Masadukayo na akina Herode, na chochote ambacho wangeweza kuwa. Unaona? Mashirika yao makubwa yote, na Yesu alisema, "Ninyi ni vipofu; mnawaongoza vipofu. Isaya alizunguza vema juu yenu", Mna masikio, na hamwezi kusikia, na mna macho ambayo hamwezi kuona." kwa kuwa Isaya alizungumza hili katika Roho, kwa hiyo Mungu wa Mbinguni amepofusha macho yenu. Mnatenda kama Hawa alivyofanya, akikubali upande wa akili, bila kujua lolote kuhusu Roho wa Mungu. Kwa hiyo, hawatatumbukia wote shimoni, kiongozi na kipofu vile vile"? Kiongozi atatumbukia pamoja na kipofu, kwa sababu yeye ni kipofu pia. Kiongozi anatumbukia, huyo ni kipofu, akimwongoza kipofu, wote wanatumbukia shimoni.

144 Na Mungu peke yake anashika huu ufunguo! Alidhihirisha jambo lile lile katika Andiko lililopita pale muda mfupi uliopita nilipolisoma, Yeye aliposema, "Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?" 294 Naye Petro akasema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

Akasema, "Heri wewe Simoni, mwana wa Yona. Mwili na damu havikukufunulia hili. Baba Yangu aliye Mbinguni! Juu ya ufunuo huu hapa, peke yake, nitalijenga Kanisa Langu. Milango ya kuzimu haitalishinda kamwe. Unaona? Sasa unaona?

145 Kwa hiyo hakuna shule, hakuna wanathiolojia, hakuna mafundisho ya Biblia miongoni mwa shule yoyote, yanayojua lolote kulihusu Hili. Hawawezi kujua lolote kuhusu Hilo Haiwezekani wao kujua chochote kuhusu hilo. Mungu ameficha zile hisi, za kulijua Hilo, kuanzia walimu wateule hasa na kila kitu kinginecho.

Ni jambo la kibinafsi, la mtu mmoja mmoja ambaye Kristo amewafunulia wao.

Na kama ukisema, "Amefunuliwa kwangu," na kisha yale maisha ambayo Kristo aliyaishi hapa katika Biblia, Maisha hayo hayo yamo ndani Yake, hayajifanyizi Yenyewe ndani yako, basi una ufunuo usio sahihi.

146 Kama nikiweka uhai wa boga katika uhai wa mti wa mpea, ungezaa maboga. "Kwa matunda yao mtawajua," Sahihi kabisa. Na ikiwa mwanzo unaweka mti, mzabibu, na kutoa matawi ya mzabibu; chipukizi la kwanza ililotoa linatoa zabibu, linalofuata likaleta malimao, na linalofuata likatoa mapea, linalofuata likatoa matofaa, kuna namna fulani ya upandikishaji pale, ambapo kila tawi huzaa kwa namna yake yenyewe. Kila dhehebu litazaa uhai wake lenyewe. Lakini kama ule mzabibu wa asili ukitoa chipukizi lingine,

utazaa zabibu kama ulivyofanya mara ya kwanza.

Na kama uzima- Uzima wa Kristo unauleta mwili mwingine wa waamini, utazaa tunda ambalo ule wa kwanza ulizaa. Wataandika Kitabu cha Matendo nyuma yake, kwa sababu utakuwa ule ule. Uzima ule ule. Unaona ninalomaanisha? Huwezi tu kuliepuka hilo. Ni maisha ya Kristo ndani yako, yanaingizwa ndani yako, na Roho Mtakatifu Mwenyewe akiishi maisha Yake kupitia ndani yako.

147 Viongozi vipofu wawaongozao vipofu!" Angalia, Mungu anashikilia huu ufunguo peke Yake. Hakuna Mwanathiolojia anayeweza kukuambia; halijulikani. Limefichwa mbali na wao. Hawajui lolote kuhusu Hilo.

Kwa hiyo shule, unaposema, "Nina Ph., LL.D.," unafanya tu... kwangu, na naamini, na kwa Mungu na kwa mwamini halisi wa kweli, inamaanisha wewe uko tu mbali kiasi kile, uliacha njia tu. Mungu hafahamiki kwa elimu. Yeye hafahamiki kwa namna ya kulielezea Hilo.

Mungu hufahamika kwa urahisi na kwa ufunuo wa Yesu Kristo hadi kwa mtu asiyeweza kusoma na kuandika. Unaona. Si thiolojia yako. Ni ufunuo wa Yesu Kristo. "Juu ya huu mwamba nitalijenga Kanisa Langu". Hakuna miamba mingine inayokubalika, hakuna vitu vingine vinavyokubalika hakuna mwamba mwingine wa Kirumi, hakuna mwamba mwingine wa Protestanti, hakuna shule nyingine, hakuna kingine chochote, ila juu hasa ya ufunuo wa Yesu Kristo katika kuzaliwa upya. Yeye anazaliwa ndani pale na Yeye anaingiza Maisha yake Mwenyewe na maisha yako yamekwisha. Na Maisha ya Kristo yanajitokeza Yenyewe kwa watu kupitia kwako pamoja na utangulizi; kwamba wanaona maisha yale yale na matendo, na ishara, na maajabu, aliyofanya Yeye yanatenda jambo lile lile kupitia kwako. Nje ya hayo, hata mengine yote yaliyosalia kujishughulisha nayo hakusaidii kitu kabisa. Tazama ufunuo mkuu wa Mungu ukizidi kukunjuliwa.

148 Kwa ukosefu wa huu ufunuo ndio sababu tuna migawanyiko tofauti mingi miongoni mwetu, na dhihaka nyingi. Migawanyiko mingi miongoni mwetu, ni kwa sababu watu hawana ule ufunuo. unaona, walimu hawana ufunuo.

Paulo baada ya ufunuo wake mkuu wa Kristo, alisema, katika 1Wakorintho sura ya pili. Uwe na hakika unalisoma hilo unapoliandika. Tazama! Lo! Alisema, "Sikuja kwenu na hekima". Mtazame yule mtu aliyekuwa na hekima, lakini mtazame huyo mtu aliyekuwa msomi. "Sikuja kwenu na namna ya maneno." Wakorintho wa Kwanza, ile sura ya pili ya Wakorintho wa Kwanza. Ee, natamani ...

306

Vema, hebu na tusome tu. Jinsi ... Mnaweza kusimama kwa dakika moja na tusome aya moja au mbili? [Kusanyiko, "Amina,"-Mh.] Ningependa tu kulisoma ili ninyi-msingeweza kucha ... Litawafanya hata watu wanaosikiliza kanda kugeuka na kufungua hapo vyovyote vile, tuwape nafasi.

Wakorintho wa Kwanza, sura ya pili. Msikilize huyu mtume mkuu hapa Paulo, mtumishi wa Mungu mwenye elimu. Hebu tutazame hapa.

...Mimi, Paulo, mimi nilipokuja kwenu, sikuja na ufasaha wa maneno ... wa hekima, niwahubiri siri ya Mungu. Sikuwahi kusema, "Mimi mi ni Daktari fulani." Unaona?

Maana naliazima nisijue lolote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulubiwa.

Nami nalikuwako kwenu katika hali ya udhaifu, na hofu na matetemeko mengi.

....neno langu na-na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu-za nguvu.

149 Hapo, unaona Hapo ndipo pana Injili. Unaona? Yesu alisema, "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili," Hakusema, "Nendeni mkafundishe." Alisema "Enendeni mkahubiri." Kwa maneno mengine "Onyesheni" nguvu, na ishara hizi zitafuatana nao." Kufundisha tu haitoshi. Inahitaji Roho Mwenyewe hasa kuonyesha hizi ishara. Unaona? Sikiliza hili.

Ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.

Lo, jamani! Unaona, kumbadilisha mwanadamu! Siyo katika kile niwezacho kukikanusha, na kusema, "Yeye siyo yule yule" wakati Yeye ni yule yule. Kama nikifanya hivyo, inaonyesha, kwangu, ni-ni ... Hakika, mtu mmoja aliniambia, angenionyesha

kuwa yeye hana ufunuo, ufunuo wa Mungu katika awamu tatu. Unaona? Sasa, na ...

Walakini katika udhaifu ... kati ya wakamilifu: ila si hekima ya dunia hii, wala ya hao wanaoitawala dunia hii, wanaobatilika:

Bali twanena hekima ya Mungu katika .... siri, unaona siri ya Mungu yenye awamu tatu, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazima tangu milele kwa utukufu wetu;

Ambaye wenye kuitawala dunia hii hawajui: hakuna makasisi, rabi-rabi ... (samahani) .... au chochote, hawakujua lolote kulihusu, maana kama wangaliijua, wasingelimsulubisha Bwana wa utukufu.

Ulisema, "Unakosea kuhusu marabi na wahubiri kule." Nani alimsulubisha Yeye? Aha-aha

Ee, tungeweza kuendelea na kuendelea. Lisome, unaona, endelea, okoeni wakati kwa sababu tuna... Hatujachelewa bado, lakini bado tuna mengi ya kusema hapa kama Mungu atatusaidia sasa. Ukosefu wa hili sasa ....

150 Na Paulo huyu mtu msomi mkuu hakuwahi kusema kwa watu maneno yake makuu ya kithiolojia,. Alilipokea Neno la Bwana kwa unyenyekevu, na aliishi Neno kwa hiyo lilijidhihirisha kupitia kwake. Aliishi Kiungu mpaka wakamwona Yesu Kristo ndani yake, mno, mpaka wakataka leso yake, waichukue na kuiweka juu ya wagonjwa. Hayo ndiyo maisha ya Kristo.

Sasa tazama wengine husema, Ee, vema, unaona, Eliya alifanya hilo muda mrefu uliopita aliilaza fimbo yake; lakini ee, hizo zilikuwa siku za Eliya." Sasa, ulimwengu ulifikiria hivyo. Makasisi wanaoenenda kiakili na mambo, na makanisa ya siku ile walifikiri hivyo.

151 Lakini kwa waamini, walijua tofauti. Waliona ufunuo wa Kristo uliokuwandani ya Eliya, kitu kile kile kilikuwa ndani ya Paulo, kikidhihirisha aina ile ile ya maisha, kwa sababu yeye alikuwa nabii. Unaona? Alitabiri mambo yaliyotokea kwa usahihi jinsi ilivyokuwa, na walijua huo ulikuwa utambulisho wa Mungu wa kumtambulisha nabii. Na wao walijua kuwa Yeye alikuwa nabii wa Mungu. Usingeweza kuwatoa katika hilo hata kidogo. Hata walipomwona Petro akitabiri yale mambo na yakatokea, walisema, "Hebu kivuli chako kipite juu yangu tu." Amina! Hilo ndilo kanisa. Hao ndio wanaoliamini hilo. Ndiyo bwana. Lilifunuliwa na ....

Mbona, Je, Paulo alisema, "Kwa sababu ni-nona PH.-, LL.D., na kadhalika, wananiamini?" Hapana. Alisema, "Niliyasahau mambo hayo yote, hekima ya mwanadamu." Akasema, "Ilipasa nife na namjue Yeye katika nguvu ya ufufuo Wake. Hilo ndilo ninakuja nalo kwenu, pamoja na uthibitisho wa nguvu za Mungu."

152 Hilo lilikuwa nini? Kumfanya Yesu Kristo yeye yule jana, leo , na hata milele. Kazi ile ile aliyofanya Yesu, Paulo alifanya hivyo hivyo. Na walimwona Mungu Baba mkuu aliyejithibitisha katika kile kichaka kilichokuwa kikungua, alilithibitisha kwa Paulo, na hapa lilikuwa likithibitishwa.

Naye ni yule katika kila kipindi. Mungu katika awamu tatu.... "jana, leo na hata milele." Nini? Mkombozi; katika Kanisa Lake; utangulizi katika ufalme unaokuja. Amina! Unaliona? Kikamilifu tu kama liwezavyo kuwa.

153 Lo, tazama! Roho Mtakatifu ni mfunuaji pekee wa ufunuo wa Kiungu wa Kristo. Hakuna shule iwezayo kufanya hilo. Hakuna msomi awezaye kulifanya. Hakuna mtu, awe msomi kiasi gani, Mcha Mungu jinsi gani, au chochote kile, hakuna mtu awezaye kufanya hilo.

Ningeweza kuumiza sana hapa. Ni wangapi ni wakristo waliozaliwa mara ya pili; inueni mikono yenu, waliojazwa kwa Roho Mtakatifu? Vema, hapa tunaendelea basi. Vema. Angalia

Na Yeye atalifanya tu kwa wale waliochaguliwa kimbele. Ndiyo kabisa. "Wote alionipa Baba watakuja, na hakuna mtu ajaye. Nisipopewa na Baba kwanza." Unaona?

154 Angalia makuhani wakisema, "Huyu mtu ni Beelzebuli. Yeye ni mpiga ramli. Yeye ni pepo."

Na yule mwanamke akitembea pale, akiishi na waume sita; alikuwa akiishi na watano, na wakati ule alikuwa na wa sita. Na Yesu akasema. "Nenda ukamlete mume wako hapa."

Akasema, "Sina mume."

Akasema, "Ndiyo, umekuwa nao sita. Umekwisha kuwa na watano, na unayeishi naye sasa si mume wako".

Akasema, "Bwana!" Nini? Ile Nuru iliigonga ile Mbegu.

Ilipowagonga wale makuhani, walisema Huyu Mtu ni mpiga ramli". Unaona, hakuna Uzima pale. Mbegu chotara kuja kuwa shirika la dini lakini ilikufa pale pale.

155 Lakini huyu mwanamke hakuwa mbegu chotara. Akasema, "Bwana, nafahamu!" Naweza kuona macho yake mazuri na makubwa yaking'aa namna ile, machozi yakitiririka mashavuni mwake, Kasema, "Bwana nakuona ya kuwa Wewe ni nabii. Namtazamia Masihi. Na yule Masihi atakapokuja, Yeye atafanya jambo hili hasa. Yeye atatuambia mambo haya."

Akasema, "Mimi Ndiye

Ee Bwana! Aliacha mtungi wake "Yuko hapa! Njooni, mwone Mtu aliyeniambia mambo" ilikuwa nini? Ile Nuru iliigonga ile Mbegu. Ule Uzima uliokuwa pale ukatoka. Jambo lile lile leo

156 Lakini mwananathiolojia atasema, "Sasa subiri kidogo. Nitatafuta ikiwa fulani, Mchungaji Moody alisema, au ..."

Mchungaji Moody anahusikaje juu ya hili siku hii? Mchungaji Moody aliishi katika siku yake, lakini sio sasa. Hakika Luther aliishi katika siku yake, lakini si katika siku ya Wesley. Wesley aliishi katika siku yake, sio katika siku ya Pentekoste. Wapentekoste waliishi katika siku yao, lakini wako mbali na Hili katika saa hii. Tuko katika saa ya mwisho. Hakika.

Mashirika yao ya dini, na kuhangaika kwao, huthibitisha kuwa Lenyewe halipo pale. Neno halijawahi kuthibitishwa kwa usahihi; ila tu kwenye uwezo wake, mbegu, madhehebu. Na wangeunda dhehebu, ndipo waweke ile mbegu za zamani za magugu yanayoota penye mawe ya chokaa ndani pamoja na ngano halisi; ikafa mara moja. Zao lilikwenda kuwa gugu linaloota kwenye mawe ya chokaa, sahihi, Waridi Mwitu la kijani kibichi na mapupu aha-aha, unaona, iliendelea kurudi huko ilikufa pale pale. Ndipo wakafyeka shamba na kuanza tena, wakapanda mbegu halisi, na baadhi ya hizo zikaota nayo yakalisonga Hili kabisa.

157 Lakini ndipo, Mungu akasema, katika hizi siku za mwisho. Yeye angeleta watu waliooshwa katika Damu Yake, Nao walikuwa wamechaguliwa tangu asili kuwa pale. Yawapasa kuwa pale. Mungu alisema hivyo. Na ingefunua... Na ile ile ishara, "Nitamtu-..." Malaki 4, na kile yeye angefanya , "kurejesha tena," kurudisha, katika siku za mwisho, haya mambo makuu aliyoahidi, yangeleta ufunuo. Kitu gani kinge.. Yeye angefanya nini, Malaki 4? Ilikuwa kurejesha Imani ya Baba kwa watoto. Unaona? Hiyo ni sahihi kuleta jambo lile lile. Nguzo ya Moto ile ile; ishara zile sahihi za maajabu yale yale, Yesu yule yule; kumfanya Yeye yule yule, kumhubiri Yeye kuwa yule yule kumthibitisha Yeye yule jana, leo, na hata milele.

Nitarejesha" asema Bwana, "miaka yote ambayo mdudu wa Methodisti, na madumadu, na Baptisti na Katoliki; na yote yaliyoliwa na wadudu, ile Imani, mpaka ikawa kisiki cha kidhehebu ambapo hakuna mbegu iliyobaki pale. "Lakini nitarejesha tena,asema Bwana, "miaka yote" Nini? Ishara zote na maajabu waliyoyaacha. Nitayarudisha kule nyuma moja kwa moja kwenye ule mti wa asili tena, na nitalirejesha," asema Bwana. Yule nabii alikuwa nabii aliyethibitishwa. Maneno yake sharti yaje kutimia. Amina.

158 Roho Mtakatifu pekee ndiye mfunuaji wa ufunuo wa Kiungu wa Kristo na ni hivyo amekuwa katika vipindi vyote. Kumbuka, vipindi vyote! Ni nani ambaye Neno la Mungu lilikuja kwake? Nabii pekee. Hiyo ni sahihi. Je, hiyo ni sahihi? Na yampasa nabii athibitishwe kwanza. Sio kwa sababu yeye alisema kuwa yeye alikuwa nabii; kwa sababu alizaliwa akiwa nabii, na kuhakikishwa kuwa nabii, na kila alichosema kilikuwa kwenye Neno kabisa na kulitukia, basi kila kinginecho chochote unakiachilia mbali. Unaona? Ilikuwa, Neno la Bwana lilikuja tu kwa njia ya Roho Mtakatifu. Biblia ilisema, "Watu wale wa zamani, waliongozwa na Roho Mtakatifu, unaona wakaandika Neno."

159 Tazama. Yohana Mbatizaji kamwe asingemfahamu Yesu kama haikuwa Roho Mtakatifu kumwonya Yeye. Hiyo ni sahihi. [Kusanyiko linasema, Amina."-Mh.]

Yohana Mbatizaji, yule nabii mkuu aliyekuja, na kusema "Kuna mmoja aliyesimama miongoni mwenu saa hii. Na Mtu wa kawaida amesimama hapa mahali fulani, ambaye ni Mwana-Kondoo wa Mungu." Yohana akasema "Basi nashuhudia, nashuhudia. Nimemwona Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu akishuka kama hua kutoka Mbinguni, naye akakaa juu Yake. Na Sauti ikasema, 'Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu. Ninayependezwa

Naye.'"

Ilikuwa nini? Roho Mtakatifu alisema, :Nitamwonyesha."

160 Hiyo ndiyo njia pekee uwezayo kumfahamu Yeye leo, njia pekee utakayopata ufunuo wa awamu tatu wa Mungu ni kwa Roho Mtakatifu. Na njia pekee hili liweze kutokea ni wewe ulichaguliwa tangu asili kuliona hili. Kama si hivyo, kamwe hutaliona. Ikiwa hukuchaguliwa kimbele kuliona, kamwe hutaliona; kwa sababu ile Nuru inaweza kumulika na ukaenda zako na kuidhihaki na kukanusha, kwa wazo la kiakili. Wakati Mungu yule yule, Mwenyewe akijidhihirisha Mwenyewe na kuhakikisha, unaona, ila, ikiwa hukuwekewa kuliona, hutaweza kuliona.

161 Mungu hakuwahi kusema tu, "Nitamchagua huyu, nimchague yule, ila alijua kwa Lake ... Sababu aliweza kuchagua kimbele, kwa kuwa Yeye hana mwanzo wala mwisho, kwa hiyo Yeye alijua kila kitu. Yeye hana kikomo, hivyo, hivyo, kwa hiyo Yeye alijua kila kitu. Alijua mwisho. na aliweza kuona mwisho tangu mwanzo. Yeye ni Mungu. Ikiwa hawezi kufanya hivyo, Yeye si Mungu. Ndiyo bwana. Yeye hana mwanzo wala mwisho. Vema

162 Yohana asingeweza kamwe kumjua Yeye, hapana, bwana, kama Roho Mtakatifu hangekuwa amemwonyesha. Unaona jinsi Mungu anavyoficha siri Yake kwa wenye elimu ya juu na kila kitu? Tazama, kila mmoja wa wale watu ...? Na urahisi hulifunua kwa yeye aliyechaguliwa kimbele kuliona. Tazama hapa! Wengine wakiwa wamesimama pale na wala hawakuwahi kamwe kumwona yule hua, hawakuwahi kuisikia Sauti, kwani ilitumwa pekee kwa ile mbegu iliyochaguliwa kimbele. Iliyochaguliwa kimbele! Hakika, ilikuwa imechaguliwa kimbele!

Mbona, Isaya, miaka mia saba na kumi na miwili kabla Yeye hajazaliwa, katika Roho, aliinuka akiwa nje ya hisia za kibinadamu, na kusema, "Sauti ya mtu aliaye nyikani, 'itengenezeni njia ya Bwana yanyoosheni mapito Yake."

Basi, ikiwa Isaya angeweza kuliona, je, Malaki asingeweza kuona jambo lile lile kwa ajili ya nabii wa mwisho aliyechaguliwa kimbele akiwafungia manabii wote wa Agano la Kale, yule mkuu... yule nabii mkuu akisimama pale mwishoni mwa Kipindi? Unaona? Yeye anasema imechaguliwa kimbele! Hakika, yeye alikuwa hivyo. Malaki alimwona vile vile.

163 Yesu alisema, "Kama mtaweza kulipokea, huyu ni yeye yule aliyenenwa, 'Namtuma mjumbe Wangu mbele Yangu,' Malaki 3 'aitengeneze njia mbele Yangu.'" Unaona? Hakika yeye alichaguliwa kimbele aone ule ujumbe. Si ajabu aliweza kutazama pale na kuona yule hua akishuka ile Nuru ambayo ilikuwa kule jangwani pamoja na Israeli ikija, ikishuka.

Mungu Mwenyewe, akisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa kukaa ndani Yake", Mungu na mwanadamu wakiwa Mmoja.

"Nashuhudia", Yohana alisema, "Nimemwona yule Mwana pekee wa Baba. Mimi ni shahidi wa hilo" Amina!

Ndilo hilo. Urahisi! Kwa mhubiri mzee, baba yake; baba yake alikuwa mwanathiolojia mkuu unajua, yeye alitoka chuoni. Ilionekana kana kwamba angerudi kwenye dhehebu la baba yake. Hilo lisingekuwa mapenzi ya Mungu.

164 Mungu alipomgusa kwenye kuzaliwa kwake nyuma kule, na alipokea Roho Mtakatifu miezi mitatu kabla hajazaliwa. Naam, bwana. Maria alipokwenda juu kule, na Yohana mdogo alikuwa na umri wa miezi sita katika tumbo la uzazi la mama yake, na hakuwahi .... Ile misuli midogo ilikuwa bado haijatembea. Na Maria aliogopa... Ile misuli midogo ilikuwa inakua, lakini Elizabeti mama yake asingeweza kuhisi uhai. Na Maria alipokuja na kumshika, na kumkumbatia, kaweka mikono yake, akaweka mikono juu yake. Unaona? Na kusema, "Mungu amenena nami, nami nitapata mtoto vile vile."

"Wewe na Yusufu mmeoana?"

"Hapana."

" Maria, hili lawezekanaje."

"Roho Mtakatifu atatia uvuli juu yangu, na kutaumbwa ndani yangu. Nami nitamwita Jina Lake 'Yesu'. Yeye atakuwa Mwana wa Mungu.

Na mara tu lile neno 'Yesu' liliponenwa, Yohana mdogo akaanza kuruka, na kushangilia, na kurukaruka katika tumbo la uzazi la mama yake.

Akasema, "Abarikiwe Bwana Mungu! Kwani katokea wapi mama wa Bwana wangu? Mama wa Bwana wangu!" Lo, jamani kwani katokea wapi mama wa Bwana wangu? Maana pindi tu sauti ya kuamkia kwako ilipoingia masikioni mwangu, kitoto changu kichanga kiliruka kwa shangwe ndani ya tumbo langu".

165 Si ajabu yeye hakutaka seminari, kitu fulani cha kumtia yeye kasumba ya jambo fulani au lingine. Alikuwa na kazi muhimu. Alikuwa mtu wa nyikani, alikwenda nyikani na kusubiri. Mungu alimwambia nje kule, kasema, sasa na kumfunulia. Lo ule ufunuo wako tena. "Nami nitakuambia Yeye ni nani. Wewe u nabii. Neno linakujia wewe. Unajijua wewe u nani. Yakupasa uje."

Hilo linajibu swali la Jumapili iliyopita. Unaona? Unajijua wewe u nani, Yohana. Ila ukae kimya; usiseme lolote. Nenda nje kule. Na utakapomwona Huyu, kutakuwa na ishara ikitoka Mbinguni, kama Nuru, hua atashuka. Huyo atakuwa Yeye utakapomwona Yeye."

166 Hiyo ndiyo sababu, Yesu alipoteremka majini, Yohana alitazama na kumwona yule hua akishuka chini, akasema, "Tazama Mwana- Kondoo wa Mungu! Yupo pale! Yeye ndiye atakayeichukua dhambi ya ulimwengu."

Yesu alikwenda moja kwa moja majini hadi kwake. Macho mawili ya Yohana yalikutana na macho mawili ya Yesu. Walikuwa mabinamu wa pili, kwa mwili. Maria na Elizabeti walikuwa mabinamu wa kwanza. Macho yao yalikutana. Kulikuweko Mungu na nabii wake, amina, wamesimama pale.

Yohana alisema, "Mimi nahitaji kubatizwa na Wewe. Mbona Wewe waja kwangu?"

Yesu akasema, "Kubali hivi sasa, ila kumbuka, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote".

167 Kwa nini Yohana alilifanya? Kwa sababu Yeye alikuwa Dhabihu. Yohana alikuwa nabii, yeye alijua; na Dhabihu yapasa ioshwe kabla haijatolewa. Lo! lo! Naye alimkubali Yeye, naye akambatiza.

Naye alipofanya hivyo, tazama, Mbingu zikafunguka, lo, jamani, na yule hua akashuka juu Yake, na Sauti ikasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa ambaye napendezwa kukaa ndani yake." King James inaliweka, ninayependwa kukaa ndani Yake ". Kwa hiyo ni namna yoyte unayotaka kuligeuza, jambo lile lile, "kukaa ndani au.... Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa kukaa ndani Yake" au kukaa ndani," lolote utakalo kuliweka, jambo lile lile. Vema.

Basi tunaona lilifunuliwa kwake. Wengine wakiwa wamesimama pale hawakusikia chochote kulihusu. Roho Mtakatifu pekee analifunua.

168 Ni hivyo hivyo Yeye anapojifunua Mwenyewe kwa Paulo, Mbegu nyingine iliyochaguliwa kimbele

Kulikuwa na Paulo akitembea kule, angeweza kusema, "Kama nikilipata lile kundi, nitalirarua vipande vipande,kwa sababu mimi ni Daktari Sauli, Nililelewa chini ya Gamalieli. Natoka kwenye Chuo cha Biblia cha Moody...." au kinginecho, unaona. "Mimi, mimi ni msomi. Najua lile ninalolisema. Nitalichana vipande vipande lile kundi la watakatifu wanaojiviringisha, Nami nakuambia, baba mkuu mtakatifu nipe tu ruhusa kwenda chini kule, na nitamkamata kila mmoja wa hao wapiga kelele chini kule. Tutayakomesha haya mambo ya uponyaji wa Kiungu.

Akaiweka mfukoni mwake, akasema, "Niko njiani kwenda"

Na siku ile, jamani, kwenye saa tano mchana, Nu-Nuru ilimulika usoni mwake, naye akaanguka chini ardhini.

169 Kwa nini? Alikuwa Mbegu iliyochaguliwa kimbele. Mungu alisema "Nilimchagua yeye naam. Nami nakwenda kumwonyesha mateso makubwa atakayopata kwa ajili ya Jina

Langu. Nitamtuma kwa mataifa na kumfedhehesha katika kila namna ambayo wanaweza kufedhehesha, lakini bado yeye atachukua Jina Langu.

Paulo alishuka chini, wakati huo hadi mambo yote ya kidini yalipomtoka, chini kule u pande wa nyuma wa jangwa, kwa miaka mitatu na nusu. Chini kule Arabuni, mpaka akajifunza Neno. Naye Neno akawa yeye.

Naye akawa mfungwa; akarudi hapa katika minyororo ya upendo! "Uzoefu wangu wote wa seminari umekwisha! Mimi ni mfungwa kwa Yesu Kristo. Amina! Filemoni, ndugu yangu, mimi ni mfungwa wa Yesu Kristo. Naweza tu kunena na kusema kile yeye anachoniambia."

170 Mungu anahitaji wafungwa leo mtakaojifunga wenyewe kwenye mapenzi Yake, kwenye Neno Lake.

Hicho ndicho alichokuwa Paulo. Haidhuru alikuwa amejifunza kiakili kiasi gani, yeye alikuwa anamjua Mungu kwa ufunuo. Naam, bwana. Kutumia akili hakukuhitajiwa tena wakati huo, wakati ufunuo ulipokuja; ambao, juu ya ule mwamba Kanisa linajengwa. Naam, bwana. Angalia, yeye alikuwa Mbegu iliyochaguliwa kimbele.

Roho Mtakatifu pekee, anaonyesha Yeye ni nani. Hakuna mtu, watakufanyizia "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," na kila kitu kingine kutoka katika hilo. Unaona? Ila Roho Mtakatifu atamfunua Yeye kama Bwana Mungu wa Mbinguni aliyedhihirishwa, hilo ndilo hilo, lo, Yeye!

171 Sasa tazama. Sio manabii, sio wafalme, sio chochote kingine; ila hapa kwa mara ya kwanza, Mungu alifunuliwa katika Kristo, katika utimilifu wa Uungu kimwili, katika mwili wa kibinadamu. Huo ndio ufunuo. Lo jamani! Nakwenda kuwaimbia aya sasa.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka

(wanafanya hivyo?)

Ishara ambazo manabii walitabiri Kanisa la Mataifa katika dhehebu, siku zao zimehesabiwa, Zimejawa na vitisho. "Rudini, enyi mliotawanyika, makwenu."

Ninyi mnaoondolewa kwa nguvu toka kwao

Siku ya ukombozi imekaribia

Mioyo ya wanadamu inazimia kwa hofu;

Mizaha yao yote ya Hollywood hailifuniki. Kama mvulana mdogo akipiga mluzi, akitembea kando ya makaburi usiku. Unaona?

Mjazwe na Roho, taa zenu zikiwa zimetengenezwa na zikiwa angavu.

Tazameni juu, ukombozi wenu umekaribia!

Manabii wa uwongo wanadanganya, Wanalikana Neno la Mungu.

Kwamba Yesu aliye Kristo ndiye Mungu wetu;

(hiyo ni sahihi).

Hiki kizazi kinasukumia mbali ufunuo wa Mungu, Bali tunatembea ambapo mitume wamekanyaga.

Siku ya ukombozi imekaribia,

Mioyo ya wanadamu inazimia kwa hofu;

Mjazwe na Roho taa zenu zikiwa zimeengenezwa na zikiwa angavu Tazameni juu, ukombozi wenu umekaribia!

172 Pata ufunuo, ndugu. Hiki kizazi kinatupilia mbali ufunuo wa Mungu! Unaona? Manabii wa uwongo wanafanya hilo. "Kwa matunda yao mtawatambua." Wamechanganya mbegu chotara. Wamezaliwa katika shirika la dini badala ya Neno la Mungu, ufunuo wa Mungu akijifunua Mwenyewe kwa njia ya Kristo, Ambaye ni Neno. Lo, jamani.

173 Tungeweza kusimama hapa, lakini ikiwa .... tukipata nafasi tena nitakaporudi, kama mkitaka. Sasa kuna ... Mnataka kuendelea? [Kusanyiko, "Amina."-Mh.] Hilo ni juu yenu, ikiwa mnataka, unaona. Kidogo tu ... Nitaharakisha hiyo, lakini nichukue muda wa kutosha ili muweze... mnao wakati wa kupumzika, baada ya hili. Vema.. Ile ile, angalia, ile Mbegu iliyochaguliwa kimbele!

174 Roho Mtakatifu pekee, anakuonyesha Yeye ni Nani; hakuna manabii au wafalme wake. Na hapa Mungu amedhihirishwa katika mwili. Hapa kuna utimilifu. Yeye anafunuliwa kikamilifu kujulishwa kwa ulimwengu. Lo jamani

Angalia juu ya Mlima wa Ugeukaji, wakati ushuhuda wa Mungu Mwenyewe, "Huyu ni Mwanangu mpendwa. Msikieni Yeye!" Musa alisimama pale akiwakilisha torati, Eliya alisimama akiwakilisha manabii. Lakini Yeye ... Waliondoka, na Yeye akasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa. Msikieni Yeye!" Kulikuwa na watatu waliowakilishwa pale; torati manabii, na Mu-,,, na Kristo. Naye akasema. "Huyu Ndiye" Mungu kamili; hakudhihirishwa katika manabii, hakudhihirishwa na torati ila alidhihirishwa katika Kristo, Yeye ndiye.

175 Kristo ana rehema. Torati inakuweka jela, lakini haiwezi kukutoa huko. Manabii ni mamlaka ya kisheria ya Mungu, kukuhukumu na kukuua kwa ajili ya hilo Hiloni sahihi. Lakini Yesu alikuwa pendo la Mungu na ufunuo, kuifahamisha, ile Mbegu iliyochaguliwa tangu asili kuwa Yeye amekuita.

"Huyu ndiye. Msikieni Yeye".

Fahamu! Utimilifu wa Uungu umefahamika. Hii siri ya fumbo imefunuliwa sasa kuwa Mungu anadhihirishwa. Mungu na mwanadamu wanakuwa mmoja, kuwa mtu aliyepakwa mafuta, Kristo! Kristo inamaanisha nini? "Mpakwa mafuta, yule aliyepakwa mafuta kwa Utimilifu wa Uungu kimwili. Lo, jamani! Watu watalitiaje shaka?

176 Wakati mmoja, kwa sehemu Musa alikuwa Naye; kwa sehemu, Daudi alikuwa Naye; Lo, jamani, lakini hapa Yeye anadhihirishwa katika utimilifu, Mungu Mwenyewe akisimama duniani. Mungu, katika utimilifu afe kwa ajili ya dhambi za watu, ili aweze kuletea Kanisa Lake Uzima uliotakaswa; kwamba aweze kuwa na utangulizi, katika utimilifu, katika Kanisa Lake, kudhihirisha kila ahadi katika siku hizi za mwisho, alizoahidi kwa ajili ya siku za mwisho. Unaona? Ilikuwa nini....

177 Sikilizeni sasa. Mnasikiliza? Sasa jibane kidogo mwenyewe sasa. Unaona? Tazama.

Yesu alidhihirishwa kwa ajili ya nini? Kumwonyesha Mungu. Yeye alikuwa Mungu. Ilipasa awe; hakuna mwanadamu angeweza kufa, hakuna nabii angeweza kufa. Yeye alikuwa Mungu. Alikuwa Mungu wa manabii. Yeye alikuwa manabii. Alikuwa wafalme. Alikuwa Ndiye historia. Alikuwa yule ambaye angekuja. Yeye aliyekuwako, Yeye aliyeko, na Yeye atakayekuwako katika siku hii; yule jana, leo, na hata milele. Yeye alidhihirishwa kusudi hilo.

Na kwa ajili ya kusudi hilo alifanikisha Kanisa, ili Yeye, utimilifu wa Mungu, aweze kutimiliza kila Neno la Mungu lililoahidiwa katika hizi siku za mwisho; Yeye atakapopata utangulizi utangulizi katika Kanisa, ile nafasi, mahali pake katika Kanisa. Yesu alisema, "Aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo naye pia atazifanya hata nyingi kuliko hizi atazifanya kwani nakwenda kwa Baba Yangu" Unaona, hilo lilikuwa kusudi Lake. Udhihirisho ulikuwa pale. Na sasa, leo, Yeye anataka kupata mtu ambaye anaweza kuona hivyo ili waliachie lile Neno..

178 Unaona, Yesu aliliona hivyo alizaliwa kikamilifu mno kwa ajili ya siku ile, hata Mungu akadhihirisha kila tendo Yeye alilolifanya. Alikuwa ufunuo wa Mungu; Mungu aliyedhihirishwa.

179 Sasa alitakasa, kwa Roho Wake na Damu, Kanisa ambalo angefanya kila ahadi katika siku hii ya mwisho ifunuliwe. Sasa, unaona, Yeye angeweza kurejea nyuma na kifichua yale ambayo hawa watendaji wengine waliyaachia bila kuyaona hapa katika siku za mwisho, na kwa Roho Mtakatifu amefunua siri yote ya Mihuri Saba. unaona, Yeye anajidhihirisha Mwenyewe. Hilo ndilo kusudi Lake. Hiyo ndiyo sababu akafa. Huo ndio mkunjo wa pili wa kusudi lake lenye awamu tatu. Kwanza, kujidhihirisha Mwenyewe katika Kristo, kisha kujidhihirisha Mwenyewe kwa Kanisa. Na jambo lile lile, Kristo alikuwa Neno, na Kanisa linakuwa Neno linaporuhusu Neno lipite ndani yao.

Lakini wanapopokea dhehebu chotara, Neno litapitaje katika hilo? linakwama, ndipo husababisha hitilafu ya umeme na kukata fyuzi ya kudhibiti moyo. Unaona?

Lalini wakati umeme unatiririka bila kuzuiwa, lile Neno la Mungu linajidhihirisha Lenyewe. "Kazi nizifanyazo Mimi nanyi pia mtazifanya." Na katika siku za mwisho hilo litatokea. Angalieni nitawapelekea Eliya nabii, naye ataigeuza mioyo ya-ya watoto irejee kwenye Imani ya baba zao."

180 Na pale, kungekuwa na wakati ungekuja wakati Yeye angejidhihirisha Mwenyewe katika utimilifu wa Uungu Wake, Uungu kwa kupitia Kanisa Lake kuwa na utangulizi katika hili Kanisa. Lo jamani! Nini? Mtu aliyepakwa mafuta; sasa watu waliopakwa mafuta; lo, jamani, kumrejesha Bibi arusi na Bwana arusi waliopakwa mafuta. Wamepakwa mafuta kwa (kwa nini?) kukubali kile Hawa na Adamu walichokataa; kurejea pamoja na upako wa Neno, kwa sababu Yeye alisema, "Neno Langu ni Roho." Unaona, aliyepakwa mafuta na Neno. Kile Hawa alichokataa, Yeye anarudi na tunakikubali. 381 Angalia jinsi ile hali ya chotara tena, kile tu alichofanya Hawa

Yeye alimwambia Hawa, "Usifanye hili, usifanye lile,na unaweza kufanya hili, na lile:

181 Na Shetani akasema, "Lo! Unajua..." Lakini aligeuka na kumsikiliza.

Lakini Hawa wa siku za mwisho hatakwenda kulifanya, kwa sababu yeye alichaguliwa tangu asili kutokulifnya, Naam, bwana. Mungu anakwenda kulitenda. Yeye anajua. atakuwa nalo. Yeye alisema Lake waa-.." Kanisa lingekuwa pale bila ila wala kunyanzi." Linakwenda kusimama pale katika ufahari Wake, Neno Lake lililodhihirishwa.

Yeye atakuwa ishara kwa ulimwengu. Yeye atakuwa ... Atakuwa kitu fulani kwa ulimwengu ambacho ulimwengu utatazama na kusema, vema, ulimwengu uliobakia useme, "Aha, yeye ni mtakatifu anayejiviringisha. Yeye ni binamu wa pili Yeye si kundi letu." Najua hilo. Hilo ni jambo jema, unaona. Yeye, yeye ni wa Kundi hili juu hapa.

182 Mtu mmoja aliniambia siku ile nyingine, tukiwa tumesimama tukiongea, akasema, "Vema, wewe ni wa dhehebu gani?"

Nikasema, "Si lolote,"

"Nini?"

"Si lolote." Nikasema, "Mimi ni wa Ufalme."

"Vema, unajiungaje nao?"

Hujiungi nao. Unazaliwa ndani yake." Aha-aha.

"Huo ni Ufalme gani?"

Nikasema, "Mwili wa siri wa Yesu Kristo."

Kwa Roho mmoja tunabatizwa katika huu mwili" kuzaliwa kwa Roho Wake, ndipo tunakuwa na Ufalme. Na maisha yetu sio Waamerika, sis sio Wajerumani, sisi si chochote; sisi ni Wakristo. Tumetulia na kutembea katika Roho, mtumwa wa upendo, kutoka kwenye mambo ya ulimwengu. Na haki zetu za ulimwengu tumeziuza na kununua hii Lulu ya Thamani Kuu, na kutembea na kumwacha Roho Mtakatifu ajidhihirishe Mwenyewe. Hicho ndicho kanisa Lake halisi lilicho, au kile nilicho, kama tutajiachia mwenyewe kwenda na kumtumikia Mungu, na kwa Neno Lake, na sio kwa kile kanuni ya imani fulani inachosema.

183 Angalia, Mtu aliyepakwa mafuta, Kristo Mwenyewe hapa, Ee Mungu anafahamika. Lakini sasa.... Tazama! Lakini, ila sasa (kwa nini?) Yeye anao utangulizi. Mungu alidhihirishwa kikamilifu, katika Yesu Kristo, siri kuu ya Mungu ya ufunuo Wake.

Hii Nuru kuu ya ufunuo siku zote imepofusha hekima ya ulimwengu huu.

Katika siku za Yesu Kristo, wakati alipokuwa duniani, wa - waliwapofusha macho. Walisema, "Kwa nini hata unajifanya mwenyewe kuwa Mungu! Unajifanya mwenyewe kuwa sawa na Mungu!" Hakuwa tu sawa na Mungu; Yeye alikuwa Mwenyewe Mungu. Unaona? Unaona, hawalipati. Na hata hivyo baadhi yenu mnaweza....

184 Niliwasikia makafiri wakati mmoja waliniambia kuwa Yesu hakuwahi kamwe kusema Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Hakika alisema. hakika alisema. Huijui tu Biblia yako. Alimwambia nini yule mwanamke pale kisimani? Unaona? Alimwambia nini?

"Najua ya kuwa yuaja Masihi. Naye atakapokuja, atafanya haya mambo."Akasema, Mimi ninayesema nawe, Ndiye. Na pia kwa Paulo, na wengine mbalimbali. Angalia. Ila sasa Kanisa lina utangulizi.

185 Siri kuu ya Mungu wakati wote imepofusha macho hekima ya ulimwengu. Hawawezi kupata. Hawaielewi tu. Shetani haielewi. Hakuna wengineo wowote wanaoilewa, ila wale tu waliochaguliwa kimbele kuilewa, jinsi Mungu na Kristo walivyo mmoja. Watamfanya watatu kila wakati. Unaona? Hakika watafanya.

186 Angalia, linalofuata, la pili, Kristo aliyedhihirishwa ndani yako, tumaini la utukufu. Yule Mungu Mkuu aliyedhihirishwa katika Kristo, sasa Kristo aliyedhihirishwa ndani yako.

Tutaharakisha

Tazama ile iliyokuwa wakati mmoja siri kuu ya Mungu, siri ya fumbo kuu katika nia Yake, sasa inawekwa katika mioyo ya waamini yaani, Mwili wa Kristo. Ile iliyokuwa wakati mmoja siri kuu ya Mungu katika nia Yake, kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu, sasa imedhihirishwa. Lifikirie hilo! unaona? Lo, Nina....

Nina hakika hatuli-hatulipati hilo. Vema, si-siwezi kuliona jinsi inipasavyo kuliona, na-nami nina hakika hamlipati. Unaona?

187 Lakini fumbo kuu la Mungu, lile Mungu wa Milele alilokuwa nalo kama fumbo, limekunjuliwa katika Yesu Kristo, na kutolewa moja kwa moja kwa Kanisa Lake. Kile kilichokuwa wakati mmoja katika nia ya Mungu sasa kiko katika Mwili wa Kristo. Yesu akifanya mapenzi kwa Kanisa, Bibi arusi Wake, akimnong'oneza Yeye siri.

Unajua jinsi unavyomwambia mke wako mambo, unajua, yule msichana mdogo unayekwenda kumuoa. Unampenda sana, unamweleza tu siri, na unamweka karibu nawe, na kukupenda na kila kitu. Unajua jinsi ilivyo.

188 Hilo ndilo Mungu, Kristo, anafanya kwa Kanisa. Unaona? Yeye anamfanya ajue siri, siri tu. Sio hawa wafanyao mapenzi bila ya kuwa mume na mke; mimi namaanisha Mke Wake. Unaona? Vema. Sasa angalia. Hapa. Kwa kufanya ufunuo wa siri Zake ujulikane kwao, kwa neema Yake! Neema ya Mungu kwa jinsi gani? Watu, nalijua ... Natumaini huwazii kuwa jambo hili limeelekezwa mahsusi kwa mtu fulani, kikundi fulani cha watu, au hiki, kile; isipokuwa ni siri ambayo Mungu anashirikisha Kanisa zima kama tu wataipokea. Unaona? Haimaanishi mimi tu au wewe tu. Inamaanisha Kanisa, lile Yeye-Yeye analojaribu kuingia ndani yake.

Nawe unasema, "Vema, kwa nini hawaipokei? "Hawawezi kuipokea. Yeye Alisema, tena, alisema haya mambo. "Na wangewezaje?"?" Kwa sababu Isaya alisema hawawezi kuona hilo. Unaona? Na siku zote Yeye amesema...

189 Nabii Paulo alisema, "Katika siku za mwisho watu watakuwa wakali, wenye kujisifu, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wanaowadharau wale walio wema, wakali, wenye kujisifu, unaona; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake; hao nao ujiepushe nao. Kwani hao ni wale waendao nyumba hadi nyumba, na kuwachukua mateka wanawake wajinga, waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi." na kaptula, na nywele zilizokatwa, na kila kitu. "Waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi, na kusema, 'Ni vyema. Lo, wale kule ni wendawazimu. Usiwa-... '" Unaona? "Wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa ile kweli. Na hawa watu waliipinga kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa," wawezao kuunda kanisa, na kuunda kikundi cha watu. Naam bwana.

"Lakini upumbavu wao utakuwa dhahiri," Yesu atakapochukua Bibi arusi Wake na kumweka pale, na kusema, Huyu ndiye Yeye" na Yeye anaondoka Naye. Hiyo ni sahihi. Na upumbavu wao utajulikana.

190 Angalia kwenye kuwa na ufunuo wa hii siri ikijulishwa kwao kwa neema Yake!. Tazama! Wakati huu ufunuo mkuu, siri iliyofunuliwa, inajulishwa kwako, basi unakataa mambo yote ya ulimwengu.

Sasa nitarejea nyuma mara moja tena. Ningeweza tu kulisema vile vile. Ninalielekea hilo. Kwa ajili ya kanda, na wale wanaokwenda mbali. Hizi kanda zinakwenda ulimwenguni kote. Unaona?

Ninyi wanawake mnaodai mnaye Roho Mtakatifu, na hamna ujasiri kuacha nywele zenu zikue; wakati Biblia inalilaani na kusema mwanamke ... mwanaume ana haki ya kumpa talaka ikiwa atafupisha nywele zake. Inakubalika mbele za Bwana kufanya hivyo. Biblia ilisema, ikiwa atakata nywele zake, yuaaibisha kichwa chake. Na ni kawaida; unajua tu, lile jambo la zamani la kawaida, kwa mwanamke hata kuomba akiwa na nywele zilizofupishwa.

Wamevaa kaptula, na hizi suruali na mambo ya namna hiyo! "Mwanamke yeyote atakaye" (lo, unasema ...) "anayevaa mavazi yampasayo mwanaume, ni machukizo mbele za Bwana," uchafu, kinyaa! kama chumba cha kuogea cha zamani kinachonuka mahali fulani. Unaona? Lo, jamani! Uchafu kwenye pua za Mungu! Na ndipo unajaribu

kuomba au kufanyia maombi kwa kitu kama kile? Mungu anakikataa na kukiondoa. Hiyo ni sahihi.

191 "Vema," unasema, "sasa subiri kidogo, Ndugu Branham, unazungumzia Agano la kale.

Yeye ni yule jana, leo na hata milele. Ni ufunuo mkamilifu wa Mungu. Ikiwa Mungu amesema lolote, kamwe hatalibadilisha. Siku zote analikuza, si kubadilisha. Torati ilikuzwa, sio kabadilishwa. Ilikuzwa!

'"Yeyote atakayezini atakuwa na hatia ya kifo, "lakini yeyote, sasa imekuzwa", amtazamaye mwanamke kwa kumtamani!" Hakuwahi kubadilisha ile amri. Aliikuza.

"Ikumbukeni siku ya sabato; itakaseni" siku moja katika juma; sasa Yeye aliikuza, kule "kupumzika" huja kutokana na kuwa na Roho wa Mungu. "Amri juu ya amri, na mstari juu ya mstari; hapa kidogo, na kule kidogo. Ushikilie sana kile kilicho chema. Kwani kwa midomo ya kigugumizi na lugha nyingine nitasema na hawa watu. Na hilo ndilo pumziko huko ni kuburudika toka kwenye Uwepo wa Bwana".

Na bado hawakuweza kusikika Hilo, na wakatikisa vichwa vyao na kuondoka kwa ajili ya madhehebu yao. Aha-aha. "Huku na kuburudika", unaona, kuikuza siku ya sabato; kwenu ninyi Wasabato, na kadhalika. Lo, jamani! Yeye habadilishi. Anaikuza. "Kuzimu kumefungua malango yake ili kuwapokea".

192 Sasa, unaweza kuona sasa, Ujumbe wa wakati wa mwisho, kwa nini unakataliwa. Unaweza kuona? [Kusanyiko linasema "Amina"-Mh.] Sasa, siyo dhehebu ila ufunuo wa siri Yake. Unaona, siyo dhehebu. Ule ufunuo! Mungu hafahamiki kwa dhehebu. Yeye anafahamika kwa ufunuo.

Tazama! Mungu katika Mwili Wake, Kristo; na Kristo katika Mwili wake, Bibi arusi. Lo-lo-lo, jamani! Mungu aliyedhihirishwa katika Kristo; Kristo aliyedhihirishwa katika Bibi arusi! Na kama Mungu alivyochukua toka katika mwili wa Adamu, yule mwanamke, naye akaanguka; basi Mungu ametoa mwilini mwa Kristo nyama yake Mwili wake, ambao ni Neno Lake, na anamtoa humo Bibi arusi ambaye hataanguka kwa dhehebu au kanuni za imani. Hapana, bwana. Lakini Bibi arusi anarejea akiwa na Neno safi la Mungu lisiloghoshiwa likidhihirishwa.

Natumaini kila mwanaume anayesikia hii kanda, na kila mwanamke, ataelewa hilo. Unaona?

Yeye ni Hawa wa pili, lakini Yeye havunji na-na kuharibu sketi Yake ya usafi na utakatifu, kwa Mume Wake. Yeye atakaa na Neno Lake bila kujali kinachosemwa na yeyote unayeweza kuwa na mifumo yote ya muungano wa makanisa unayotaka na ushirikishaji wote.

193 Nao wanakwenda kuleta mateso ya imani hivi punde, na kufunga makanisa yote. Unaona hilo. Na makanisa kama haya ambayo si dhehebu watayatumia kama ghala. Na ikiwa mtu yeyote anakwenda na kufanya maombi kwa mtu mwingne ambaye sio wa muungano wa madhehebu atapigwa risasi pale pale. Ni tayari. Yule mhudumu wa Kilutheri mkuu wa hilo alisema hivyo. Na liko hapa hapa unaweza kusoma hapa hapa kwenye gazeti lako. Hiyo ni sahihi.

Kile wanachosema hakileti tofauti yoyote, lile Kanisa litasimama kwa uaminifu katika hii Nuru. Lilishahakikisha tayari nyuma kule, na litafanya hivyo tena licha ya kukabiliwa na kila kitu. Ni Neno la Mungu. Na wao, muungano wa madhehebu na kila kingine, vitakuwa vimemalizika. Hilo litakuwa Pale bila waa wala kunyanzi. Hiyo ni sahihi. Hilo litasimama pale.

194 Angalia, Mungu alijidhihirisha Mwenyewe katika mwili Wake, Kristo. Sasa unaona hizo awamu tatu, jambo jema?

Kristo katika Mwili Wake, Kanisa, akithibitisha Neno Lake la ahadi, kama Mungu alivyofanya kwa njia ya Kristo.

Alisema, "Nani awezaye kunihukumia dhambi? Kama sizifanyi kazi za Baba, basi ni wapi ambapo mimi - wapi ambapo nimeshindwa? Sasa ninyi watu husema kuwa mtalifanya, ninyi dhehebu, sasa, nionyesheni Mimi. Naam,. Nionyesheni pale niliposhindwa kuwa Masihi. Nionyesheni niliposhindwa, kwenye ishara moja ambayo Mungu alisema Masihi angefanya, ambayo sijatimiza". Yeye alisema, Mnaona? Mungu katika Mwili Wake.

195 Sasa Kristo, "Kazi nizifanyazo Mimi nanyi pia mtazifanya;"Unaona, unaona Mungu yule yule . Unaona? Kazi nizifanyazo Mimi nanyi mtazifanya; zaidi ya hizo, kwani Nakwenda kwa Baba Yangu," Lile Kanisa pia litakuwa kwenye Nuru kwa kitambo kirefu kidogo, unaona, likithibitisha Neno Lake la ahadi. Kama Mungu alivyofanya ahadi Zake katika mwili wa Kristo, vivyo hivyo Kristo anafanya kazi Zake zile zile katika Mwili wa

Kristo, lile Kanisa, unaona, sasa anafanya siri Yake ifahamike kwa Mti wa Bibi arusi wake katika siku ya mwisho, akileta yale matunda yaliyokuwa katika ule Mti hapo mwanzo.

196 Tazama, mti unatoa tawi, Ulutheri. Lilifanya nini? Mti ulipoanza kukua hapo linakuja tunda pamoja nao. Kulitokea nini? Wanalifanya kuwa dhehebu. Kwa hiyo mkata matawi anakuja, Baba Mkulima, na kukata lile....? "Linakufa".

Unatokeza - U-Wesley, ulifanya vizuri kuja. Ulifanya nini? Lile tunda lilirudi moja kwa moja kwenye mti tena, kwa hiyo Yeye akakata ule mzabibu, ukafa.

Nionyeshe moja, kanisa moja ... Nataka kujua. Nina miaka thelathini na mitatu ya historia ya Kanisa. Nionyeshe wakati mmoja, ambapo kanisa lolote lililoundwa kuwa shirika la dini ambalo halikufa papo hapo. Nionyeshe sehemu moja walipoinuka tena, mbali ya kuongezeka kwa idadi na mambo mengine, sio uamsho. Unaona? Haliko. Hapana, bwana. Limekwisha lote.

197 Je, mkulima wake alifanya nini? Alikuja na kulikata. Unaona? Lilileta tunda la kidhehebu; malimao, kwenye mchungwa, kwa hiyo Yeye alilikatilia mbali, unaona. Akalileta na kuliweka.

Lakini moyo wa mti uko wapi? Pale pale katikati. Na ameyakatia chini yote, hadi juu kileleni..

Yeye ana mbegu chini hapa kwenye mzizi. Kama mti uliopandwa kandokando ya mito ya maji, yeye achukuaye sheria ya Mungu na upendo moyoni mwake. "Naye atakuwa kama mti". Zaburi 1, "Uliopandwa kandokando ya mito ya maji; wala majani yake hayatanyauka, uzaao matunda yake kwa majira yake." na hapa hili ni sahihi...

Ni wapi tunda huiva haraka zaidi? Sehemu ya kilele cha mti. Kwa nini? Mwanga uko juu yake. Amina! Hiyo ni sahihi. Na pale pale juu kileleni pa mti, katika hizi siku za mwisho, Yeye analeta Mti wa Bibi arusi.

198 Sasa kumbuka, Yeye ndiye ule Mti wa Uzima, kinyume na "uzao wa nyoka" unaona. Yeye ndiye ile Mbegu, "Uzao wa mwanamke," ule Mti wa Uzima bustanini. " Wasije wakatoa mikono yao wauvute huu Mti, wangeula huo Mti na kuishi milele." Naye ndiye Mti pekee ambao unaweza kuliwa, ambao unaweza kuishi milele. Neno lake ni Uzima. Na lile likiwa ndilo Neno basi, lile Neno la Mungu ambalo Hawa alilikataa katika Bustani ya Edeni; basi hapa yupo Kristo, aliye Neno, lililodhihirishwa.

Naye alipokuja duniani, alikuwa ule Mti wa Uzima. Unaamini hilo? [Kusanyiko, "Amina,"-Mh.] Na Rumi, walifanya nini? Ilimpasa akatiliwe chini. Na aliwekwa juu ya mti wa aibu, "amelaaniwa aangikwaye mtini, akawa laana kwa ajili ya jamii ya wanadamu.

Na sasa kupitia hilo, analeta Mti wa Bibi arusi, ambao utakuwa Mti wa Uzima uliorejeshwa Kwake, kama Mume na Mke katika Bustani ya Edeni (lo, atukuzwe Mungu), kwa Neno lile lile na Mungu yule yule aliyedhihirishwa katika Mume na Mke, kurudi kwa ule ule Mti wa Bibi arusi.

199 Angalia! Kufanya lifahamike! Jinsi gnai, jamani, kuna mengi tu hapa, tungeweza kuendelea tu. Angalia, mti wa Mwili wa Kristo Bustanini, Akifanya sasa- Akifanya fumbo Lake kufahamika kwa huu Mti wa Bibi arusi.

Tazama, aliyekombolewa na Kristo, Adamu wa pili! Mnaamini Yeye alikuwa Adamu wa pili? [Kusanyiko linasema "Amina,"-Mh.]. Anarudi nyumbani, Edeni, pamoja na mke Wake, aliyeanguka akiwa amekombolewa na kurudishwa nyumbani tena. Huyo ni Kristo, na Kanisa leo, akimrejesha Mke Wake. Unaona siri yenye awamu tatu sasa? ["Amina.] Mungu aliyedhihirishwa katika Kristo; akadhihirishwa katika Kanisa;; wote pamoja kumrudisha Adamu na Hawa wa asili tena, mwanaume na mwanamke, ambao ni mmoja, waliofanywa kutokana na Damu moja na Roho mmoja, na kila kitu.

200 Kanisa ni Damu ya Kristo, kwa Roho, kwa sababu U-Uhai uko katika Damu. Huo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu ambaye anatubatiza sisi katika Mwili Wake, anayetambua Mwili Wake, nyama Yake, Neno Lake pekee. [Ndugu Branham anaipigapiga pole pole

Biblia yake mara kadhaa-Mh.]

Dhehebu haliwezi, halijawahi kugusa hilo. Ni ufunuo. Bibi arusi anajua hilo. Hawa alijua hilo, lakini alianguka; ila huyu analijua, na hataanguka. Bibi arusi amepangiwa hivyo. Haleluya! Loo! Yeye amepangiwa asianguke. Yeye hawezi kushindwa. Alichaguliwa kimbele kwa hilo. "Amebarikiwa mtu yule ambaye Mungu hamhesabii dhambi." Ninyi wahudumu mnajua ninachokizungumzia, mkiwa dazeni kadhaa mmekaa hapa. Unaona? "Amebarikiwa mtu yule ambaye Mungu hamhesabii dhambi." Daudi.

201 Angalia amemkomboa arejee, pamoja Naye anakwenda Nyumbani kurejea kwenye Uzima wa Milele katika mwili wa kibinadamu, akila, akinywa, akiishi milele. Isaya alisema, "Wangejenga nyumba na kuishi humo, watapanda mizabibu na kula matunda. Hawatajenga na wengine waichukue." Watoto hawatachukua, ila watakuwa pale pamoja na watoto wao. Yeye atajenga na kukaa pale. Amina. "Hajengi na mwingine ale; anajenga na kula, mwenyewe." Amina! Ni kitu gani? Bibi arusi Wake akirudi pamoja Naye, aliyekombolewa na kurudi kwenye Adamu na Hawa wa asili tena, kwani kifo kimeachwa nyuma. Walitazama nyuma msalabani na kuona kuwa kifo kimekwishalipiwa.

Na sasa, kwa imani, tumefufuka pamoja Naye, tumekaa katika Ulimwengu wa Roho sasa hivi, tukitazama nyuma kile kilichotukomboa; tukisubiri Mume aje; twende Nyumbani pamoja na Yeye.

202 Kusudi la Mungu lenye awamu tatu lililodhihirishwa katika Adamu na Hawa, na kila nabii, na katika vipindi vyote na Yeye yule ajaye; Yeye aliyekuwako, Yeye aliyeko, nasi... Yeye yule ajaye. Ule udhihirisho wote, ufunuo wa Neno la Mungu, Adamu na Hawa wakirudi Nyumbani tena, waliokombolewa, Mungu akijiweka Mwenyewe afahamike.

203 Ataketi pale kwenye Kiti cha Enzi cha Daudi, hiyo ni sahihi, na atamiliki, atatawala mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Kutakuwa na m-mti kila upande. Na kila taifa litakaloingia huu uponyaji utakuwa kwa ajili yao. Haya majani yatakuwa kwa ajili ya uponyaji wa mataifa. Wafalme wataleta heshima zao ndani yake. Hakutakuweko na chochote chenye kunajisi, au kitu chochote kitakachoingia mle ndani. Nao Mlima Sayuni utakuwa na Nuru juu yake, mchana na usiku, na waliokombolewa watatembea katika hiyo Nuru. Lo, haleluya!

Kwa kufikiri, sio hadhithi ya kubuni, si wazo la kithiolojia. Ni ufunuo wa Yesu Kristo, kwa Neno Lake, linalotoa mwanga unaoshinda mingineyo limekuwa kweli katika vipindi vyote, na ni kweli katika kipindi hiki. Ni kweli hapa sasa, Ni kweli kwangu, ni kweli kwako, na kila mwanaume na mwanamke anayeushikilia ufunuo huu. Amina.

204 Na kuona Mungu Mwenyewe akifanya Yeye Mwenyewe kufahamika, na huku Yeye Mwenyewe akipita katika maisha akiunguruma, kwamba wewe ni mfungwa Kwake sasa. Wewe ni mfungwa wa upendo Wake. Ulimwengu unaweza kucheka, wakiwafanyia kebehi, wakisema, "Tokeni huko" Ungeweza kwenda, lakini wewe ni mfungwa. Unaona? Wanawake wengine wanaweza wakaenenda wakifuata machafu ya Hollywood, lakini si ninyi. Wewe ni mfungwa. Amina. Unaona, wewe ni mfungwa wa Kristo. Watu wengi wanaweza kuvuta sigara na kunywa pombe na kuishi maisha mabaya na kufanya mambo ya kitoto kama wanataka, na kujiita wenyewe kuwa ni Wakristo, mashemasi, na hata wahubiri, lakini sio wewe. Wewe ni mfungwa kwa Neno, Naam, bwana, Naam, bwana.

205 Akifanya siri Yake ijulikane kwa Mti wa Bibi arusi Wake; aliyekombolewa na Kristo, yule Adamu wa pili; akirudi nyumbani, akirejeshwa kwenye Eden ya asili, aliye huru mbali na kifo, ugonjwa, huzuni, aibu, akirejea na uzima wa milele.

Basi, sikiliza, watu wengi sana wana mawazo mapotovu. Ile -ile... Kuwageuzia watu kwenye Ukristo, na kwenye serikali yake, si wazo la Mungu kamwe. Unasema, "Tuliwaingiza watu kwenye Ukristo - Ukristo kwa njia ya serikali Yake". Siyo hivyo. "Vema, hawapaswi kunywa pombe. Hawapaswi kudanganya Unajua, Waislamu wanaweza kukushinda. Unawajua wapagani katika Afrika, wale watu weusi na wanazo sheria miongoni mwa makabila yao ambazo zinaweza kushinda chochote unachoweza kufanya katika Ukristo.

206 Mbona, nimekwenda kwa lile kabila la Shungai kule. Ikiwa msichana mdogo hajaolewa kufikia umri fulani, yampasa aondoke - atoke kwenye hilo kabila, aondoe rangi yake ya kikabila. Anakwenda mjini; anakuwa mfanyaji vibarua tu. Na ikiwa yeye... Kabla hajaolewa, yampasa ahakikishwe ubikira wake. Akikutwa na kosa la kufanya

uasherati na mwanaume fulani, ilimpasa kusema ni nani na wote wawili wanauawa pamoja. Aha-aha. Lo, wanaweza- wanaweza kushinda kile kinachoitwa....

Vipi kama mlifanya hilo katika wanaoitwa Wakristo? Asilimia tisini na tisa wangekufa kabla hakujapambazuka. Hiyo ni shahihi. Hiyo ni sahihi wanaume na wanawake. Unajua hilo ni sahihi.

"Nini?" Unasema, Vema, mimi ni msafi!"

207 "Yeyote amtazamaye mwanamke na kumtamani ameshazini naye tayari moyoni mwake." Sasa vipi kuhusu hilo? Vipi kuhusu wewe dada uliyejiweka mwenyewe kwa yule mtu namna ile? Wewe una hatia kama tu uliyetenda hilo. Unaona?

"Ee, ila ni vyema." Mchungaji anaogopa kusema hilo, kwa sababu kwa nini? Makao makuu ya dhehebu lake yatamtoa nje kama akienenda katika usahihi juu ya hilo. Wao ni mbegu chotara. Hawalipokei Neno. Neno lilisema hiyo ni kweli. Yesu alisema hiyo ni kweli, na yeye ndiye Kichwa.

208 Sasa angalia, Mungu akifanya Yeye Mwenyewe- kufahamika. Siyo, hatupaswi kuwaingiza watu kwenye Ukristo kwa njia ya serikali; ila kwa ufunuo, Kristo ndani yako, kama Mungu alivyokuwa ndani ya Kristo. Kama Mungu alivyokuwa ndani ya Kristo Kristo ndani yako! Wakati, kile Mungu alichofanya ndani ya Kristo, Kristo anafanya ndani yako! Zile ishara Mungu alizofanya ndani ya Kristo, Kristo anafanya ndani yako! Lo, ni zuri namna gani? Lo! Lo, jamani Nalipenda hilo.

Yesu alisema, "Siku ile," yaani siku hii. "Siku ile," wakati huu ufunuo unapojulikana "mtajua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Ufunuo unapodhihirishwa. "Siku ile mtajua ya kuwa Mimi na Baba ni Mmoja. Mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani Yangu." Basi ufunuo unapokuja, basi ni, "Mimi ndani yako, na wewe ndani Yangu," Ndivyo hivyo. Unaona namna nyingi awamu tatu nam-... Kwa ajili gani? Kulirudisha. Yapasa tuwe hivyo.

Kama Kristo alivyokuwa Neno la Mungu. Yeye alithibitisha hilo, ikiwa Yeyeikiwa Yeye hakuwa Neno

Asingekuwa amedhihirisha Neno, Yeye angelikwisha kuwa mwanatheologia fulani mkuu.

209 Hivyo asingelikwishakuwa yule Masihi halisi ambaye ulimwengu ulikuwa unamtazamia. Unaona? Naam, bwana, huyo hangekuwa Yeye.

Hicho ndicho wanachokitafuta leo fulani - fulani mtu fulani anayeweza kumzidi Billy Graham, au mtu fulani anayeweza kujifunika na shirika lao la dini, akainuka na kuwaonyesha Wabaptisti kuwa hawajui walikosimama. Hakika. Wanatafuta hilo. Lakini Kanisa linatafuta unyenyekevu na ishara za Mungu aliye hai, Kristo. Unaona?

210 Yesu hakuwa mwanathiolojia mkuu. Alikuwa mkulima wa kawaida, aliitwa mwana wa seremala. Unaona? Yeye alitembea, lakini Mungu... Alisema "Baadhi yenu wanionyeshe kile Biblia inasema kuwa nitafanya ambacho sijakidhihirisha."

Kwa hiyo Kanisa linaweza kufanya jambo lile lile leo. Kile alichofanya Kristo ndicho Kanisa linafanya sasa. "Siku ile mtajua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, na ninyi ndani Yangu." Naam? Unakwenda pale, ukitembea kwenda Sayuni, kwenda (wapi?) kwenye Ufalme! "Siku ile mtajua kuwa Mimi ni ndani yenu".

211 Na tazama hapa! Ni jema hapa. Sitaki ulikose hili. Sasa kila mtu, na ninyi watu mnaosikiliza kanda, nje huko msituni na popote utakakolisikia, sasa sikiliza.

Yesu alisema, "Na kama Baba alivyonituma, nami nawatuma ninyi". Unaona? Sasa tazama. Yule Baba aliyemtuma Yeye alikwenda ndani Yake, kujithibitisha Mwenyewe kwa usahihi kwani Yeye alikuwa Neno. Na Yesu yule yule anayekutuma anakwenda pamoja nawe tena ndani yako, kumdhihirisha Mungu yule yule. "Kama Baba alivyonituma Mimi, Nami naishi kwa njia ya Baba; hivyo nawatuma ninyi, nanyi mtaishi kwa njia ya Mimi". Yeye ni nini? Yeye ni Neno. Unaishi kwa Neno. Lo, jinsi gani ningependa kuandaa somo juu ya hilo, na kuhubiri sasa kwa masaa kadhaa juu yake, unaona, juu ya hilo, jinsi tunavyojua ya hilo. Angalia, "Naye Baba aliyenituma Mimi", alikwenda pamoja Naye, yule Baba anayetuma.

212 Yule Yesu, anayetutuma, anakwenda ndani. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu

haunioni tena; bali ninyi mnaniona, kwani Mimi," kiwakilishi binafsi, "Mimi," Mtu, Yesu, "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu mpaka mwisho wa ulimwengu. Kazi nizifanyazo Mimi nanyi mtazifanya." Sasa rudi nyuma ukaone Yeye alichofanya, basi uangalie wewe unachokifanya ndipo ujilinganishe mwenyewe.

213 Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu. Na kama siku za Lutu," wakati Billy Graham wa kisasa Oral Roberts waliposhuka Sodoma na kuhubiri kwa Wasodoma, na kuwapofusha macho yao, unaona, kwa Injili. Malaika mmoja alibaki nyuma, Mjumbe pamoja na Abraham na Kundi Teule, na Yeye alifanya ishara gani? Unaona? Naye Abraham alimwita nani? Elohim, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Yesu akionyesha kuwa Yeye Mwenyewe, Mungu ndani Yake, atadhihirishwa ndani ya Bibi arusi Wake katika siku za mwisho! Lo, jamani, jamani! Hakuna tu mwisho wa hilo ni ufunuo wa Mungu tu! Ni ya Milele, ukiendelea na kuendelea na kuendelea tu.

214 Angalia anamkomboa basi, Mmoja kama Adamu na Hawa wa kwanza, kabla dhambi haijawatenganisha katika kifo; sasa Kristo, Adamu wa pili, katika Uzima unamkomboa Bibi arusi Wake kutoka mautini; na sasa akiwa njiani kurudi Edeni ya asili, akimrejesha Bibi arusi Wake katika ushirika, akimrejea Mungu, kama Mume na Mke, katika Bustani ya Edeni, hakika, Kristo na Bibi arusi Wake.

215 Na Mungu siku ile, "Ufalme ukabidhiwe kwa Baba; Yeye aweze kuwa yote katika yote." "Wakati bado akinena nitasikia." Daudi, Kristo, Daudi akiwa anaketi penye Kiti cha Enzi, Mfalme wa jamaa yote ya wanadamu. "Na wakiwa bado wakiwaza nitajua kile wanachowazia. Kabla hawajasema nitawajibu. Mbwa mwitu na mwanakondoo watakula pamoja. Simba atakula majani kama fahali, na watakula pamoja na kulala chini. Hawataumiza wala kuangamiza katika Mlima Wangu mtakatifu wote," kurudi Edeni yenyewe kabisa tena kwa dhati kama iwezekanavyo.

Hilo ndilo kusudi lenye awamu tatu. Ee Mungu, tusaidie kujua hili! Tusaidie kulijua!

216 Sikiliza kwa karibu sasa tena tunapoendelea, tukirejea kwenye Edeni ya asili.

Basi tunapozaliwa Naye, tunajazwa Naye. Unaona, uzima wako, Uzima Wake u ndani yako. Basi yapasa matendo yetu yote yamtangaze Yeye.

Kama kuchukua-kuchukua uhai toka kwenye mti mmoja na kuuweka ndani ya mwingine. Chukua uhai toka kwenye mti wa mpea na kuuweka kwenye mti wa tofaa, utazaa mapea. Unabidi uzae hayo, kwa sababu utomvu, uhai ndani yake, mbegu ni mti wa mpea. Vema.

Tunalo Jina Lake Hilo ni sahihi? [Kusanyika linasema, Amina."-Mh.] Yatupasa kuchukua Jina Lake.

217 Na kumbuka, sisi sasa, kama Bibi arusi Wake tumetiwa mimba kwa Roho Wake. Lo, jamani. Kanisa, likizaa watoto, unaona, waliotiwa mimba kwa Roho Wake, kwa Jina Lake, wenye Jina Lake, wenye Uzima Wake, wakizaa ishara za Uzima wake, dhahiri pamoja na utangulizi, ushahidi wa ufufuo Wake; kuonyesha kuwa Yeye si mfu ila yu hai milele na milele. Huu ni uzima wa Milele, na uliothibitishwa, unathibitisha kwa ulimwengu kuwa tuko hai ndani Yake. Loo!.

218 Unajuaje, kwa sababu wewe ni mwanajumuiya wa kanisa? Kwa sababu Kristo anaishi kwa kupitia ndani yako, ukiwa umetiwa mno mimba kwa Roho Wake hata wewe-wewe ni mfungwa kwa chochote kile. Umefungiwa, lo, jamani, kwenye Injili, umefungiwa kwenye Neno, na watoto wote utakaoweza kuwazaa ni hivyo, kwa sababu wewe ni mfungwa.

Huwezi kufanya uzinzi, umetiwa mimba tayari. Utukufu! Yeye hawezi kushika Tumbo la uzazi la uzima limefungwa kwa kitu kingine chochote kisiingie. Wewe tayari ni Wake, kwa kuchaguliwa kimbele. Ile mbegu imekuwa na Uzima; hakuna ulimwengu utakaoingia. Lo! Lo, jinsi ambavyo tungependa kukaa tukiongea hili kwa kama saa moja! Nina hakika mnaelewa. Unaona? Kristo, na Yeye aliye Wake pekee, tayari, imemalizika. Ile Mbegu ilikuwa pale. Ile Mbegu ilikuwa tayari. Ilikuwa lini pale? "Kabla ulimwengu kuwekwa misingi ametuchagua kimbele kupata Uzima wa Milele." Na mara tu ule mtiririko uletao Uzima, ile Mbegu ikiwa imelala pale... Zile mbegu nyingine ambazo zingeingia tu, zisingeshika, zisingeweza tu. Ila ile Mbegu inapoingia inasitisha tumbo la uzazi haraka; mbegu nyingine zote zinatolewa nje, unaona, namna hiyo.

Nawe unakuwa mfungwa, uliyezingirwa, katika Kristo. Kristo ndani yako, Uzima Wake ukileta ushahidi Wake, ishara Zake. Lo, jamani, jamani, jamani! Tazama, akileta ishara Zake za Uzima kama ushahidi wa kufufuka Kwake, akihakikishia ulimwengu ule Uzima wa Milele, akithibitisha kwa ulimwengu kuwa tu hai ndani Yake. Na fikiri hilo, hai pamoja na Mungu, Mkombozi wetu. Aliyetuumba kwa kusudi lile lile, Kanisa, na Uzima Wake uwezao kuumba ukiwa ndani yetu.

Yaani, Musa angeweza kusema, kwa Neno la Mungu, "Na inzi zije," na inzi wakaja. Mungu anaweza kuumba inzi anaweza kuumba kindi. Unaona?

219 Kwa hiyo Yeye anaweza kufanya lolote alitakalo. Anaweza kuumba. Anaweza kufanya lolote. Yeye ni Mungu. Mungu yule yule, ule Uzima wenye kuumba, unaona, ule ulio ndani yako, unaweza.... Wewe ni mfungwa; huwezi kulinena mpaka Yeye ulisema ulinene. Lakini, uliponena, ni Neno la Mungu. Amelithibitisha kuwa hivyo. Kila kitu kingine ni sahihi, naye anajua, lile linaponenwa, inabidi liwe hivyo. Unaona?

Musa alichukua fimbo yake, na kusema, "Na kuwe na vyura," kwa sababu Mungu alisema "Na kuwe na vyura." Yeye alilitoa nje tu. Hiyo ni sahihi. Na vyura walikuwa katika kila kitu, kila mahali kulikuwa na vyura. Walitoka wapi? Hakuna ajuaye. Hawakuwa pale kabla . Lakini Muumbaji, Mungu, akitenda kupitia mtu, aliumba vitu, vitu vyenye uhai.

Mungu yule yule aliyeumba chura wa kwanza anaweza kuumba chura wa pili. Anaumba vyura wote. Lo, jamani! Unaona ninalomaanisha? Aliumba kindi wa kwanza, anaumba kindi wa pili, anaumba kindi yeyote; anaweza kuumba kindi pale ambapo hakuna kindi. Yeye anaweza kufanya lolote atakalo kufanya! Yeye ni Mungu! Uzima Wake! Lo, jamani!

Ninapoliwazia, linanifanya nitetemeke!! Aha-aha.

220 Lo, kuishi naye, kwenda nyumbani pamoja Naye, kuishi pamoja Naye! Kwenda Nyumbani pamoja Naye kuishi pamoja Naye milele tukiwa Uzima wa Milele.

Hii ni siri kuu ya Mungu ya upendo iliyodhihirishwa, kuwa Mungu na mwanadamu wanakuwa mmoja. Unaona? Jambo lote ni Mungu na mwanadamu, mmoja. Mungu na mwanadamu walikuwa mmoja, pale; na Mungu na mwanadamu ni mmoja, hapa. Unaona? Kujazwa na Roho Wake, Yeye kuwa na utangulizi. Hilo lilikuwa mafanikio ya Mungu, hilo ni kusudi la Mungu kufanya hilo: kuwa Yeye aweze kuwa ndani ya Kristo; na Kristo ndani yetu; na sote pamoja, mmoja. Roho Mtakatifu, Kitu kile kile kilichomfunulia Kristo, kinafunuliwa hapa; Nguvu ya Kiungu inayoumba. Lo, jamani!

221 Mungu yule yule ambaye angeweza-ambaye angeweza kusema hilo kwa Musa, "Na kuwe na vyura," yule yule Mmoja aliweza kusimama pale, "Na haya maji yageuke kuwa divai." Unaona? Amina. Hiyo ni sahihi? [Kusanyiko linasema, "Amina." -Mh.] Yeye ni Mungu yule yule, yule yule Mmoja.

Huwa tu habadiliki. Ni Mungu ndani ya mtu. Huo ndio udhihirisho wake. Hilo ndilo analofunua. Hilo ndilo analojaribu kufanya, na Neno Lake Mungu Mwenyewe likifunua huonyesha kwamba mtu hawezi kuumba; Mungu Ndiye Muumbaji. Na si mwanadamu tena; ni Mungu muumbaji, ndani ya mwanadamu, ambaye sasa ni Kanisa Lake. Amina!

222 Tunakwenda Nyumbani Mbinguni, tuishi naye milele. Mungu anadhihirisha upendo wa Milele kwa Kanisa.

Sikiliza, sikiliza kwa makini sasa. Nawataka msishindwe kupata hili. Hakuna kanisa lingine, hakika ishara nyingine, hakuna ushirika mwingine hakuna serikali nyingine, hakuna ushuhuda mwingine, hakuna kanuni za imani nyingine, hakuna dhehebu, linakubalika nje ya Hili. Mungu hakubali kingine chochote ila yule, Kristo ndani yako, tumaini la utukufu," kitu pekee ambacho Mungu anakitambua. Hakuna ushirika, hakuna kanisa, hakuna kanuni za imani, hakuna dhehebu, hakuna chochote, kila kitu kingine kimekufa. Ni vipande vinavyopasa kukatwa na kuondolewa, kupogolewa mbali kwenye jambo lenyewe, ili Kristo aweze kuishi akiwa na utangulizi ndani yako.

Siyo kurejea ya nyuma! Nina moja liko hapa, linalosema, "Ni "shirika langu la dini". Hilo linapaswa kukatiliwa mbali pia. "Nina fulani hapa. Huyu anasema hili. Mama yangu ataniambia mimi ni mtakatifu anayejiviringisha. " Hilo linapaswa kukatiliwa mbali vile vile. Unaona? "Vema, najua mume wangu anataka nivae hizi kaptula" Hilo linapaswa kukataliwa mbali pia.

Unaona? Linapaswa kukataliwa na kupogolewa mpaka kuwe na wewe na Kristo tu pekee. Unaona.

223 Fikiri! Kwa njia ya Uwepo ulio hai wa Kristo aliye Hai kwa Neno lililo hai; lo, Kristo aliye hai. Uwepo hai, Neno hai! Tazama! Kwa udhihirisho Wake Mwenyewe binafsi, binafsi unathibitisha Kanisa lake.

Si washirika wa kanisa! Hakuwahi kulifanya kamwe katika siku za Musa, Hakuwahi kulifanya katika siku za yeyote mwingine mwishoni mwa ulimwengu, inapokuja mahali ambapo ingekuwa maangamizi. Siku za Lutu, haikuwa kuwa mshirika. Ilikuwa uthibitisho wa binafsi, Mungu katika mwili, unaona, uthibitisho wa binafsi.

224 Kumbuka! Liwazie, kuwa, watu waliozaliwa kwa Roho Wake, katika siku kama hii, katika kipindi hiki kikuu cha udhehebu tunachoishi, na Mungu aliye hai anachukua Neno Lake hai na-na kulithibitisha, kibinafsi, huu Uzima ulioko katika Neno, kiini kilichoko ndani ya Mbegu! Na Neno ni Mbegu ambayo mpanzi alikwenda kupanda. Na Uzima ni Kristo, katika Neno, kibinafsi ndani yako: akithibitisha jambo fulani ambalo huwezi kufanya, akihakikisha Mwenyewe kuwa si wewe, ila ni Yeye. Na mmekuwa mmoja, m-n-mtumwa wa upendo Kwake, kuwa Bibi Arusi.

225 Ashukuriwe Mungu aliye hai aliyeumba mbingu na nchi na yote yaliyomo ndani yake. Si ajabu, "Yeye ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Yeye aliyekuweko, Yeye aliyeko na atakayekuweko. Shina, na Mzao wa Daudi; Nyota ya Asubuhi ing'aayo" Yeye ni yote katika yote.

226 Uwepo Wake, kwa kila mmoja mmoja pamoja na uthibitisho binafsi Wake Mwenyewe akijidhihirisha Mwenyewe, lile Neno hai lililoahidiwa kwa siku hii, likijidhihirisha Lenyewe kwa kupitia kwako, uthibitisho wa ufunuo mkuu wa Mungu. Tazama, huja katika mtu mmoja pekee, kamwe sio katika kikundi! Mtu mmoja; si katika kikundi! Utambulisho wake ni kwa mtu mmoja mmoja. Unaelewa hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina"-Mh.] Sio kwa Methodisti, sio kwa Baptisti, si Presbiteri, sio Lutherani, si Wapentekoste, ila kama mtu mmoja mmoja!

Nitamtwaa mmoja, na kumwacha mmoja; Mimi nitawatenganisha." Hiyo ni sahihi. " Kutakuwa na wawili kondeni nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja. Watu wawili watakuwa katika kitanda kimoja, na nitamtwaa mmoja na mmoja nitamwacha."

Si kikundi. Ni uthibitisho binafsi wa mtoto wa Mungu aliyetiwa mimba aliyejazwa kwa Roho Mtakatifu, aliyejisalimisha mno kwa Mungu ambaye hajali kitu kingine chochote. Roho Mtakatifu akiishi Maisha Yake, kwa kupitia ndani yake akiunguruma akionyesha uthibitisho wa Neno, Lenyewe, likijidhihirisha Lenyewe kwa watu na kwa ulimwengu.

227 Ulimwengu unawezaje kupitia jambo kama hilo bila kuliona? Kama tu Wakatoliki walivyompitia Mtakatifu Patrick na hawakutambua mpaka baada ya yeye kufa. Jambo lile lile waliofanya kwa Mtakatifu Martin, hawakulitambua. Jambo lile lile wamelifanya katika vipindi vyote.

Jambo lile lile walifanya kwa Joan of Arc. Kanisa Katoliki lilimchoma moto, kama kwamba alikuwa mchawi, kwa sababu alikuwa wa kiroho. Karibu miaka mia na hamsini baadaye, walifukua miili ya wale makasisi na kuwatupa ndani, ili kufanyia kitubio.

228 Linapitia pale pale karibu nao na hawalitambui hata linapokuwa limekwishapita. Linanyakua tu ile Mbegu iliyochaguliwa kimbele ile Mungu aliyoichagua tangu asili kabla kuwekwa misingi ya dunia. Jambo lile lile likipita katika siku za Nuhu, jambo lile lile likipita katika siku za Musa, siku za Eliya, siku za manabii, siku za Yesu, kote mpaka saa hii hasa mtu aliyetiwa mimba mwenye Mbegu ya Mungu, lile Neno ndani pale likijidhihirisha Lenyewe, aliyejisalimisha sana chini ya mapenzi ya Mungu kwamba lile Neno, na lile Neno pekee, linajidhihirisha Lenyewe ndani ya huyu mtu, mfungwa, kwa mtu binafsi.

229 Si kusema, "Kanisa langu..." "Sasa Kanisa langu" halihusiki na hilo

Ni mtu binafsi, mtu mmoja! Kuzimu kote kuko kinyume na hili Fundisho, Kuzimu kote kuko kinyume na hii Kweli lakini ndiyo ile Kweli.

Yesu hakuwahi kamwe kusema, "Sasa Petro, wewe na Yohana, na watu wote mnao ufunuo, sasa kanisa lote limeokoka".

Ilikuwa kwake, kibinafsi. "Nakuambia wewe, wewe," Si kwa wao. "kwako, wewe

ndiwe Petro juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu.” Na neno “Petro”, lamaanisha “jiwe.” Jiwe lamaanisha “aliyekiri” au “aliyetenganishwa”.

Juu ya jiwe fulani, juu ya kitu fulani; unaona, aliyeitwa, Kanisa lililoitwa juu ya hili jiwe, juu ya huu “ufunuo” “Nyama na damu havikukufunulia hili. Ila juu ya ufunuo huu, kikundi kilichoitwa, nitalijenga Kanisa Langu ndani yao. Na malango yote ya kuzimu hayataweza kamwe kulihimili.

Hakuna hata unywele mmoja wa kichwa chako utakaopotea. Wewe ni Wangu! Nitakufufua siku ya mwisho, nimpe Uzima wa Milele, na kumfufufa siku za mwisho.“ Ndilo hilo, ule ufunuo. Si wao; ila ”yeye“, mtu mmoja binafsi! Si kikundi; mtu mmoja mmoja! Kuzimu kote kuko kinyume nalo.

230 Lakini siri Yake inafunuliwa tu kwa mpendwa Bibi arusi Wake. Huyo ndiye pekee angeweza kuona.

Akasema, “Isaya alinena juu yenu, ninyi nanyi wanafiki, ninyi nyoka katika majani. Mnatoka nje hapa na kusema, ”Lo, wale manabii wakuu watakatifu!“ ”Tumeyatia alama makaburi yao. Tunayang'arisha.“ Yeye alisema ”Ninyi ndio mliowaweka ndani mle. Je, Yeye alisema hilo?

Jambo lile lile Yeye angesema kwa makanisa ya Katoliki katika siku zao, walipotumia wale manabii wa zamani, Agano la Kale kabla hawajawa na Nikea, pale Rumi, na kuchagua. Wale manabii wa zamani walitoka kule wakila funza na vitu vya ardhini, bila hata kuvaa nguo, wakiwa wamejifunga ngozi ya kondoo, na wakajaribu kusimamia ile Kweli ya Biblia. Lakini Kanisa Katoliki walitaka wazo lao la kiakili. Ndipo wakatoa ... Akaja pale Mtakatifu

Ireaneus, Polycarp, Martin, na wengine wote. Nao walifanya nini? Waliwaweka kaburini, Joan of Arc, Mtakatifu Patrick na wengine, waliwekwa kule, sasa wanarudi na kung'arisha zile kuta kama walivyomfanya Joan of Arc. Walifanya nini? Waliwaweka ndani mle.

231 Basi nasema, Roho Wake anapokuita, “Kuta zilizopakwa chokaa! Ninyi wanafiki, mkijiita wenyewe kitu fulani, wakati mnachukua wazo la kiakili la mwanadamu, na kuliacha Neno liende. Badala ya kuja ukiwa umetiwa mimba ya Mbegu ya Mungu lile Neno ndani yako, umechukua kila mbegu chotara”. Si ajabu hilo kanisa linakaa kama kahaba mkuu kwa sababu “linafanya uzinzi wa kiroho, likifundisha watu mambo ya mwanadamu na si mambo ya Mungu.

Lakini alisema, “Msiogope, enyi kundi dogo, ni mapenzi mema ya Baba yenu kuwapa huo Ufalme.” Hiyo ni sahihi Hakika. Hapo tunalo hilo.

232 Biblia ilisema, katika Ufunuo, “Huu mji mkuu ulitawala wafalme wote wa nchi”. Ilisema alikuwa “kahaba mkuu” Ni nini hicho? Mwanamke anayedai kuwa mwanamke mwenye tabia nzuri na anafanya uzinzi. “Alikuwa na kikombe mkononi mwake,” cha kunywea na kupongezana na ulimwengu kwa kugongesha vikombe, vya.... kilichojawa na machukizo na machafu ya uasherati wake.“ Naye alikuwa na mabinti makanisa ya Kiprotestanti, ambayo kila moja linalotoka kwake linakuwa na mafundisho yale yale ya uwongo, mabatizo yale yale, na kwa kupeana mikono, badala ya ubatizo wa Roho Mtakatifu; na fundisho lao la uwongo la ”Baba, Mwana, Roho Mtakatifu“, na yote haya, badala ya kuchukua Jina la Bibi - Bwana arusi, na kadhalika.

Unasema, “Haileti tofauti yoyote.” Inaleta.

Ikiwa nitaweka jina langu kwenye hundi na kusema, “mchungaji,” kwa mhudumu na kadhalika, hiyo haitatoa pesa taslimu yoyote. Hiyo ni kweli. Inakataliwa kule benki. Aha-aha. Tazama. Vema.

233 Lakini siri hii yote inafunuliwa kama Yeye alivyoahidi kwa Bibi arusi Wake. Kuzimu kuko kinyume na ukweli huu, wa ufunuo wa siri hii. Lakini Bibi arusi anasimama juu yake. Huo ndio msimamo Wake.

Kanisa, kwa nini unasikia njaa. Kwa nini unaona kiu? Ni Baba akijaribu kukufunulia siri hii iliyofichwa. Lakini umeruhusu mambo mengi kuondoa hiyo njaa na kiu kutoka ndani yako. Umeruhusu kazi yako, umeruhusu mke wako, umemruhusu mume wako, umewaruhusu watoto wako, umeyaruhusu masumbufu ya ulimwengu, umemruhusu mchungaji fulani umemruhusu mtu fulani aiondoe kutoka kwako, hali akijua ndani moyoni mwako mna kiu, njaa. Ni Mungu anajaribu kukufunulia siri Yake (unaona?) ule

ufunuo. Siku ya mwisho imewadia. Tazama sasa.

234 Hebu na tutazame nyuma tena. Siwezi kuliruka lote hili. Unaona? Nataka tu utazame hapa kwa muda mfupi sasa, na tutafunga dakika chache zijazo. Mtakuwa ... Nipe tu usikivu wako wote kwa muda mfupi.

235 Tazama, Wakolosai, aya ya 18 hapa. Katika Kitabu cha Wakolosai aya ya 18.

Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu; ili ili kwamba-ili kwamba awe mtangulizi katika yote.

236 "Naye ndiye Kichwa cha mwili, yaani cha Kanisa, na Yeye anataka utangulizi." Sikiliza sasa, sikiliza kwa makini tunapoendelea. Nini? Yeye anakuwa Kichwa cha Mwili wa Bibi arusi Wake, uliotolewa Kwake; nyama na mifupa, kama katika Adamu, unaona, Bibi arusi.

"Mzaliwa kutoka kwa wafu," unaona, huyo ni, mzaliwa kutoka kwa wafu, dhambi ya kutokuamini.

Nini kilimwua Hawa? Kutokuamini. Ni sahihi hilo? Kutokuamini kwao katika nini? Kwa, kwa... kutokumwamini Mungu? Hapana. Alikuwa na imani katika Mungu. Hakika. Je, alisema, "Hakuna Mungu."? Hapana, bwana. Hakuwa kafiri. Alisema, "Vema," "unajua siliamini Neno Lake kabisa"? Ee, hapana. Aliamini lote kasoro jambo moja dogo. Unaona?

237 Sasa Biblia haikusema, katika Kitabu cha Ufunuo, Yesu alisema Mwenyewe, "Mimi-Mimi Yesu nimemtuma malaika Wangu kushuhudia mambo haya kwenu."? Mtu yeyote akiondoa Neno moja katika Hilo, au akiongeza neno moja kwa hilo" Na ikiwa hizi huzuni kubwa na masononeko yalipasa kuja kwa sababu mwanamke alitilia shaka Neno moja la Mungu, je, Yeye atakuachilia ukitilia shaka Neno moja? Yeye atakuwa dhalimu Ahaaha-. Unaona? Unaona, hiyo haitakuwa sahihi. Aliye hatiani...

Yuko hapa mtu mmoja amesimama, naye alisababisha hii huzuni kubwa yote kwa sababu ya kutilia shaka - neno moja; basi anaendelea na kupata ujuzi wa miaka mingi na kila kitu katika Biblia, na kadhalika, na hata wengine wamejitolea mhanga maisha yao kwa ajili ya hao, ndipo aseme, "Ah, unaweza kuendelea na kula hilo. Hiyo ni sawa. Nitakurejesha kwa vy ovyote vile. Ah. hapana. Mungu hana upendeleo. Lakini....? Unaona? Unaona? Mungu hana ubaguzi. Sasa tazama.

238 Sasa tazama. "Naye ndiye Kichwa cha Mwili" uliozaliwa kutoka katika dhambi, ya kutokuamini Neno la Mungu. Hilo linar..... hilo linahusisha kila dhehebu, kila kanuni ya imani, unaona. Kutokuamini Neno; ambalo ni Yeye Mwenyewe. Neno la Uzima. Unaona? Lile Neno, pekee, lina Uzima. Neno lingine lolote ni mbegu chotara. Hata kama litaonekana limefanana Nalo kiasi, lakini si Neno.

Neno huzaa Uzima Wake Lenyewe, ule ambao Hawa alibadilishana kwa kuuachia na kupokea maarifa binafsi. Unaona jinsi kanisa lilivyo leo, linaongozwa na ufahamu wa watu fulani?. Musa alikuwa na ufahamu mwingi wa Mungu mpaka akakutana na kichaka kilichokuwa kikiwaka moto, ndipo akaona kushindwa kwake mwenyewe. Kile kichaka kilichokuwa kinawaka moto kilikuwa na yale Musa aliyokuwa amepungukiwa. Neno lina kile ambacho dhehebu halina.

"Yeye, aliye Kichwa, Ndiye malimbuko ya ufufuo."

239 Tutaondoka hapa penye juu "ufunuo" kuendelea tu mbele zaidi kidogo, ikiwa mtasema hivyo. [Kusanyiko linasema,"Amina".-Mh.] Vema. Vema, sawa kidogo tu sasa.

"Yeye ni malimbuko ya ufufuo." Hiyo ni sahihi? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Tazama. Basi, Yeye ni nani? "Yeye ni kichwa cha Mwili, ambao ni Kanisa Lake, Bibi arusi." Aha-aha.

Basi, Mwili wa Bibi arusi lazima ufuate Kichwa, kwani huo ni sehemu ya ufufuo Wake na sehemu ya ile siri. Haiwezekani huo usiende, Lo, jamani! Ni sehemu ya siri ya Mungu, jinsi Mungu alivyojifunua mwenyewe hapa na kuufufua kwa Neno, ndivyo Yeye analifunua Kanisa Lake na kulifufua kwa Neno lile. Ni sehemu ya siri yake yenye mikunjo mitatu.

240 Kama Kichwa kilivyotolewa kaburini, hivyo Mwili lazima umfuate Yeye kurudi Edeni. Ambapo, Kichwa cha familia, Mwanaume, Bwana arusi; Bibi arusi akiwa ule Mwili wa Bwana arusi, Bibi arusi lazima amfuate kwa sababu hicho ndicho Kichwa. Na Kichwa

kimefunuliwa, na kurejea na Uzima wa Milele; na Mwili lazima ukifuate hicho, kwa sababu ni Mume na Mke tena.

Amina! Na ili mradi umetiwa mimba kwa Neno lile lile, ambalo ni Mwili Wake; umechukua Mwili Wake, unakuwa ndani Yake ulipochukua Neno. Si kanuni ya imani; lile Neno! Lo, jamani!

Je, hilo lisingefanya somo la kuendelea kwa ajili ya mchana huu? Aha? Jamani, hilo ni la ajabu! Unaona? Liwazie tu sasa, ni kitu gani.

Kwa hiyo, Mwili hauwezi kutambua ... Usikose hili. Kwa hiyo, Mwili hauwezi kutambua ukuu mwingine ila Neno. Kwani, Ki-Kichwa kimeunganika na Mwili, na Kichwa ni Neno, na ni Neno lile lile. Ukuu mmoja! Kwa hiyo, madhehebu, na baba watakatifu, na kila kitu, ni samadi isiyo na virutubisho. Kuna ukuu mmoja, nao ni Kristo. Ule Mwili unatambua jambo moja pekee, Neno!

241 Sasa nionyeshe mahali ambapo mtu alibatizwa katika Mwili katika jina la

"Baba, Mwana, Roho Mtakatifu"? Nawe unatambua nini? Unaona? Nafahamu nazungumza na maelfu, kwenye kanda, unajua, na tuna huduma y a kanda ulimwenguni kote. Wewe umebatizwa katika "jina gani? "Kwani hakuna jila lingine tumepewa chini ya Mbingu," Neno lilisema, "Ambalo mtu aweza kuokolewa kwalo". Ikiwa umebatizwa, kuonyesha kuamini kwako katika Kristo, halafu uchukue jina la kanuni ya imani, basi wewe ni mbegu chotara. Ikiwa hufanani kabisa na lile kanisa na fundisho lao....

242 Basi, ninyi Wakatoliki, unaona, mtakwendaje chini ya mamlaka ya papa sasa, mkisema kuwa yeye ni mrithi kufuatana na urithi wa papa unaoanzia kwa .... unaoanzia kwa Petro, wakati huyu papa na hili kanisa hufundisha kinyume mno na lile Neno la kwanza ambalo Mungu alilitambua kwa ishara na miujiza, kuwa ndilo Kanisa Lake? Na kuona Neno lile lile likiletwa leo katika usafi wote, likionyesha ufufuo ule ule Aliokuwa nao pale, Mungu akiishi miongoni mwa Watu wake, akifanya mambo yale yale, halafu uweze kukubali ukuu katika Rumi?

Ukuu wetu uko Mbinguni. Mimi siendi Rumi; Nakwenda Mbinguni nitakapokufa. Unaona? Unaona? Ukuu uko Mbinguni.

243 Na Mwili sharti ufuate Kichwa, kama mke anavyomfuata mume. Adamu akiwa hakudanganywa, aliambatana tu na Hawa. Hawa alidanganywa, yeye alikuwa kwenye uhalifu, au ufufuo wote wa Mwili wote ungetoka siku ile ya Bwana Yesu wakati Yeye alipotoka kaburini. Lakini ilimpasa Yeye amkomboe, ambaye ni Mwili Wake. Imempasa akombolewe ili aje Kwake, [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili-0Mh] Unaliona? [Kusanyiko linasema "Amina". -Mh.] Lo, jamani! Unaona, isingeliwezekana hilo litokee wakati ule. Ukombozi unaendelea.

244 Sasa mnaona Mihuri? Yeye alipokuwa kwenye kazi Yake ya Upatanishi nyuma kule, akikomboa, lakini siku fulani atakuja kuchukua hiki Kitabu ambacho Yeye amekikomboa . Na yote yaliyoko katika hiki Kitabu na lile Neno ni Yeye. Na wale wote waliomo katika hicho, Yeye anakuja kwa ajili ya hiki Kitabu cha Ukombozi ambao majina yao yameandikwa kwenye Kitabu.

Naye yupo hapa leo, katika Neno Lake, akidhihirisha jambo lile lile alilofanya pale. Hawezi kutambua ukuu mwingine. Hapana bwana, Hakuna askofu, hakuna chochote. Yeye anatambua Ukuu mmoja, nao ni Kristo, na Kristo ni Neno. Lo, jamani! Loo! Nalipenda hilo. Lo! Naam, bwana.

245 Kama kichwa kilivyochukuliwa toka kaburini, vivyo hivyo lazima Mwili wake umfuate Yeye hadi Edeni. Kwa hiyo, Mwili hauwezi kutambua ukuu mwingine, ila Ukuu wa Neno.

Hakuna dhehebu liwezalo kuweka chochote kwenye Hilo. Kwani iwapo mtu yeyote ataondoa Neno moja moja kwa hilo, ni kundoka toka kwa Hilo" Umekufa, umekuwa mbegu chotara papo hapo. Amerudi hapa, huu ushuhuda mikononi mwake, machafu ya uasherati wake, akifanya uasherati wa kiroho" kinyume na Neno lile lile analodai kuliamini. Unaona?

246 Hivyo basi ni Neno, au si chochote. Hiyo ni sahihi. Yeye, lile Neno! Unajuaje liko sahihi? Yeye, lile Neno, limethibitishwa. Mnaona? Yeye, lile Neno lililothibitishwa kikamilifu, ndilo Ukuu, Kichwa cha Kanisa. Yeye ni Neno, Ukuu, Yeye ametambulika kikamilifu, ametambuliwa, amethibitishwa kwaRoho Wake Mwenyewe, katika Kanisa Lenyewe, yule halisi.

Akijionyesha Mwenyewe, katika uthibitisho, ni ushahidi wa wazi kwa Mwili mzima. Basi wewe huhitaji kanuni za Imani. Madhehebu yamechakaa. Lakini Ukuu Wenyewe, ukitambulika katika Mwili kwa uthibitisho binafsi, unaona, akijithibitisha Mwenyewe unauhakikishia Mwili ule Ukuu. Basi,, tunaunganishwa chini ya Ukuu mmoja uliothibitishwa, ambao ni Kristo, Neno la Mungu, si chini ya kanisa lolote.

247 Basi, Ukuu wetu ni Ufalme. "Ufalme wa Mungu upo ndani yenu," ilisema Biblia, Yesu. Ufalme! Sisi si dhehebu. Sisi ni wa Ufalme, na Ufalme ni Neno la Mungu lililofanywa Roho na Uzima katika maisha yetu wenyewe, ikisababisha kila ahadi ya leo kutimia kama ilivyofanya katika siku ile Neno na Mungu walipokuwa mmoja. Na Neno la Mungu ni mmoja katika Kanisa Lake leo, akilifanya liwe ndio Ukuu wa Mwili ule uliokombolewa, kuleta Ujumbe katika siku ya mwisho; na kuchukuliwa kutoka kwa wafu, katika ufufuo kurudi na kurejesha tena, kama Adamu na Hawa, hapo mwanzo katika Bustani ya Edeni. Ile siri ya Mungu yenye hatua tatu, Mwili wake! lo, jamani! Angalia kwa makini sasa, kama katika mifano, Israeli wa zamani.

248 Je, Nachukua muda mwingi kupita kiasi juu yake? [Kusanyiko linasema, "Hapana". -Mh.] Msiniache, msiniache niende mno... Sasa sikiliza. Sasa tuna kama kurasa ishirini zaidi. Unaona? Unaona? Lakini sasa... Kidogo tu sasa,na ndipo- ndipo nitawaacha nyote muondoke mpaka wakati wa kiangazi kijacho, au wakati mwingine, ikiwa Bwana atapenda. Unaona?

249 Sasa tazama, angalia sasa tumeunganika pamoja chini ya Ukuu mmoja, katika namna inayofanana, mfano wa Israeli wa zamani. Sasa nyote mnalipata? Kama Israeli wa zamani; Mungu mmoja; aliyethibitishwa kwa Nguzo y a Moto na kujifunua Mwenyewe kwa njia ya nabii, kuwa Neno.

Mungu yule yule, ile ile Nguzo ya Moto, njia ile ile; Yeye hawezi kubadili njia Zake. Hiyo ni Kamilifu tu kama liwezavyo kuwa Sivyo? Unaona? [Kusanyiko linasema,"Amina." -Mh-]

250 Mungu mmoja! Israeli walikuwa na miungu wangapi? [Kusanyiko linasema, "Mmoja,"-Mh] Bibi arusi anao wangapi? ["Mmoja."] Daima kutakuwa na wangapi? ["Mmoja,] Kweli. Kweli.

Unaona chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, ambaye alikuwa Nguzo y a Moto katika siku za Musa, nabii mkuu. Aliongozwa na Nguzo ya Moto. Hivyo ni sahihi? [Kusanyiko linasema, "Amina"-Mh.] Vema. Akienda nchi ya ahadi.

251 Na katika kipindi cha Ukristo kulikuwa na Mungu Mmoja aliyeonekana katika umbo la Nguzo ya Moto, kwa nabii aliyeitwa Paulo, aliyetumwa kwa Mataifa, kutoa humo watu kwa ajili ya Jina Lake. Hilo ni sahihi. [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.]

Na katika siku za mwisho, ameshuka katika hali ile ile, akijithibitisha Mwenyewe, unaona, katika ishara ile ile, maajabu yale yale, Nguzo ya Moto ile ile, Neno lile lile, udhihirisho ule ule.

252 Mwili Wake utafanya zile kazi alizoahidi, kama katika Marko 16 na kadhalika. Mwili Wake haukushikiliwa kaburini, ila ulitambulika naye katika ufunuo. Je mnalipata hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh] Basi, Mwili wa watoto wake waaminio hautashikiliwa kaburini Yeye atakapokuja, ila utatambulika, pamoja Naye, kwa sababu Yeye alikufa kwa kusudi la kufufua Bibi arusi Wake, ule Mwili. Ametambuliwa, kwa sababu huo ni mwili Wake, kwa sababu huo ni Neno. Huo umejiachilia kabisa kutoka katika mambo ya kidhehebu, kuwa Kwake. Umetolewa kabisa kwenye mambo ya kidhehebu, na kujisalimisha kabisa Kwake, na Yeye ni Neno. Unaona? Na inatambulika Naye kwa sababu sasa tuna malimbuko ya ufufuo wetu kwa kujua kuwa tumepita toka mautini kwenda uzimani, kuwa wafungwa Wake. Naye Mungu akituhakikishia sisi kwa Ukuu Wake binafsi kuwa Yeye ni yule jana, leo na hata milele, kwa kufanya mambo yale yale kwa njia ya Kanisa yale ambayo Yeye aliyafanya wakati ule. "Yeye ndani yangu, nami ndani Yake, ndani yenu, unajua, na kadhalika. Hilo ni sahihi.

253 Mwili Wake haukushikiliwa kaburini. Ulitambulika Naye katika ufufuo ule ule kama Yeye alivyo sasa, sikiliza, hilo linamaanisha hivi: Neno Lake, ambalo ni Yeye, limeanza kufufuka. Lile Neno, lile kote katika kipindi cha Luther, Wesley, unaona, limeanza kuinuka hadi kufikia nguvu Yake; pale lilianza kutembea, baadaye likatembea zaidi kidogo, sasa linakuja juu kwenye utambulisho. Unaona? Tazama. Sasa, kwa Uzima ndani ya Mwili, ni uthibitisho wa Unyakuo kuwa uko karibu. Unapoona Ukuu na Mwili

ukifanyika kuwa Mmoja na utimilifu wa kipimo cha udhihirisho Wake, inaonyesha kuwa Mwili u karibu tayari kupokelewa na Ukuu.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka.

254 Unaona ninachomaanisha? Yeye ameanza kuupa Mwili Wake Uzima, (kwa nini?) Yule ambaye yeye amemkomboa. Kazi ya upatanishi imemalizika, Yeye analeta Uzima Wake kwenye Mwili, katika uthibitisho kwa ajili ya Unyakuo, Kumbuka, sasa, katika siku ya mwisho....

Mimi-mimi, ikiwa mtaniruhusu, nivumilieni tu kwa muda kidogo juu ya hili sasa, sasa, itakuwa vyema. Sitaki mlikose hili. Mimi-mimi, nami nina ... Yanipasa kuchukua hii kanda sasa, kwa vile nilianzia mbali hivi. Nataka kutoa tamko moja zaidi kuu ikiwa ningeliendelea kidogo juu yake.

255 Sasa, angalia. Sikiliza hili. Sasa ni jambo kuu. Sasa ndipo hapo tunapotaka kupatazama. Kumbuka, katika siku za mwisho, tutarudi nyuma na kuthibitisha ile siku ya kwanza: unaona, Adamu na Hawa, Mume na Mke bila dhambi, Uzima; ndipo anguko. Angalia, angalia kwa makini.

Mpotoshe. Aha-aha

Angalia kilichosababisha, Ibilisi! Ibilisi anatenda sasa kama alivyotenda wakati wa kwanza.

Kama tu ule ufalme wa Mataifa ulivyoletwa, pamoja na Mfalme Nebkadreza ulithibitisha jamii ya Mataifa kwa nabii ambaye aliweza kufasiri lugha zisizojulikana, maono, ndoto. Na umekuja chini katika mataifa, bila chochote, Wamedi na Waajemi tu, na chuma na kadhalika, na kwenye miguu unatokomea kwa njia ile ile tu, ufalme wa Mataifa.

256 Mtazame Ibilisi katika siku za mwisho, anatenda kama alivyotenda mwanzo. Ibilisi alifanya nini? Jambo la kwanza alilofanya Ibilisi kutenganisha ushirika wa Mungu na mwanadamu, alitaka kumjengea muungano wa Ufalme, wenye utukufu mkuu zaidi na kuonekana kwa nje kuwa wenye maarifa na elimu ya juu zaidi, ufalme mkuu zaidi kuliko aliokuwa nao Mikaeli, Kristo.

Mmelipata? [Kusanyiko, “Amina.”-Mh.] Sasa, sasa ikiwa umelikosa nyanyua mkono wako tu, nitalisema tena, unaona. Unaona.

Ibilisi, hapo mwanzo, kusudi lake moyoni lilikuwa kufanikisha jambo lenye kung'aa na kuu zaidi Mbinguni kuliko alilokuwa nalo Kristo, hiyo ni sahihi, linaloonekana kwa nje kuwa lenye maarifa na elimu ya juu zaidi lenye urembo zaidi, lenye utukufu zaidi, kuliko Ufalme wa Kristo. Unadhani tutakuwa na motokaa katika Utawala wa Miaka elfu, na eropleni? Unaona? Unaona kile anachofanya Ibilisi?

257 Sasa, madhehebu makubwa yaliyorembwa kiakili yanafanya jambo lile lile, yakijikusanya pamoja kufanya jambo lile lile. Unaona? Wanajikusanya na wakijiunda wenyewe kidhehebu kila moja likijaribu kulishinda lingine. Na sasa wamepata fahari mno, hawajui la kufanya ila kuliunganisha na kanisa Katoliki. Unaona? Ibilisi akijenga tena ufalme mkubwa zaidi, kusukuma nje wale watu wasioamini madhehebu; na hata kuchukua majengo ya makanisa yao na kuyafanya maghala na wachungaji wa jinsi hiyo hawana haki kabisa.

Na mtu yule ambaye ni mtu aliyetumwa na Mungu kamwe hangekaa katika dhehebu baada ya kusikia Hili au kuliona Hili ikiwa yeye-ikiwa amepata ya kutosha kumtoa nje na kulitazama. Hakika. Sisemi hilo kwa kukosoa; nasema hilo kwa kuwa mkweli, unaona, kuona hilo limefunuliwa.

258 Angalia, katika hizi siku za mwisho, Ibilisi anafanya jambo lile lile. Unaweza kuliona? [Kusanyiko linasema, “Amina.”-Mh.] Shetani alifanya jambo lile lile, akijenga kanisa chotara lililochanganya mbegu kutokana na washiriki machotara, chotara kwa njia ya maarifa badala ya Neno, kwa kuongozwa na mtu anayetumia akili tu badala ya mtu aliyezaliwa mara ya pili, wakijenga ufalme wa kiakili ambao utang'aa kuliko kundi dogo la Kristo. Unaona? Ni nini kilichofanya hilo? Malaika walioanguka.

Biblia inasema ilikuwa malaika walioanguka waliomsikiliza Ibilisi badala ya Kristo ambao hapo awali walikuwa Wake Kristo. Hiyo ni sahihi [Kusanyiko linasema, “Amina”-Mh.]

259 Sasa sikiliza kwa makini, "malaika walioanguka." Malaika wa jinsi gani? Luther, Wesley, Katoliki, Wapentekoste, ambao hapo awali hawakuweza kutunza makao yao ya kwanza kama Malaika walivyofanya, na wameangukia kuwa mashirika ya dini, kama ngome kuu ya Ibilisi kule Nikea. Nao wamefanya nini? Wametengeneza jumuiya kuu ya wahudumu wa makanisa, kufanya "alama ya Mnyama," kama Biblia ilivyosema. Na kujenga uchumi wa Kikristo ambao utafunga milango ya hili kanisa na mengine yanayofanana nalo. Unaomwona Ibilisi akiwa kazini kwake?

Najaribu kuwaletea ufunuo wenye hatua tatu, au siri ya Mungu.

260 Walifanya nini? Malaika walianguka wametekwa na fikira za hekima na elimu, kama Hawa alivyofanya. Wesley alikuwa mtu wa Mungu; lakini nini kilimfuata? Malaika walioanguka waliingia katika hilo. Kwanza hawa malaika walikuwa nini? Viumbe wa Mungu, lakini walianguka kwa ajili ya hekima ya Ibilisi, walianguka kwa ajili ya Ibilisi - hekima ya Ibilisi. Na unaona wanakuwa nini? Malaika walioanguka. Na mashirika ya dini , na watu wa Mungu waliokwenda kusimamisha kweli duniani; kabla ile Kweli kuweza kuendelea na kutangazwa na kufikia ufunuo halisi wa Kristo, malaika walioanguka wanaingia na kuichukua na kuunda madhehebu katika hilo. 553 Hiyo ndio sababu ufunuo wa siri ya Mihuri Saba ilipasa ikunjuliwe.

Sasa mnaliona hilo? Kile walichokiachia? Ikiwa Luther angeweza kuendelea ingekuwa hapa. Kama Wesley angeendelea, ikiwa Pentekoste ingeendelea, wangekuwa wamefanya nini?

261 Sasa kuna jambo moja pekee liwezalo kutokea. Inapasa kuwe na Ujumbe wakati wa mwisho, wakati hakuna chochote kingine kiwezacho kuufuata huo. Na sasa ulimwengu wa muungano wa madhehebu umeweka utawala kwamba hakutakuwa na dhehebu na hakuna chochote kingine kitaufuata; ama uko ndani yake au hauko ndani yake. Lile tunda liko kileleni pa mti, na Nuru inaliangaza lile tunda lililochaguliwa kimbele. Na linakomaa kuwa tunda lililofanana na Kristo, likileta ubivu ule ule na utamu ule ule, na Roho yule yule ambaye, Yeye alikuwa ndani Yake. Natumaini mnaliona! Unaona?

Na-najaribu kuweka mengi katika siku moja. Nawachosha. [Kusanyiko linasema, "Hapana."-Mh.].

262 Kwa hiyo, tazama walitekwa na fikira, walite kwa na fikira za kidhehebu kama "Ingewezekana niwe wa dhehebu hili! Me-Meya huwa anakwenda katika kanisa hili." Unaona? Kama ningeweza kuwa Mmethodisti au Mpresbiteri". Tazama tu kule walikokwenda. Sasa, nimeshaeleza tu, miguu imekuishapogolewa. Imekufa. Haikuunganishwa na Kristo tena; la sivyo wangekuwa wanaleta Uzima ule ule. Hakuunganishwa na Hilo.

Lakini wako kama tunda la mti wa jamii ya michungwa, milimao, ndimu n.k. laweza kuishi juu ya mti wa jamii ya mchungwa, mlimao, mndimu ila litazaa tunda lake lenyewe. Unaweka tunda mbalungi katika-katika mchungwa, litaishi kwa kutumia mchungwa, lakini litazaa mbalungi. Unaweka limao ndani pale, na tunda la jamii ya mchungwa, mlimao, mndimu, mbalungi, litazaa limao chachu la kizamani, ila linaishi kwa kupata uzima wake hapa. Na hili ndilo madhehebu yanalofanya kwa chini ya jina la kanisa.

Ni Bibi arusi ndiye Mti wa asili, yule Roho wa asili. Ufunuo hutoka kwa Kristo, si dhehebu. Kristo! Angalia.

263 Dhehebu linajaribu kufanya nini? Kujikuza lenyewe, kama Ibilisi. Wanajiita wenyewe"lile Kanisa, Bibi arusi." Ambapo, wapo katika Ufunuo 17, kama inavyonenwa, Bibi arusi wa uwongo. Juu ya kundi dogo la Kristo, Bibi arusi, Ibilisi hufikiri na kujiinua mwenyewe juu ya Neno nyenyekevu la Kweli ya Mungu kwa njia ya maarifa na ufunuo, na amejiweka mwenyewe kwa njia ya elimu ya seminari na thiolojia, hata wamejiweka wenyewe juu. Na kama hujawa katika kundi lao, basi wewe ni mtu mpotovu aliyekataliwa [Sehemu tupu kwenye kanda-Mh.]

264 Kama Ibilisi alivyofanya hapo mwanzo, aliwaambia watu kile tu hasa Ibilisi alichomwambia Hawa, "Hakika Mungu atatupokea! Tunawalisha maskini." Hilo ni jema. "Hakika atatupokea. Sisi ni dhehebu kuu. Sisi ni kanisa zuri. Mbona, hebu tazama majengo yetu makubwa. Tazama washirika wetu walivyo wengi. Tuko kwenye mamilioni. Hakika Mungu hataliacha lile kundi."

Jambo lile lile alilofanya Kaini, alileta matunda mazuri toka alikolima ardhini, na kujitahidi, na kufanya kazi, na kuleta matunda, na akakataa damu nyenyekevu ya mwanakondoo.

265 Mungu uwe na rehema, kwamba wanaume na wanawake hawatafikiri nalisema hili kukweza jambo fulani, au ufunuo fulani wa binafsi, au jambo fulani. Nawaambia tu ile Kweli. Je Hamwezi, kuona kile wanachofanya? Unaona? Mimi nanena hili kwa sauti kubwa na kali lakini yakupasa kupigilia msumari mpaka ukaze sana, ikiwa jambo hili linakwenda kukusaidia unaona, hadi ulione. Unaona?

266 Sasa, kusema kwa watu, "Hakika! unamaanisha kuniambia kuwa kanisa letu kuu la Katoliki, lililosimama wakati wote huu, letu kuu Methodisti na yote hayo? Tazama mababu zetu!" Unaona? Lakini walihalifu Neno la Bwana. Na Hawa alikuwa wa Mungu, mmoja wa walio Wake na ... yeye alikuwa zao la Adamu; na kwa sababu alitilia shaka Neno moja la Neno la Mungu, ilifanya hilo.

267 Na Ibilisi yupo hapa kwenye kazi yake tena, leo. Na, kumbuika, mpinga Kristo sio ukomunisti. Mpinga Kristo anakaribiana mno na kila jambo halisi mpaka ingeliwadanganya wale Wateule hasa kama ingewezekana. Yesu alisema, Mathayo 24 "Wateule kama ingewezekana". Ibilisi tena Ibilisi anavunja tena umoja wa Mungu katika mwanadamu, kwa kule kule kulifungia Neno la Mungu ndani ya mipaka ya mawazo yake. Kile anachofikiri hicho ni sawa, na kile anachofikiria kinahalifu Neno la Mungu.

Na alifanya jambo lile lile katika siku za Yesu. Naye Yesu akasema "Ninyi, kwa mapokeo yenu, mmefanya Neno la Mungu lisiwe na matokeo yaliyokusudiwa.

Na madhehebu, kwa mawazo yao yaliyopangwa kiakili, kimefanya Neno la Mungu lisiwe na matokeo yaliyokusudiwa juu ya watu. Hiyo ni sahihi. Hawawezi tu kuliona hilo. Ndipo wanasema, "Mungu wa Biblia yuko wapi?" Yuko hapa hapa. Yeye ni Biblia, hicho ndicho alicho Yeye.

268 Angalia sasa Ibilisi anakuja katika hila na kuharibu muungano wa Mungu kwa mwanadamu, kama tu alivyofanya katika Edeni, kwa majaribu makuu ya ahadi ya kupata madaraka binafsi ya kujiamulia mambo na fahari "Mbona, unaweza kuwa askofu ikiwa utakaa nasi tu. Unaweza kuwa kasisi wa jimbo. Kwa nini uende kwenye kitu kama Kile? Unaona? Hiyo ni Pentekoste, Katoliki na kadhalika; unaona, ahadi kuu ya udanganyifu kwa mwanadamu, kupokea uwezo nje ya Neno la ahadi ya Mungu. Unapokea Nguvu wakati Roho Mtakatifu amekuja juu yako, si unapokuwa askofu au shemasi, au chochote alichokuwa. Unaona? Lakini Ibilisi yuko kwenye kazi yake tena.

Je, Hili kanisa linaelwa hilo? Inueni mikono yenu ili nione hilo. [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Vema. Sitaendelea kulizungumzia.

Kuachana na kuwa mbali na Neno la Mungu. Unaona.

269 Alifanya hili hili pale Nikea, Rumi. Unajua Costantine aliwapa nini? Mlijifunza juu ya vipindi vyote vya Kanisa. Aliwapa... Hawakuwa na chochote, ila Kristo tu. Nao walikaa katika vijumba vidogo vidogo vya kizamani popote walikoweza kwenye sakafu za miamba migumu. Mnajua hilo kama umesoma kitabu cha "Baraza la Nikea" na "Kabla ya Baraza la Nikea" na Mababa wa Nikea, na kadhalika na historia ya kanisa. Hawakuwa na chochote. Lakini walipokuwa na hili baraza na kuingiza baadhi ya upagani wa Kirumi katika Ukristo, na kuweka mtu mtakatifu na maaskofu, na kadhalika, na mapapa na upuuzi huu wa aina hii, Costantine aliwapa nini? Namwuliza mwanathiolojia yeyote aniambie. Aliwapa mali. Aliwapa uhuru na yote yale waliyotaka.

Na walibadilishana wao kwa wao kulitoa Neno la Mungu na wakapokea hekima na utamaduni wa mwanadamu. Na hilo ndilo jambo lile lile Ibilisi alilofanya wakati ule yeye alilifanya katika bustani ya Edeni, na wao wakafa pale pale. Kanisa la Kipentekoste lilikufa pale Nikea, Rumi lakini lipate kufufuliwa katika Mti wa Bibi arusi mnamo siku za mwisho.

270 Angalia, Ibilisi anaingia, mwerevu, kama alivyofanya wakati ule, na kwa majaribu na ahadi za uwongo, za nguvu nje, mbali na Neno la Mungu. Alifanya hilo hilo pale Nikea, Rumi. Anafanya hilo hilo leo kwenye baraza la Makanisa Ulimwenguni.

Papa anasema, "Sote tuungane pamoja." "Nawataka ndugu zangu wote wanaopenda Muungano wa madhehebu yote y a Ukristo ulimwenguni kuungana na mimi. Sisi ni wamoja." Hiyo ni sahihi, katika mashirika ya dini ninyi ni wamoja. Lakini hilo halihusiani na Bibi arusi wa Kristo; kwa lolote lile, ndugu. Kamwe hutaweza

kumkokota katika kitu kama hicho.

271 Sasa imeahidiwa, katika siku za mwisho, kuwa ile Imani ya kwanza katika lile lile, ingerejeshwa kwa watoto wa Mungu wakati wa Mti wa Bibi arusi. Mungu alisema, Malaki 4, "Kabla dunia haijateketezwa kwa moto angalieni nitawapelekea Eliya nabii, naye atarejesha Imani ya watoto." Sasa, huyo hakuwa Eliya wa kwanza atakayekuja. Hapana, hapana.

Sasa, hapa hatufundishi kuhusu vazi la Eliya na mablanketi ya Eliya, na mambo yote hayo namna hiyo. Tunafundisha tu Neno la Mungu. Unaona? Hicho ndicho Yeye alichosema. Unaona, tunao namna zote za Eliya huyu na Eliya yule, ambayo ni upuuzi. Hiyo ni-hiyo ni ....Tunajua hilo. Yaani, sizungumzii juu ya hilo, na ninyi mlio wa kiroho mnaelewa. Unaona, kama ambavyo saa hii ya mwisho, inakwenda kuishia na siwezi kuyaweka yote kwenye hii kanda bila shaka.

Sasa, ile ahadi katika siku za mwisho, sasa ikiwa....

272 Yesu alisema, katika-katika Mathayo, naamini sura ya 11 au sura y a 6 na ile ya 11... Hapana, ni sura ya 11 na kama aya ya 6. Yohana alipotuma wanafunzi wake kule kuona kama yeye alikuwa Ndiye, Yesu akasema, "Mlikwenda nje kule kumwona nani? U-u-upepo... unyasi ukitikiswa na upepo? Mlikwenda kumwona fulani?" na fulani akasema , "Au mlikwenda kumwona nabii?" Akasema, "Aliye mkuu zaidi ya nabii," Yohana alikuwa zaidi ya nabii, alikuwa mjumbe wa Agano. Naye akasema, "Ikiwa mtaweza kulipokea, huyu ndiye aliyenenwa na manabii, Nitamtuma mjumbe Wangu mbele y a uso Wangu."

Sasa, hili liko katika Malaki 3, Si Malaki 4 Kwani yule Elisha aliyekuwa aje katika Malaki 4, dunia ilikuwa iteketezwe kwa moto wa tanuru, na wenye haki walikuwa watembee katika utawala wa miaka elfu wa Kristo juu ya majivu ya waovu. Unaona? Kwa hiyo si hilo. Unaona?

273 Sasa tunaona ahadi ikitimizwa. Kristo, Ukuu wa kweli akiingia, akija ndani ya Bibi arusi Wake, akifanya kazi zile zile alizofanya hapo mwanzo na kufanya tayari na kutimiza Neno lake kama alivyofanya, hapo kwanza, katika Yohana 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya." Ndipo, Kichwa na Mwili vinafanyika kuwa Mmoja katika kazi na katika ishara na katika Uzima, vikithibitishwa na Mungu Mwenyewe kwa njia ya Neno Lake la ahadi kwa ajili ya siku za mwisho. Yeye aliahidi hili katika siku za mwisho. Basi, ikiwa wewe ni wa kiroho utalidaka hili.

274 Basi, twaweza kuona kuwa ile Karamu ya Arusi i karibu. Sasa kama sitaonana nanyi tena, kumbukeni, karamu ya Arusi i karibu. Na ndipo ule Ufalme kutokana na ahadi uko tayari kuletwa, ule utawala mkuu wa Kristo wa Miaka elfu, kuchukuliwa juu kwa Kanisa, na kuangamizwa kwa waovu. Na dunia chini ya Muhuri wa Sita, itasafishwa kwa volkeno, kutoa uharibifu na dhambi ya ulimwengu na kuufinyanga tena, na kuleta utawala mpya wa Kristo wa miaka elfu unaong'aa kwa ajili ya kipindi kitakachokuja.

Wakati tunapoona yote haya, ufunuo mkuu wenye awamu tatu Mungu katika Kristo; Kristo katika kanisa; ule Ufalme ukija. Adamu na Hawa wamekombolewa na kurudi Bustani ya Edeni, katika onyesho la Kristo na Bibi arusi Wake, na ndipo ule Ufalme unakwenda kurejeshwa kufuatana na ahadi Yake. Mungu asifiwe! Sasa, kwa ufunuo wa lile fumbo lenye awamu tatu, ile siri, na kwa Neno lililothibitishwa binafsi kwa Ukuu Wake wa mwanzo.

275 Sio kusema, "Vema, utukufu kwa Mungu, tunapiga kelele, haleluya, tunaimba." Hilo, hilo silo lenyewe. Mimi ni mmisionari, nimesafiri kuzunguka ulimwenguni mara saba. Unaona? Nimewaona wapagani, mashetani na kila kitu kingine wakicheza na kupiga kelele. Nimeona, namna zote za madhihirisho ya kimwili. Hiyo ni kimwili.

276 Lakini mimi naongea kuhusu Ukuu wa Kristo. Angalia, akiwa ametambulishwa binafsi na ule Ukuu wa kwanza, tunalo jibu kwa swali la shetani. Amina! Utukufu! Tunalo jibu kwa swali la shetani. Yeye, Kristo, amefufuka na amelipa thamani, na kufufua Kichwa... au ule Mwili.

Shetani hawezi kuvumilia hili. Hiyo ndiyo sababu hizi falme za muungano wa madhehebu yote ya Ukristo zinaundwa. Hiyo ndio sababu wote wanakuja katika kile wanachokifanya sasa. Hiyo ndio sababu shetani anapiga kelele jinsi hiyo. Uovu wake umekuwa.... Hila zake zimefunuliwa na Kristo aliyefufuka katika Ukuu juu ya Mwili Wake. Utukufu!

277 Mnadhani nimerukwa na akili? Sivyo. Tunalo jibu kwa shetani. "Sio mimi ninayeishi,

ila Kristo aliye Neno akiishi ndani yangu.” Si wazo langu; ni Uwezo Wake. Si wazo langu; ni Neno Lake. Yeye aliahidi hilo liko; hapa. Yeye alisema lingekuwa hapa, na hili liko hapa. Tunalo jibu lake.

Kristo amefufuka na amelipa thamani kwa ajili ya ukombozi wetu. Kile Mungu alichodhihirisha katika Kristo, Yeye alikipa ule mwili, hicho na damu, ili katika ile damu uweze kuja Uzima, na mwili ukombolewe, ili-ili Mungu katika huu mwili uliokombolewa aweze kudhihirisha Neno Lake kwa ajili ya hii siku kama alivyofanya katika ile siku. Loo! Utukufu!

Mnaliona? [Kusanyiko linasema, “Amina.”-Mh.] Lo, jamani! Nitamaliza wakati gani? Liangalieni. [“Endelea!”]

278 Basi, tunasimama katika Uwepo wa Mungu tuliohesabiwa haki. Kama tone la wino linalodondoka katika pi-pi-pipa lililojaa dawa inayoondoa madoa kamwe hutakuta doa la wino tena. Lilikwenda mahali fulani. Kamwe halitarudi tena. Na mtu anapokombolewa kikweli kweli, ile Mbegu iliyochaguliwa kimbele ile inayoliona na kulipokea, dhambi zake zimeangamizwa. Zimeondoka. Zimetengwa. Zimedondoshwa katika wino wa ile-wa ile Damu ya Yesu Kristo, na kamwe hazitakumbukwa. Mungu anazisahau. Na yeye anasimama kama mwana na binti wa Mungu, katika Uwepo wa Mungu. Amina na amina! “Sasa tu wana wa Mungu.” Sio tutakuwa; tu wana! Sasa tumekombolewa.

279 Tunalo jibu kwa shetani. Mungu amejithibitisha Mwenyewe. Mungu anajihakikisha Mwenyewe, kwa ahadi Yake katika siku hii. Haleluya! Ukuu uko hapa Amina! Kristo, Bwana aliyefufuka yupo hapa katika Uwezo ule ule wa ufufuo Wake ambao Yeye amekuwa tangu asili akijidhihirisha Mwenyewe. Hilo hapo jibu kwa shetani.

280 Hiyo ndio sababu wakati huyu mtu aliyekaa hapa, siku ile, alipoanguka chini na kufa, wakati alikuwa ameketi hapa, basi tuliweza kusema, “Uzima rudi!”- Kwa sababu ni Roho Mtakatifu alisema hivyo.

Hiyo ndio sababu Aliweza kumtendea hivyo yule mtoto mdogo kule Mexico, alikuwa amekufa kwa karibu masaa kumi na matano, ono lilipokuja na kusema, “Mwite huyo arejee kwenye 'kifo', ”Uzima.“ Na kusema, Hebu huyu mtoto mdogo na aishi.” Na yule mtoto mdogo ambaye madaktari waliandika taarifa, alikufa saa tatu asubuhi ile, na saa tano usiku ule akarudia uhai; anaishi leo.

281 Ni kitu gani? Si wale watu. Ukuu na ule mwili wamekuwa kiungo kimoja. Ni Mungu aliyedhihirishwa katika watu Wake. Hiyo ndiyo sababu mume na mke si wawili tena, ni mmoja. Mungu na Kanisa Lake ni mmoja. “Kristo ndani yenu,” ufunuo mkuu wa Mungu. Atukuzwe Mungu! Hata kuchukua Jina Lake; Jina Lake ni Yesu, Mpakwa Mafuta. Sababu ya Yeye kuitwa Yesu, Yeye ni Mpakwa Mafuta. Ni Mwili wa Kristo uliopakwa mafuta, ukihakikisha, uliodhihirishwa, unaofanana na Mungu, mwili Huo ulivyokuwa. Na ule mwili alikomboa kila moja ya hii, hii miili, na kupitia pale Mungu hufanya udhihirisho Wake wenye awamu tatu, kwenda kwenye Ufalme. Kwa kufufuka, alilipa gharama! Tumekombolewa. Mungu amelihakikisha, na kulithibitisha. Unaona.

282 Na tunasimama mbele Yake tukiwa tumehesabiwa haki katika Kristo. Kwa sababu Yeye hawezi kupitisha hukumu, kwani Yeye tayari ameshauhukumu ule Mwili, ambao mimi ni sehemu yake. Vipi, jinsi gani mimi ni sehemu yake? Lipo hapa; Liko ndani yangu. “Kama Yangu .... mkikaa ndani Yangu, na maneno Yangu ndani yenu, basi kile mnachosema... ombeni Baba lolote katika Jina Langu, litafanyika, kwa sababu Liko pale”. Umehesabiwa haki! Atukuzwe Mungu.

283 Lo, Laiti kama ningeweza kufanya ulimwengu ulione hilo! Kwa nini? Ndilo hilo. Mwili wa Kristo uko pale ukiishi, ukiwa kwenye nafasi yake kuwa umekombolewa. Uliokombolewa! Lo, jamani!

Tumehesabiwa haki machoni Pake. Kwa nini tumehesabiwa haki? Sisi ni ushindi Wake. Kanisa ni ushindi Wake. Tunakuja katika hizi siku za mwisho pamoja na Injili hii tukufu tukionyesha ushindi Wake. Alikufa kwa ajili ya hili kusudi, nasi ni uthibitisho wa ushindi Wake. Amina! Tunapomwona Yeye akishuka na kuishi miongoni mwa Kanisa, huo ni ushindi Wake. Inaonyesha kuwa asingeweza kumshikilia Yeye kaburini, wala hawezi kutushikilia sisi. Hiyo ni sahihi. Yeye...?... Nasi tayari, kimsingi tumefufuliwa, kwa sababu tumefufuka kutoka kwa wafu, kutokuamini Neno Lake, kutoka kanuni za imani za madhehebu, kwenda kwenye Neno la Milele la Mungu wa Milele; ambalo ni Yeye, Yeye Mwenyewe akitenda kupitia sisi akijidhihirisha Mwenyewe kuwa Yeye ni yule jana,

leo na hata milele.

284 Na ndipo Neno linashuka chini katika Mwili, toka kwenye Kichwa. Ni kitu gani? Neno hili hili. Hakuna kiwezacho kuongezwa au kuondolewa kutoka Hilo. Kwa hiyo Neno lile lile linatembea toka Kichwani, jinsi ile Siku inavyokaribia, mpaka chini kwenye Mwili, mpaka chini kwenye Mwili, likithibitisha kuwa hao ni Mmoja. Wao ni Mume na Mke. Wao ni nyama ya nyama Yake, Neno la Neno Lake; Uzima wa Uzima Wake, Roho wa Roho Wake. Unaona? Amina! Unalijuaje? Linashuhudia, tunda lile lile, Neno lile lile. Unaona, linamdhihirisha Kristo; Uzima ule ule, Mungu yule yule, Roho yule yule, Neno lile lile, Kitabu kile kile! Amina! Ishara zile zile. "Mambo yale niyatendayo, ninyi nanyi mtayafanya pia" Lo, haleluya! Jamani!

285 Angalia. Neno lililothibitishwa katika Mwili Wake ndiyo ule ushindi Wake halisi na sababu ya kifo Chake, Unaona, kifo, si katika Roho Wakati Yeye alipokufa, Yeye alikufa tu katika mwili. Roho Wake alikwenda kuzimu na kuzihubiria nafsi zilizoko kifungoni. Hiyo ni sahihi. Mwili Wake, pekee ulikufa, ndipo Yeye akaufufua tena na kuuhuisha. Huisha maana yake kufanywa hai," nyama Yake ambao ulikuwa ndio mwili Wake. Na hilo ndilo Neno. Lilikuwa limekufa kwa miaka, lakini, kidogo kidogo lilianza kuja katika kipindi cha Matengenezo ya Kanisa na sasa amesimama juu ya miguu Yake

286 Lo, natamani jinsi gani ningekuwa na wakati nirudi katika Ezekieli, na kuvuta nje ile "mifupa mikavu," na kuwaonyesha. Alisema, "Je mifupa hii yaweza kuishi?"

Akasema, "Toa unabii!"

Unabii utakujaje? Kupitia nabii pekee. Ni Neno la Mungu. "Enyi mifupa mikavu, lisikieni Neno la Bwana!" Na mishipa, ngozi ikaja juu yao, nao wakasimama jeshi lenye nguvu mno. Na kuanza kwenda kuelekea Sayuni. Atukuzwe Mungu! Huyo ni Yeye. Huyo ni Yeye, ule ushindi.

Waliokombolewa na Bwana watakuja Sayuni kwa shangwe, wakati huo.

Milima Yake mitakatifu yote, hakuna kitakachodhuru au kuangamiza

Naam.

287 Basi Yeye anahakikisha Uzima wa ufufuo Wake hapa kama anavyojithibitisha Mwenyewe. Yeye, Bibi arusi, yuko huru mbali na wengine wote Yeye ni Mwanamke aliye huru, ndege Mkuu mwenye madoadoa aliye tofauti na wengine wote. Mnakumbuka Biblia juu ya hilo? "Ndege mkuu mwenye madoadoa." Ila, Yeye alikuwa na Jina Lake, Yeye alikuwa na Uzima Wake. Kwani .....

Walimwekaje huyo ndege madoadoa? Wote wawili walikuwa weupe, na ndipo walimng'oa ndege mmoja kichwa na kumtoa damu yote na kuiweka juu ya yule mwingine. Naye yule ndege mwingine akapata madoadoa kwa damu nyekundu, na kupigapiga mabawa yake hivi, na damu ikalia, "mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu," ilipokuwa ikilowesha ardhi.

Kwa hiyo Kristo, Rafiki aliyekufa, aliweka Damu Yake, Damu yake kutoka kwenye uzima Wake ndani yetu; akanyu-... akichukua Damu Yake, akilia, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana!" Ni ndege anayeonekana wa kipekee. Hakika, ndivyo. Lakini Yeye, Bibi arusi, anaanatambuliwa na Yeye, naye yu huru mbali na wengine wote. "Uwe na Yeye peke yake wakati wote ninyi wawili mnapokuwa hai. Ukae na Yeye peke Yake, yule Neno" hakuna, hakuna uzinzi, hakuna ishara hata moja ya dhehebu, hakuna ishara hata moja ya kanuni ya imani, hakuna uzinzi hata kidogo. Lile Neno, na Yeye peke Yake!

"Nasimama juu ya Kristo mwamba imara, ardhi nyingine yote ni mchanga unaodidimia" alisema Eddie Perronet. Aha-aha.

288 Hilo ndilo, Kristo aliye Neno! Yeye alikuwa Neno; Yeye ni Neno. Na Kanisa linakuwa Neno, kwa Yeye kulifanya hilo kuwa sehemu Yake, na hilo Ndilo Neno tena. Linatambulika kibinafsi na Yeye, mali Yake Mwenyewe, Mali Yake Mwenyewe. Limekombolewa na Yeye kwa njia ya Yeye, kwa ajili Yake, na kwa ajili Yake Mwenyewe. Hiyo ni sahihi Basi kile shetani anachopigia kelele, kuwa hili linafunuliwa.

289 Tuko katika wakati wa hatari. Kumbuka Andiko linasema "Wakati mambo haya yaanzapo kutukia hakuna wakati tena." Kanisa linafifia, tunapoona udhihirisho.

"Matetemeko ya nchi." mliona wale elfu waliokufa siku ile nyingine ' Matetemeko ya ardhi katika sehemu mbalimbali.

Kasema, "Vitu vinavyotisha angani, nguzo za moto," vikielea kama visahani vikielea angani. Hawajui ni kitu gani. Unaona? Hawajui lolote kuhusu hayo.

290 Mliona Malaika wale walioshuka, wakaichunguza Sodoma kabla

Sodoma haijaangamizwa? Mnakumbuka hilo? [Kusanyiko, "Amina.-Mh.]

Kulikuwa na kundi lao lililoshuka chini, watatu. Mmoja wao alikaa na Abraham. Mnakumbuka hilo, ["Amina."] Walikuwa Nuru kutoka Mbinguni, zilizoshuka katika upelelezi wa hukumu. Mmoja ni ....

Tazama mahali ambapo wanapatikana wote. Kule Pentagon, na mambo hayo wanawakuta. Hiyo ni hukumu ya ulimwengu, Sodoma. Na kuna Mmoja aliyewakilishwa, atawakilishwa miongoni mwa makanisa, atakuwa Kristo Mwenyewe, akijithibitisha Mwenyewe. Unaona? "Vitu vinavyoonekana kwenye.... juu mbinguni, na ishara chini duniani." Hakika.

Alitambulika!

291 Lo, shetani anapiga kelele juu ya hili. Kweli iliyodhihirishwa ya ahadi ya Neno ndani ya Bibi arusi.

Wao hawana jibu. Yesu alipokuja, kwa nini wale Mafarisayo? Akasema, "Ikiwa natoa pepo kwa kidole cha Mungu, ninyi huwatoa kwa kutumia nini?" Unaona? Yeye alisimama peke Yake.

Na Kanisa Lake husimama peke yake. Halifungamani na chochote. Ila Yeye alitambulishwa na Mungu, akiwa ule mwili ambao Mungu alikaa ndani yake; na Kanisa limetambulishwa na Mwili Wake, likifanya jambo lile lile.

Hilo ni Mwili Wake., Kweli iliyodhihirishwa na Neno Lake linaloahidiwa kwa ajili ya siku za mwisho. Na Hilo, na Hilo peke Yake, linasimama katika Hilo Neno. Hiyo ndio sababu Shetani anapiga kelele, haya mashirika makubwa ya dini kuweka jambo fulani ili kumfungia Yeye. Kamwe hawatalifanya. Yeye atachukuliwa juu, si kufungiwa. Yeye ameshafufuka sana, na kwa nguvu za Neno lililothibitishwa aliloahidiwa Bibi arusi. Amina.

292 Jinsi gani Bibi arusi anavyoshikilia ile ahadi! "Yeye aliniambia kuwa Yeye angerudi kwa ajili yangu. Nitaliamini hilo." Aha-aha. Unaona? Naam, bwana. Akutane na Ukuu Wake, Mkombozi Wake, Mume Wake, Mfalme Wake, Bwana Wake, Mpenzi Wake, Mwokozi Wake, kwenye mahali

palipoandaliwa pa kukutania

Yeye anapo mahali pa kukutania nao. Unajua, Yeye... Naam, Bwana arusi, haachi chochote. Yeye ana pete, ule utambulisho. Yeye analo vazi rasmi ambalo Bibi arusi anavaa, nguo Zake. Unaona? Naye ana mahali palipoandaliwa kukutana na Bibi arusi ambako ni hewani. Kila kitu kimeandaliwa. Karamu ya arusi tayari imeshatayarishwa; wageni wameshaalikwa, wameshachaguliwa. Malaika wote wamesimama pale, watumishi wake, wako makini . Lo-lo-lo-lo-lo!

Lo, kutakuwa na kusanyiko hewani,

Baadaye katika ule uzuri

Nitakutana nawe, nitakutana nawe Kule

Nyumbani kule nyuma ya wingu;

Kuimba kutakowahi kusikika daima Kusikowahi sikika na masikio yapatikanayo na mauti Nasema itakuwa ya utukufu! Naye Mwana wa Mungu Mwenyewe, ataongoza, udhihirisho kamili wa Mungu, Kwenye lile kusanyiko hewani. Lo, jamani!

Tazama uthibitisho Wake sasa.

Mmesikia-sikia hadithi ya Musa katika nyasi,

Umemsikia Daudi jasiri na kumbeo lake;

Umesikia habari ya Yusufu akiota,

Ya Daniel na simba tunayoimba mara kwa mara.

Lo, kuna wengi, wengine waliothibitishwa katika Biblia,

Nasema, hata lini tukutane nao wote Halafu Bwana ataturuhusu kukutana nao,

Kwenye lile kusanyiko hewani.

Kwani kutakuwa na kusanyiko hewani

Baadaye katika ule uzuri; Nami nitakutana nawe, kukusalimu Kule Nyumbani kule nyuma ya wingu. Kuimba kutakakowahi kusikika, kusikika daima kusikowahi sikika na masikio yapatikanayo na mauti.

Nasema itakuwa ya utukufu! Naye Mwana wa Mungu Mwenyewe, ataongoza, Kwenye lile kusanyiko hewani. Lo, jamani!

293 Je, unalipenda hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Sasa kusudi lenye awamu tatu la siri Yake kuu ya ufunuo limefunuliwa. Yeye ndiye Mkuu. Huyo Ndiye. Lo. jamani! Hebu tuimbe. Siwezi kuhubiri zaidi. Najisikia vizuri mno, unaona.

Lo, kutakuwa na kusanyiko hewani

Baadaye katika ule uzuri,

Nami nitakutana nawe, kukusalimu Kule

Nyumbani kule nyuma ya wingu; Kuomba kutakowahi kusikika daima na masikio yapatikanayo na mauti Nasema itakuwa na utukufu! Naye Mwana wa Mungu Mwenyewe, ataongoza Kwenye lile kusanyiko hewani?

Mnakwenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." -Mh] Amina Kwa neema ya Mungu, kwa neema ya Mungu! Unaona? Lo, jamani.

Mmesikia ya mtoto Musa katika nyasi,

Mmesikia ya Daudi jasiri na kombeo lake;

(yote ni mifano)

Mmesikia hadithi ya Yusufu akiota,

Na ya Danieli na simba tunayoimba mara kwa mara

Lo, kuna wengi, wengine katika Biblia

(ambayo ni Yeye)

Nasema itakuwa ya utukufu! Naye Mwana wa Mungu Mwenyewe, ataongoza Kwenye lile kusanyika hewani.

Ila kuna mkuu Mmoja!

Lo, kutakuwa na kusanyiko hewani, Baadaye katika ule uzuri nami nitakutana nawe, kukusalimu kule

Nyumbani kule nyuma ya wingu;

Kuimba kutakakowahi kusikika kutasikika na masikio yapatikanayo na mauti.

Nasema itakuwa ya utukufu! Naye Mwana wa Mungu Mwenyewe, ataongoza Kwenye lile kusanyiko hewani.

294 Sasa, tunakwenda kukutana kule. Hebu sote, Wamethodisti, na Wabaptisti, na chochote ulicho, ulizaliwa upya kwa Roho wa Mungu, shikaneni mikono tunapoimba.

Lo, kutakuwa na kusanyiko hewani,

Baadaye katika ule uzuri

Nami nitakutana nawe, kukusalimu Kule

Nyumbani kule nyumba ya anga;

Kuimba kutakakowahi kusikika kutasikika na masikio yapatikanayo na mauti

Nasema itakuwa ya utukufu! Naye Mwana wa Mungu Mwenyewe, ataongoza Kwenye lile kusanyiko hewani.

Lo-lo-lo, hilo ni zuri, unaona, unaona kile Yeye atakachokuwa. Sasa tazama

295 Tunapaswa kufunga, marafiki,. Inakaribia saa nane, unaona, na tuta-tutakuwa hapa kwenye chakula cha jioni. Nina ukurasa baada ya ukurasa wa hilo bado, unaona, kwa hiyo tunakwenda kufunga kwenye hili. Kwa hili hakuna mwisho.

Ni ufunuo. Ni wa Milele kama Neno la Mungu lilivyo la Milele. Tazama ila kusudi

lenye awamu tatu la siri kuu ya Mungu limefunuliwa! Mungu alidhihirishwa katika Kristo; Kristo alidhihirishwa katika Kanisa, ili kumkomboa Hawa aliyepotea na kumrudisha kwenye hali ya asili katika bustani ya Edeni. Lo, jamani!

Lo, kutakuwa na nyakati kuu katika Siku ile! Naam. Ni moja kwa moja Tunaliamini. Je, hmliamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Nafikiria tu kuhusu ule wimbo wakati wote ninapofikiria juu ya hilo.

296 Yeye alijithibitisha Mwenyewe ndani ya Danieli, na ndani ya Musa, na ndani ya Yeremia. Wao walikuwa akina nani? Manabii ambao Neno lilikuja kwao, unaona, watu wakuu. unaona, umesikia hadithi iliyosemwa na Yusufu akiota ndoto, unaona, na Danieli katika tundu la simba, na hao wengine wote, unajua. Wao, wale walikuwa nani? Manabii. Unaona? Lakini yule mkuu Mmoja... Mungu alikuwa tu, kwa kitambo, mfano ndani yao.

Yeye Mwenyewe alikuwa mfano ndani ya Adamu, akijua kile kilicho sahihi lakini alitoka kwenda kumkomboa mke wake, kwa sababu alikuwa amekosea. Kristo haikumlazimu kufanyika dhambi, ila Yeye alitoka na kuchukua dhambi, amkomboe mtoto Wake aliyepotea. Unaona. Unaona? Yeye alikuwa mfano kujihusu Mwenyewe.

Na Musa katika nyasi

Nawe umesikia juu ya Daudi jasiri na kombeo lake;

Umesikia hadithi ya Yusufu akiota, yule nabii, Na ya Danieli na simba tunayoimba mara kwa mara.

Lo, kuna wengi, wengine katika Biblia.

Na mimi...

Wao, wao ni Biblia. "Na mimi ..." Wote walidhihirishwa ndani Yake hata hivyo. Unaona? Bila Yeye, wote wamepotea. Unaona? Nami yanipasa kuwa sehemu ya Hilo, kuwa Yeye. Amina! Unaona?

Nasema natamani kukutana nao wote

Hiyo ni sahihi

Ila Mwana wa Mungu Mwenyewe, atakuwa Ndiye ataongoza.

Kwenye lile kusanyiko hewani.

297 Waebrania 11, ilisema, "Wasingekamilika bila sisi." Mikono na miguu haiwezi kukamilika bila ubongo, maarifa, kichwa, na kadhalika. Unaona? Na sote tunakamilishwa katika Yeye. "Kwa hiyo kwa Roho mmoja tunabatizwa sote katika Mwili mmoja," huru toka Hukumuni, kutoka dhambini, katika kifo... Amina! Mwana na Mungu Mwenyewe ataongoza kwenye lile kusanyika hewani. Je Mnapenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.].

Nampenda, nampenda Kwani ...

Bwana Yesu, upako wa Roho Mtakatifu uje juu ya hizi leso, Bwana, na uwaponye wagonjwa.

298 [Sehemu tupu kwenye kanda-Mh.] ... Sasa hivi ndani yetu. Jinsi gani Yeye, Yeye alifunuliwaje? Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza. Yeye alifanya nini?

Akanunua wokovu wangu Juu....

Atukuzwe! Yule Malaika mkuu wa Agano, yule Ambaye alikuwa na Musa Jangwani, yule Ambaye alimjia Paulo akielekea Dameski, yule yule aliyeruhusu picha Yake ipigwe na sisi; yule yule Ambaye alikuwa katika picha, katika gazeti la Life siku ile. Neno lile lile, kwa Mungu yule yule katika mapito yale yale, kwa njia ile ile kwa ahadi ile ile! Popote wakutanikapo wawili au watatu kwa Jina Langu, nami niko katikati yao". Basi Yeye yupo hapa. "Malaika wa Mungu huweka vituo kwa wale wanaomcha" wale wanaolishikilia Neno Lake pekee. hakuna mtu awezaye kuliheshimu lile Neno bila kumcha Mungu. Unaona? Ndipo, hapa yeye yupo hapa asubuhi hii, pamoja nasi, tunapomwabudu katika Roho.

299 Lo, baada ya Ujumbe mgumu kama huu, nafikiri tunapaswa tu kumwabudu Yeye kidogo katika Roho. Unaona, fumba tu macho yako na tumwimbie huo tena, "Nampenda, nampenda," mnapo-mnapoinua mikono yetu, kama Kwake.

Nampenda, nampenda

Sababu.... alinipenda kwanza Na akanunua wokovu wangu

Pale Mtini Kalvari

Lo , jamani, jinsi tunavyompenda!

Imani katika Baba, imani katika Mwana, Imani katika Roho Mtakatifu, hawa watatu ni mmoja; Mapepo watetemeka, na wakosaji wanaamka.

Imani katika Yehova inatingisha kila kitu.

300 Amina! Atukuzwe Mungu! Tunavyompenda! Mwabudu tu moyoni mwako sasa mpende Yeye tu, waza tu jinsi Yeye alivyofanya vyema. Tazama kile alichotufanyia. Miaka yote hii ya maono. Hakuna hata moja lililoshindwa. Kila moja Yeye alilosema lingetukia, lilikuja sawasawa tu jinsi Yeye alivyosema.

301 Nawapenda, Msisahau amri za Mungu kwenu, watoto wadogo, "Pendaneni ninyi kwa ninyi" Mpende kila mtu. Aliye sahihi na mkosaji, mwenye dhambi na mtakatifu wapende, vyovyote vile. Iwapo huwapendi, basi mwombe Mungu akusaidie, kwa sababu Mungu alimpenda mwenye dhambi. Na asili ya Mungu iko ndani yako. Ikiwa mtu amekosea, mpende kwa vyovyote vile. Usishiriki dhambi zake Unaona? Usishiriki dhambi Lakini kwa upendo si katika uchungu na kukaripia, katika upendo mwambie juu ya tumaini la uzima likaalo ndani yako kwa njia ya Yesu Kristo akifunuliwa kwako na Roho Mtakatifu.

Peleka Jina la yesu

Mtoto wa huzuni na shida

Litafurahisha na kukufariji Lo, lichukue, usisahau sasa, popote uendako.

Lo, thamani, lile Jina! Lo, tunalo Jina Lake.

Tumaini la dunia na furaha ya Mbingu Jina la thamani, tamu mno!

Tumaini la dunia na furaha y a Mbingu.

302 Sasa nakwenda kuwapa siri ndogo, mpaka nitakapoonana nanyi tena. Kumbukeni hili, tunaposimama. Kumbukeni hili.

Kwa Jina la Yesu ninainama

Nikianguka kifudifudi miguuni Pake Mfalme wa Wafalme mbinguni tutamvika taji Yeye! tutamvika taji Yeye.

Wakati safari yetu ikikamilika

Jina la Thamani, Jina la Thamani Ee ni Tamu mno!

Tumaini la...

Nini? Ufunuo wenye awamu tatu! Tumaini na furaha ya Mbinguni, imefunuliwa ndani Yake.

Jina la thamani, Jina la thamani, Ee ni tamu mno!

Tumaini la dunia na furaha ya....

303 Nini? Tumaini la dunia na furaha ya mbinguni, kila kitu kimedhihirishwa katika Kristo Mungu, Kanisa kila kitu kingine, kimedhihirishwa ndani ya Kristo. Biblia ni Kristo. Biblia ni Neno lililoandikwa. Ambalo, Yeye ndiye Neno. Udhihirisho Wake ndio ushahidi wa ule Uzima unaokuja katika mwili wa lile Neno, ili kulidhihirisha Hilo. Ee, je hili si zuri mno!

Peleka Jina la Yesu na ....

Sasa sikiliza kwa makini sasa.

Kama ngao (usisahau hilo sasa).... kila mtego;

Wakati majaribu yatakapokuzunguka, … Unatakiwa ufanye nini?

Lilia Jina hilo takatifu katika maombi

Jina la thamani, Jina la thamani Ee tamu mno! tamu mno!

Jina la thamani, Jina la thamani

Jina tamu mno, Ni tamu mno

Tumaini la dunia na furaha ya Mbingu.

304 Bila kujua ... Bila shaka, ukiwa wa kiroho, unatazama mambo ya kiroho. Bila kujua hili; Mungu analijua. Lakini kama ukigeuka na kutazama saa iko kwenye doti, saa nane, mwisho wa Mvuto wa Pili. Mvuto wa Tatu u karibu! "Unaona?

Mbele ya Jina la Yesu najiinamisha,

Naanguka kifudifudi miguuni Pake

Mbinguni tutamvalisha, Taji Yeye,

Ndiye Mfalme wa wafalme Safari yetu itakapokwisha.

Jina la Thamani …

Mvuto wa Pili umedhihirishwa

Tumaini la dunia na furaha ya Mbingu; Jina la Thamani tamu mno!

Tumaini la dunia na furaha ya Mbingu.

305 Je, mlimwona Roho alichukua wimbo huu huu na kuchambua sauti nane juu zaidi namna hiyo? Mvuto unaofuata u karibu! Amina! Aha-aha.

Peleka Jina la Yesu,

Siku zimepita kuliko unavyofikiri

.... huzuni na taabu;

Itafurahisha na kukufariji,

Lo, peleka kokote uendako.

Jina la Thamani Jina la Thamani, Tamu mno!

Tumaini la dunia na furaha ya Mbingu; Jina la Thamani na Tamu mno!

Tumaini la dunia na furaha .....

Kama majaribu yakija, unafanyaje? Peleka Jina la Yesu

Liwe ngao kwa kila mtego; Wakati majaribu (ya kitu cha kukufanya kutokuamini sasa) yakija

Kumbuka tu, lilia lile jina takatifu katika maombi

Jina la Thamani na tamu! mno!

Tumaini la dunia na furaha ya mbingu;

Jina la Thamani, Jina la thamani, Tamu mno!

Tumaini la dunia na furaha ya mbingu.

306 Tuinamishe vichwa vyetu sasa, kila mtu, kwa kicho. tazama sasa.

Kwa Jina la Yesu nikiinama .....

[Ndugu Branham anaimba mstari mwingine wa Peleka Jina la Yesu. ndugu fulani anaanza kunena kwa lugha. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu mwingine anafasiri-Mh.].

Sasa kama unaelewa, Roho wa Bwana alishuka kwenye mkutano juu ya lugha zisizojulika akanena kwa mtu asiyejua; kulifasiri na mtu mwingine asiyelijua. neno la Bwana. Mnakumbuka adui alipokuwa anakuja na hawakujua wangefanya nini? Roho wa Bwana alimshukia mtu, na akafunua kile kilichopasa kufanywa.

Tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa unyenyekevu. Mungu awabariki.

Hata tuonane! hata tuonane! Hata tuonane miguuni pa Yesu; Hata tuonane!

Vema, mchungaji.

Mungu awe nanyi mpaka tuonanapo.

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7